# JIMBO LA MAINE

# KITUO CHA UTUNZAJI WA WATOTO
# KANUNI YA LESENI

## VITUO VYA KUTUNZIA WATOTO, SHULE ZA CHEKECHEA, TAASISI ZA UTUNZAJI WA WATOTO, MIPANGO MINGINEYO

## 10-148 KANUNI YA SHERIA ZA MAINE
## SURA YA 32


**Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya Maine**
**Ofisi ya Huduma za Watoto na Familia**
**11 State House Station**
**Augusta, Maine 04333-0111**


**Tarehe ya Kutumika:**
**Tarehe 27 Septemba, 2021**

## Jedwali la Yaliyomo


**1. KAULI YA AZIMIO NA FASILI ..... 1**
- A. Kauli ya azimio ..... 1
- B. Fasili ..... 1

**2. MASHARTI NA TARATIBU ZA KUPEWA LESENI ..... 8**
- A. Kupewa Leseni ..... 8
- B. Ustahiki wa mwombaji na mkurugenzi ..... 9
- C. Maombi ..... 10
- D. Uchunguzi wa kina ..... 11
- E. Aina na kipindi cha leseni ..... 11
- F. Usimamizi ..... 12
- G. Mabadiliko ya leseni ..... 17
- H. Ondoleo ..... 17

**3. ADA ..... 18**
- A. Ada ..... 18
- B. Ada za taasisi zinazowahudumia Watoto 3 hadi 12 ..... 18
- C. Ada za taasisi zinazowahudumia Watoto 13 au zaidi ..... 18
- D. Ada za Shule za Chekechea ..... 18

**4. UKAGUZI NA UCHUNGUZI ..... 19**
- A. Ukaguzi ..... 19
- B. Haki ya kuingia ..... 19
- C. Vipengele vya ukaguzi ..... 19
- D. Ripoti ya ukaguzi ..... 20
- E. Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa ..... 20
- F. Uchunguzi ..... 20

**5. REKODI USIMAMIZI NA UHIFADHI ..... 21**
- A. Rekodi usimamizi ..... 21
- B. Kutunga rekodi ghushi ..... 21
- C. Ukaguzi wa rekodi ..... 21
- D. Rekodi za watoto ..... 21
- E. Rekodi za wahudumu. Rekodi ya wahudumu sharti iwekwe kwa Wahudumu wote wa Utunzaji wa Watoto ..... 23

**6. MASHARTI YA KURIPOTI ..... 25**
- A. Mabadiliko ya utunzaji wa watoto ..... 25
- B. Ripoti ya lazima ya tuhuma za Kuwanyanyasa na/au kuwatelekeza watoto ..... 25
- C. Kuripoti kwa Idara matokeo mabaya ya maji ya kunywa ..... 25
- D. Kuripoti kuharibika kwa mfumo wa maji machafu ..... 25
- E. Kuripoti kuhusu hatua za kisheria ..... 25
- F. Taarifa nyinginezo ..... 26

**7. UWIANO WA WAHUDUMU NA WATOTO, USIMAMIZI NA USTAHIKI ..... 28**
- A. Watoto wa umri wa chini ya wiki 6 ..... 28
- B. Watoto wa Wahudumu wa Utunzaji wa Watoto ..... 28
- C. Uwiano wa Wahudumu na Watoto ..... 28

D. Usimamizi 29
E. Mpango wa kukabiliana na majanga 30
F. Ustahiki wa wahudumu 30
**8. MAFUNDISHO 33**
A. Wajibu wa Taasisi ya Utunzaji wa Watoto 33
B. Mafundisho ya uzoefu 33
C. Mafundisho yanayoendelea 33
D. Kunukuu mafundisho 34
**9. KUWASHAURI WATOTO 35**
A. Mbinu chanya za kuwashauri Watoto 35
B. Utekelezaji thabiti na unaofaa wa kanuni za mpango 35
C. Mbinu bora za ushauri 35
D. Vitendo vibaya 35
**10. HAKI ZA WATOTO NA WAZAZI 37**
A. Haki za Watoto 37
B. Haki za wazazi na walezi wa kisheria wa Watoto wanaopokea utunzaji kutoka kwa Taasisi za Utunzaji wa Watoto 37
**11. KURIPOTI KUHUSU KUNYANYASWA NA KUTELEKEZWA KWA WATOTO 38**
**A.** Masharti ya kuripoti kuhusu Kunyanyaswa na kutelekezwa kwa Watoto 38
**B.** Masharti ya Taasisi ya Utunzaji wa Watoto ya kutoa taarifa 38
**C.** Maagizo yaliyoandikwa ambayo yamewasilishwa 38
**D.** Nambari ya dharura iliyochapishwa 38
**12. AFYA NA MATIBABU 39**
A. Chanjo 39
B. Masharti ya tathmini 39
C. Ushauri wa huduma za afya 40
D. Ufuatiliaji wa afya 40
E. Kuwatuma Watoto Nyumbani wanapougua 41
F. Ugonjwa, majeraha makubwa, matukio na ajali 41
G. Huduma ya kwanza 41
H. Kutoa dawa 41
I. Kunawa mikono 42
J. Kuzuia kuhatarishwa na damu na viowevu vya mwili 42
K. Taratibu za hali ya dharura 42
**13. MAJI SAFI NA MAJI TAKA 43**
**A.** Maji Safi 43
**B.** Vipimo vya maji vinavyoendelea vya kila mwaka kwa Taasisi za Utunzaji wa Watoto zenye visima 43
**C.** Vipimo vya maji vya miaka mitano kwa taasisi zenye visima 43
**D.** Mikataba ya maji ya chupa 43
**E.** Mifumo ya maji isiyo ya muda mfupi, isiyo ya jamii 43
**F.** Maji safi na maji choo 44
**14. MAZINGIRA NA USALAMA 45**
A. Hali ya jumla ya jengo na majengo yaliyo karibu 45

B. Wakati wa kucheza nje na kupumzika unahitajika 46
C. Viwango vya kuridhisha vya madini ya risasi 46
D. Monoksidi ya kaboni 47
E. Kiwangojoto cha jengo 47
F. Mwangaza na upenyezaji hewa 47
G. Nafasi ya chini zaidi inayoweza kutumika 47
H. Sehemu za nje za kuchezea 48
I. Silaha 49
J. Nyenzo, Vinyago, Vifaa na shughuli 49
K. Vifaa 50
L. Vitanda vya watoto na matandiko 50
M. Vyoo 51
N. Kutumia nepi/Kwenda choo 52
O. Wanyama vipenzi 52
P. Mazoezi ya kutoroka moto 53
Q. Mpango wa kujiandaa jambo la dharura 53

**15. KUOGELEA NA KUTEMBEA MAJINI 54**

A. Sera kuhusu shughuli za ndani ya maji na taratibu za usalama 54
B. Ruhusa ya mzazi 54
C. Sehemu 54
D. Kiwango cha chini cha mafundisho na leseni inayohitajika kwa shughuli za maji 54
E. Usafi 55
F. Ufikiaji wa bwawa 55
G. Taratibu na mazoezi ya kjiandalia hali za dharura 55
H. Uwiano wa Wahudumu na Watoto wakati wa shughuli za maji 55
I. Mabwawa ya kuogelea 55
J. Mabwawa ya nje ya kituo au hifadhi asili za maji 56
K. Watoto wasiojua kuogelea 56

**16. VIFAA VYA VYAKULA NA VYA JIKONI 57**

A. Vyakula na vitafunio vyenye virutubisho vyote 57
B. Kunawa mikono 57
C. Mizio 57
D. Majukumu ya Wahudumu wa Utunzaji wa Watoto 57
E. Hifadhi ya chakula 58
F. Maandalizi ya chakula 58
G. Vifaa na vyombo 58
H. Vifaa vya jikoni 58

**17. USAFIRISHAJI 60**

A. Masharti ya madereva 60
B. Uwezo wa gari usiopaswa kukiukwa 60
C. Usalama katika magari 60
D. Ziara za nyanjani 60

**18. MIPANGO YA WATOTO 62**

**A.** Sheria za ziada za mpango zinazowahudumia watoto 62

**B.** Vizuizi vya ghorofa ya kwanza 62
**C.** Kukuza mahitaji ya kimaendeleo 62
**D.** Kula 62
**E.** Kulala/kupumzika 63
**19. UTUNZAJI WA WATOTO WA USIKU 64**
A. Sheria za ziada za utunzaji wa usiku 64
B. Utunzaji wa kibinafsi 64
C. Vyumba vinavyotumika kulala au kupumzika 64
D. Vitanda na matandiko 64
**20. MIPANGO YA BAADA YA SHULE NA UTUNZAJI WA MARA KWA MARA 65**
A. Sheria za ziada za vituo vya utunzaji wa watoto wa umri wa kwenda shule 65
B. Mipango ya utunzaji wa mara kwa mara 65
**21. UTEKELEZAJI, UTUMAJI MAOMBI TENA NA RUFAA 66**
A. Utekelezaji 66
B. Adhabu za Kiraia 66
C. Leseni yenye masharti 66
D. Kusitishwa kwa leseni 66
E. Rufaa na Mamlaka ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali 67
F. Kukataa kutoa au kusasisha leseni 67
G. Kubatilishwa kwa leseni 67
H. Kughairiwa kwa leseni yenye masharti 67
I. Makubaliano ya idhini 67
J. Kizuizi cha utumaji maombi tena baada ya kunyimwa au kughairiwa kwa leseni 67
K. Ombi la baadaye la leseni kamili 68
L. Kutolewa kwa leseni kamili baada ya mapungufu kusahihishwa 68
M. Haki ya kukata rufaa 68
**MAMLAKA YA KISHERIA NA HISTORIA YA UDHIBITI 69**

**10-148 CMR**
**Sura ya 32**

**Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu**
**Ofisi ya Huduma za Watoto na Familia**

# KITUO CHA UTUNZAJI WA WATOTO KANUNI YA LESENI

## VITUO VYA HUDUMA YA WATOTO, SHULE ZA WATOTO, TAASISI ZA UTUNZAJI WA WATOTO, MIPANGO MINGINEYO

---

## KAULI YA MUHTASARI

Sheria hii imewekwa ili kudhibiti utoaji wa leseni kwa Vituo vya Utunzaji wa Watoto katika Jimbo la Maine, ikijumuisha Vituo vya Utunzaji wa Watoto, Shule za Chekechea, Vituo Vidogo vya Utunzaji wa Watoto na Mipango Mingine, na kulinda afya, usalama na ustawi wa Watoto wanaohudumiwa.

---

## MAMLAKA

Sheria hii imetangazwa chini ya mamlaka ya 22 M.R.S. Sura za 1661, 1663, 1673 na 1675.

## TAREHE YA KUTUMIKA

Tarehe 27 Septemba, 2021

## SEHEMU YA 1. KAULI YA AZIMIO NA FASILI

**A.** **Kauli ya Azimio**. Madhumuni ya sheria hii ni kuweka viwango vya kutoa leseni kwa Vituo vya Utunzaji wa Watoto. Kwa madhumuni ya kanuni hii, "Taasisi za Utunzaji wa Watoto" zinafafanuliwa kwa upana, kulingana na 22 M.R.S. §8301-A(1-A)(B), itajumuisha Vituo vya utunzaji wa watoto (22 M.R.S. §8301-A(1-A)(A)), shule za chekechea (22 M.R.S. §8301-A(1-A)(D)), taasisi ndogo za utunzaji wa watoto (22 M.R.S. §8301(1-A)(E)), na mipango mingine (22 M.R.S. §8301-A(1-A)(B)); ambapo Huduma za Utunzaji wa Watoto zimerejelewa, kanuni hii inasimamia utendakazi wa kila aina ya taasisi hizo. Ambapo kifungu cha kanuni hii kinatumika kwa mojawapo tu ya aina hizo za taasisi, kanuni hiyo itasema hivyo.

Kanuni hii inaanza kutekelezwa kwa mujibu wa 22 M.R.S. Sura ya 1661, 1663, 1673 na 1675 na inaeleza masharti ya chini zaidi ya utoaji leseni na uendeshaji wa Vituo vya Utunzaji wa Watoto. Kanuni hiyo inaunga mkono huduma za Utunzaji wa Watoto zinazokidhi mahitaji ya kisaikolojia na ya ukuaji wa Watoto, huku zikitoa mazingira salama, ulinzi na afya.

**B.** **Fasili.** Kama inavyotumika katika kanuni hii, isipokuwa muktadha ukionyesha vinginevyo, maneno yafuatayo yana maana zifuatazo:

**1.** **Dhuluma au Kutelekezwa** ni tishio la afya au ustawi wa Mtoto kutokana na majeraha au uharibifu wa kimwili, kiakili au kihisia, unyanyasaji au dhuluma ya kingono, kunyimwa mahitaji muhimu au kukosa kulindwa dhidi ya mambo haya, ambayo yanafanywa na mtu anayewajibikia Mtoto.

**2.** **Ajali** ni tukio ambalo husababisha uharibifu au majeraha yanayoonekana (mkwaruzo, alama ya kuumwa, goti lililochubuka, kutolewa kwa huduma ya kwanza, n.k.).

**3.** **Mtu mzima** ni mtu wa umri wa miaka 18 na zaidi.

**4.** **Yanayolingana na umri** ni shughuli, nyenzo, mtaala na mazingira ambayo yanawiana kimaendeleo na umri wa mpangilio wa Mtoto/watoto wanaohudumiwa.

**5.** **Mwombaji** ni mtu yeyote anayeomba Leseni chini ya Kanuni hizi.

**6.** **Rekodi ya Mahudhurio** ni orodha ya majina ya Watoto waliopo wenyewe kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto wakati wowote.

**7.** **Vichafuzi vya kibayolojia** ni viumbe hai (kama vile bakteria, vimeng'enyaji, kuvu, virusi) au bidhaa zake ambazo zinaweza kuwa hatari kwa afya ya wanyama au binadamu ikiwa atazipumua, kumeza au kufyonza kwa njia nyinginezo mwilini.

**8.** **Mlinzi wa Uokoaji Aliyeidhinishwa** ni mtu aliye na cheti cha sasa cha mbinu za kuokoa maisha kinachotolewa na mwalimu aliyehitimu kutoka shirika linalotambulika baada ya kuhitimu kwa mafundisho ya moja kwa moja.

**9.** **Mtoto au Watoto** ni mtu au watu walio chini ya umri wa miaka 13.

**10.** **Taasisi ya Utunzaji wa Watoto** kwa mujibu wa 22 M.R.S. §8301-A(1-A)(B), ni kituo cha utunzaji wa Watoto, shule ya chekechea au kituo kidogo cha Utunzaji wa watoto, kama ilivyofafanuliwa katika §§8301-A(1-A)(A), (F), na (E), mtawalia, pamoja na mpango wowote wa Watoto walio na umri wa chini ya miaka 5 ulio katika shule ya kibinafsi na mipango yenye mkataba na kituo kimoja au vingi vya Mifumo ya Huduma za Maendeleo ya Watoto (22 M.R.S. §8301-A(1-A)(B)).

**a.** Taasisi ya Utunzaji wa Watoto inajumuisha:

i. **Kituo cha Utunzaji wa Watoto** (22 M.R.S. §8301-A(1-A)(A)) inamaanisha (1) Nyumba au mahali pengine ambapo mtu hufanyia au kutekeleza kwa njia nyingine mpango wa kawaida, kwa uzingatiaji, kwa sehemu yoyote ya siku kutoa utunzaji na ulinzi kwa Watoto 13 au zaidi wenye umri wa chini ya miaka 13; au (2) Eneo au maeneo yoyote yanayoendeshwa kama mpango mmoja wa Utunzaji wa Watoto au na mtu au watu wakati kuna zaidi ya Watoto 12 wanaotunzwa;

ii. **Shule ya Chekechea** (22 M.R.S §8301-A (D)). Nyumba au mahali pengine ambapo mtu hutoa huduma kwa Watoto 3 au zaidi wa umri wa kati ya miezi 33 na miaka 8, kwa kikao kisichozidi saa tatu na nusu kwa kipindi kimoja;

iii. **Kituo Kidogo cha Utunzaji wa Watoto** (22 M.R.S. §8301-A(1-A)(E)). Nyumba au mahali pengine, ambapo sio makazi ya mwendeshaji, ambamo mtu hufanyia au vinginevyo kuendesha mara kwa mara mpango uliopangwa, kwa sehemu yoyote ya siku, kutoa utunzaji na ulinzi kwa Watoto 3 hadi 12 wa umri wa kati ya wiki 6 na miaka 12;

iv. **Mipango Mingine** (22 M.R.S. §8301-A(A-1)(B)). Mpango wowote wa Watoto wa umri wa chini ya miaka 5 ambao unapatikana katika shule ya kibinafsi na mipango ambayo imeweka kandarasi na kituo kimoja au vingi vya Mfumo wa Huduma za Ustawi wa Watoto zinahitajika kupewa leseni kama Kituo cha Utunzaji wa Watoto (yaani, mipango shirikishi ya Maandalizi ya Umma inayojumuisha Mpango wa Kuanza Mapema (Head Start), Huduma za Maendeleo ya Mtoto, au matunzo ya watoto yanayofadhiliwa na watu binafsi).

**b.** Taasisi ya Utunzaji wa Watoto haijumuishi:

i. Mtoa Huduma za Utunzaji wa Watoto wa Familia (22 M.R.S. §8301-A(1-A)(C));

ii. Kambi ya majira ya kiangazi ya makazi au ya usiku kucha iliyoanzishwa kwa madhumuni ya burudani na elimu pekee, iliyoidhinishwa kwa mujibu wa 10-144 CMR Sura ya 208, Kanuni Zinazohusiana na Kambi za Vijana, Kambi za Kimsingi na za Safari;

iii. Mpango unaotoa maagizo mwafaka kwa Watoto kwa madhumuni ya kufundisha stadi moja kama vile karate, densi au mpira wa vikapu;

iv. Shule ya kibinafsi inayotambuliwa na Idara ya Elimu kama mtoaji wa mafundisho ya usawa kwa madhumuni ya mahudhurio ya usawa ya shule; au

v. Shule rasmi ya umma au ya kibinafsi ya asili ya shule ya chekechea, msingi au sekondari iliyoidhinishwa na Kamishna wa Elimu kwa mujibu wa Kifungu cha 20-A.

**11. Mhudumu wa Utunzaji wa Watoto** ni mtu binafsi:

**a.** (1) Ambaye ameajiriwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto na ambaye analipwa fidia, ikijumuisha mmiliki, Mhudumu wa kandarasi au mtu aliyejiajiri; au (2) Ambaye shughuli zake zinahusisha uendeshaji au usimamizi wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto au ufikiaji usiosimamiwa wa Watoto wanaotunzwa au kusimamiwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**b.** Mhudumu wa Watoto hajumuishi mtu ambaye ana uhusiano na Watoto wote ambao wanapokea huduma za utunzaji, au mkandarasi anayefanya matengenezo na ukarabati katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto ambaye hana ufikiaji usiosimamiwa wa Watoto wanaotunzwa au kusimamiwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**12.** **Mtoto mwenye mahitaji maalum** ni Mtoto ambaye:

**a.** Ana umri wa hadi miaka 13 ambaye amethibitishwa na kusajiliwa na mtaalamu aliyehitimu kuwa "Mtoto anayeishi na ulemavu" kama inavyofafanuliwa katika kifungu cha 602 cha Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (20 U.S.C. §1401);

**b.** Anastahiki huduma za usaidizi wa mapema chini ya Sehemu ya C ya Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (20 U.S.C. §§1431, et seq.); anastahiki kupokea huduma chini ya kifungu cha 504 cha Sheria ya Urekebishaji ya 1973 (29 U.S.C. §701);

**c.** Anakidhi masharti ya ufafanuzi wa ulemavu chini ya Sheria ya Wamarekani Wenye Ulemavu ya 1990 (ADA) (42 U.S.C. §12102); au

**d.** Anachukuliwa kuwa katika hatari ya matatizo ya afya na/au ya kiustawi kutokana na sababu za hatari za kibayolojia, na/au kutokana na sababu za hatari za kimazingira zilizotambuliwa ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu, ukosefu wa makazi, unyanyasaji na/au kutelekezwa, sumu ya madini ya risasi, na kuhatarishwa na dawa za kulevya au pombe kabla ya kuzaliwa.

**13.** **Kusafisha** ni kuondoa uchafu, vifusi na viowevu vya mwili kwa kusugua na kuosha kwa mchanganyiko wa sabuni na kusuuza kwa maji.

**14.** **Makubaliano ya Kibali** ni masharti yaliyoandikwa ambayo Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitafuata kama masharti ya kupewa leseni.

**15.** **Siku** inamaanisha siku za kalenda, isipokuwa ikifafanuliwa vinginevyo.

**16.** **Idara** ni Kitengo cha Utoaji Leseni ya Utunzaji wa Watoto ndani ya Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu chenye jukumu la kufanya ukaguzi na kutoa leseni, isipokuwa kama ikibainishwa vinginevyo ndani ya sheria hii.

**17.** **Mwafaka kimaendeleo** ni vitendo, mazingira, vifaa, nyenzo, mawasiliano, maingiliano au shughuli ambazo zinatokana na mahitaji binafsi ya kimwili, kihisia, kijamii na kiakili kwa kila Mtoto anayehudumiwa.

**18.** **Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa**ni mpango ulioandikwa ambao umetayarishwa na Idara kufuatia ukaguzi au uchunguzi ambapo ukiukaji wa sheria hii umetambuliwa. Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa unajumuisha taratibu, mbinu, mabadiliko mahususi yatakayotungwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto ili kurekebisha maeneo yote ya ukiukaji. Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa pia unajumuisha muda ambao Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitarejea kutii sheria husika.

**19.** **Mkurugenzi** ni mtu aliyehitimu ambaye ana jukumu la kutekeleza sera na kusimamia mpango.

**20.** **Nidhamu** ni kufundisha Watoto kuhusu matarajio, miongozo na kanuni, kudumisha usalama, kukuza uwezo wa kufanya uamuzi bora na kukuza na kudumisha nidhamu binafsi.

**21.** **Hitimisho** ni uamuzi uliofanywa na Mpelelezi wa Nje ya Nyumbani kwa kuzingatia ukweli na ushahidi uliokusanywa wakati wa uchunguzi ili kuegemeza uamuzi wa mtu anayewajibikia Mtoto, kwa kuzingatia ushahidi, kuhusu Mtoto aliyenyanyaswa au kutelekezwa.

**22.** **Baraza Linaloongoza** ni mtu au watu ambao hatimaye wanawajibikia uendeshaji wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kilichojumuishwa.

**23.** **Kikundi** kinamaanisha Watoto mahususi walikabidhiwa Wahudumu mahususi wa Utunzaji wa Watoto ndani ya chumba kimoja au nafasi ya shughuli inayoweza kutambulika.

**24.** **Nyenzo Hatari** ni bidhaa au kitu chochote (ya kibayolojia, kikemikali, kirediolojia na/au kihalisi), ambayo ina uwezo wa kusababisha madhara kwa binadamu, wanyama au mazingira, yenyewe au kwa kuchanganywa na nyenzo nyinginezo.

**25.** **Mshauri wa Afya** ni daktari, msaidizi wa daktari, mhudumu wa muuguzi au muuguzi aliyesajiliwa mwenye uzoefu wa matibabu ya watoto au huduma kwa Watoto, aliyepewa leseni ya kufanya kazi nchini Marekani.

**26.** **Tishio la Papo Hapo** ni hali ambayo Kituo cha Utunzaji wa Watoto kimesababisha kwa kutotii sehemu moja au nyingi za sheria hii, au kuna uwezekano wa kusababisha, madhara au matatizo kwa Mtoto, na kunaendelea kuwa na hatari ya papo hapo ya madhara au matatizo isipokuwa hatua za haraka za kurekebisha zichukuliwe.

**27.** **Hatari ya Papo Hapo** ni hali ambayo Kituo cha Utunzaji wa Watoto kimesababisha kwa kutotii sehemu moja au nyingi za kanuni hii, au kuna uwezekano wa kusababisha, majeraha mabaya au kifo cha Mtoto, na kunaendelea kuwa na hatari ya papo hapo ya majeraha mabaya au kifo cha Mtoto isipokuwa hatua za haraka za kurekebisha zichukuliwe.

**28.** **Tukio** ni jambo kuu linalotokea, ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu mlipuko mkali, madai ya tabia isiyofaa ya Mhudumu wa Watoto, tabia isiyofaa ya ngono ya Mtoto, tukio lisilo la kawaida, mabadiliko ya tabia yanayoshuhudiwa au utambuzi wa unyanyasaji au kutelekezwa unaofanywa na Mtoto au mzazi.

**29.** **Mtoto mchanga** ni Mtoto wa umri wa wiki sita hadi miezi 12.

**30.** **Mpango wa Watoto wachanga/Watoto** ni Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinachohudumia Watoto wa umri wa wiki 6 hadi miezi 36.

**31.** **Uchunguzi** ni msururu wa utaratibu wa mahojiano, ukaguzi wa rekodi na uchunguzi unaofanywa kwa madhumuni ya kubaini uwepo wa unyanyasaji na/au kutelekezwa kwa Mtoto na/au ukiukaji wa sheria hii.

**32.** **Mwalimu Mkuu** ni mtu binafsi anayewajibikia mpango kwa kikundi cha Watoto wanaohudhuria Kituo cha Utunzaji wa Watoto. Mwalimu mkuu anaweza pia kufanya kazi chini ya Mkurugenzi au kuwa Mkurugenzi mwenyewe.

**33.** **Mlezi wa Kisheria** ni mtu au wakala aliyeidhinishwa kisheria kuchukua hatua kwa niaba ya Mtoto.

**34.** **Leseni** ni ruhusa, iwe ya muda mfupi, ya kimasharti au kamili, iliyoandikwa na Idara ambayo inaidhinisha utendakazi wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**35.** **Uwezo Ulioidhinishwa kwa Leseni** ni idadi na umri wa Watoto, waliobainishwa kwenye leseni, wanaoruhusiwa kuwa kwenye kituo wakati wowote.

**36.** **Kufuli** ni kifaa cha kufunga kinachofunguliwa kwa ufunguo, mseto au mfumo mwingine ambao umeambatanishwa kwenye chuma au kisanduku kilichofungwa kabisa au sefu ambayo inazuia ufikiaji wa dawa, vifaa vya kusafisha na sumu nyinginezo, rekodi za siri na kumbukumbu.

37. **Kufungwa** ni hali ya kufungiwa, na ikiwezekana kujificha, ndani ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto wakati si salama kuondoka kwenye kituo hicho au kuwa nje wakati wa hali ya dharura.

38. **Mpiga Ripoti Mwenye Mamlaka** ni mtu ambaye anatakiwa kisheria kuripoti tuhuma za kuaminika za unyanyasaji au utelekezaji wa Watoto.

39. **Upeo wa Ukubwa wa Kikundi** ni jumla ya idadi ya Watoto ambao wanaweza kukabidhiwa kwa Mhudumu mahusus wa Utunzaji wa Watoto, wanaokaa kwenye darasa binafsi, nafasi iliyobainishwa vyema ndani ya chumba kikubwa zaidi, au eneo la uwanja wa michezo. Upeo wa ukubwa wa kikundi hubainishwa na aina ya mpango na uwiano unaoruhusiwa kama inavyofafanuliwa katika sheria hii.

40. **Dawa** ni dawa ambazo mhudumu wa afya aliyeidhinishwa ameagiza, na pia dawa ambazo hazijaagizwa.

41. **Uendeshaji wa Vituo Vingi** unamaanisha shirika la Utunzaji wa Watoto lenye leseni tofauti zinazoshiriki baraza moja tawala, linaweza kuwa na kazi jumuishi za biashara, uwekaji kumbukumbu na uongozi.

42. **Hifadhi Asilia ya Maji** ni bahari, ziwa, bwawa, mto, hifadhi, machimbo, chemchemi, kijito na eneo la mabonde ambalo linaweza kutumika kwa shughuli za burudani za maji.

43. **Utunzaji Wakati wa Usiku** unamaanisha Utunzaji wa Watoto unaolipiwa ambao unatolewa kati ya saa sita usiku na saa kumi na mbili asubuhi (12 a.m. na 6 a.m.)

44. **Asiyeogelea** ni Mhudumu wa Watoto au Mtoto ambaye hawezi kuogelea futi 25 kwa tumbo, futi 25 kwa mgongo na kukanyaga maji kwa dakika 1.

45. **Mpango wa Utunzaji wa Mara kwa Mara** ni Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinachowahudumia watoto kwa kufanya ziara au kwa njia nyingine isiyo ya mara kwa mara wakati wazazi hawapo ndani ya jengo; kwa mfano, Huduma ya watoto iko katika eneo la kuteleza majini au kituo cha ununuzi.

46. **Kitengo cha Uchunguzi wa Nje ya Nyumbani (OOH)** ni kitengo ambacho kinawajibikia kuchunguza ripoti za tuhuma za unyanyasaji na utelekezaji Watoto unaofanywa na watu au katika vituo vilivyopewa leseni kwa mujibu wa 22 M.R.S §§8351-8358.

47. **Mzazi** ni baba, mama, au mtu asiye wa jinsia mbili ambaye ni mzazi asili au wa kambo. Kwa madhumuni ya kanuni hii, Mzazi anajumuisha Mlezi wa Kisheria.

48. **Mpango wa Utekelezaji** ni mpango ulioandikwa ambao umetayarishwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa kushirikiana na Idara wakati wa ukaguzi au mpango ulioandikwa ambao umetayarishwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto na kuwasilishwa kwa Idara. Mpango wa Utekelezaji unajumuisha taratibu, mbinu, mabadiliko mahusus yatakayotungwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto ili kurekebisha maeneo yote ya ukiukaji. Mpango wa Utekelezaji pia unajumuisha muda ambao Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitarejea kutii sheria husika.

49. **Majengo** ni sehemu zote za mali isiyohamishika ambayo imeunganishwa, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, ardhi, njia za kibinafsi, na majengo au miundo yoyote, ambayo Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinamiliki, au kina udhibiti au ubia wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja, ingawa huenda Watoto hawahudumiwi katika sehemu zote za mali hii isiyohamishika.

50. **Mtoto wa Shule ya Chekechea** ni Mtoto wa miaka 3 hadi 5.

51. **Barua ya Kustahiki kwa Mtoa Huduma** ni barua inayotumwa na Idara kwa mtu ambaye anafanyiwa ukaguzi wa kina, ambayo inaripoti hali ya ustahiki kwa kipekee na haifichui maelezo mahusus ya kutostahiki au taarifa yoyote ya siri kuhusu mtu huyo.

**52.** **Ukiukaji unaorudiwa** ni ukiukaji wa kanuni mahususi ya utoaji leseni ambayo imetajwa awali kwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**53.** **Dawa ya Uokoaji** ni dawa iliyoagizwa na kufungwa kwa ajili ya matumizi ya Mtoto mahususi katika hali ya dharura, kama vile Epi-pen au dawa ya kufungua njia za kupumua.

**54.** **Kupumzika na Kustarehe** ni wakati wa kufurahia tulivu bila kupewa maelekezo. Hii inaweza kujumuisha vipindi vya kusoma, kulala usingizi mwepesi wa mchana, au shughuli zingine tulivu za kibinafsi zinazolingana na umri wa Watoto.

**55.** **Hatari** inamaanisha uwezekano kwamba Mtoto anaweza kupata aina fulani ya madhara, majeraha au unyanyasaji na/au kutelekezwa kulingana na mambo na/au hali ambazo Mtoto huyo amekabiliwa nazo.

**56.** **Mtoto wa Umri wa Kwenda Shule** ni Mtoto ambaye ana umri wa angalau miaka 5 na chini ya miaka 13.

**57.** **Mpango kwa Watoto wa Umri wa Kwenda Shule** ni mpango unaotoa utunzaji wa Watoto walio na umri wa kwenda shule pekee. Mpango kwa watoto wa umri wa kwenda shule huendeshwa kabla au baada ya siku ya kawaida ya shule na pia unaweza kuendeshwa wakati wa likizo za shule, kipindi cha kiangazi, au wakati wowote ambapo shule zimefungwa, ikijumuisha siku za kwanza za kutolewa.

**58.** **Jeraha Kubwa** linamaanisha:

**a.** Jeraha au ugonjwa ambao unahitaji matibabu kutoka kwa daktari au wahudumu wengine wa matibabu, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, kupelekwa kwenye chumba cha dharura na/au kulazwa hospitalini, ikijumuisha majeraha ambayo yanatokana na ajali inayohusisha usafiri wa kwenda au kutoka hafla inayofadhiliwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto; au

**b.** Ugonjwa wowote ambao ni hali inayopaswa kuripotiwa, kama inavyotambuliwa na Idara kwenye https://www.maine.gov/dhhs/mecdc/infectious-disease/epi/disease-reporting/documents/notifiable-list.pdf.

**59.** **Kukaa kwenye Makazi** ni kubaki ndani ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto wakati wa hali ya dharura, wakati hali zinaonyesha kuwa si salama kuondoka kwenye kituo hicho.

**60.** **Bwawa la Kuogelea** ni chombo chochote kilichojaa maji, kilicho ndani ya nyumba au nje, kwa kuogelea au cha shughuli za burudani, na kilicho na kina cha zaidi ya inchi ishirini na nne (24”) wakati wote.

**61.** **Mtoto mdogo** ni Mtoto wa umri wa miezi 13 hadi 36.

**62.** **Kitu chenye Sumu** ni kemikali au mchanganyiko wowote ambao unaweza kudhuru mazingira na afya ya binadamu ikiwa mtu ataupumua, kuumeza au kuufyonza kupitia ngozi.

**63.** **Tahadhari za Usalama kwa Wote** ni mbinu ya kudhibiti maambukizi ambapo damu yote ya binadamu na viowevu fulani vya mwili wa binadamu vinachukuliwa kana kwamba vinajulikana kuwa na HIV, HBV na viini vya magonjwa vinavyoenezwa kwa damu.

**64.** **Ondoleo** ni ruhusa iliyoandikwa na Idara ili kurekebisha kifungu cha kanuni hii.

**65.** **Shughuli za Maji** ni matumizi ya mabwawa ya kutumbukia, mabwawa ya kutembea majini, mabwawa ya kuogelea yenye vitelezi au yasiyo navyo, na hifadhi nyingine za maji sawa na hivyo, ikiwa ni pamoja na madimbwi, mito na bahari, bila kujumuisha meza za maji na vinyunyizio.

**66.** **Mhudumu wa Usalama Majini** ni mtu aliyepewa jukumu la kuwaangalia Watoto wanaoshiriki katika shughuli za maji ambaye amemaliza kozi ya msingi ya usalama wa maji iliyoidhinishwa na Idara ambayo inajumuisha mafundisho ya mbinu za uokoaji zisizo za kuogelea ndani ya miaka mitatu iliyopita.

**67.** **Bwawa la kutembea ndani** ni bwawa lenye kiwango cha maji kinachodumishwa kwa inchi 24 au chini na kisichozidi kipenyo cha futi 4. Bwawa hili halihitaji chujio na huenda lisiwe na maji yaliyotiwa kemikali.

**68.** **Mhudumu wa bwawa la kutembea ndani** ni mtu ambaye ana cheti halali cha Huduma ya Kwanza na CPR kwa watu wazima na watoto na ana jukumu la usimamizi wa Watoto katika bwawa la kuogelea kama ilivyofafanuliwa hapa juu.

## SEHEMU YA 2. MASHARTI NA TARATIBU ZA KUPEWA LESENI

### A. Kupewa Leseni

**1.** Hakuna mtu au shirika linaloweza kuendesha Kituo cha Utunzaji wa Watoto chenye zaidi ya Watoto wawili bila leseni kutoka kwa Idara inayotumika, inayoidhinisha uendeshaji huo, kwa mujibu wa 22 M.R.S. §7801(1)(E).

**2.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kichapishe maudhui yafuatayo, mahali ambapo yanaonekana kwa urahisi, kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto:

**a.** Leseni ya sasa iliyotolewa na Idara;

**b.** Matokeo ya ukaguzi wa hivi majuzi, kuonyesha ukiukaji wowote wa kanuni hii;

**c.** Hatua zozote za utekelezaji, ikijumuisha Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa au leseni yenye masharti; na

**d.** Notisi au barua zozote zinazohitajika na Idara zinapaswa kutumwa, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu matokeo ya vipimo vya maji au tathmini yoyote ya hatari.

**e.** Idara itachapisha ripoti za ukaguzi kwa tovuti inayopatikana kwa umma kwa ujumla, kwa muda wa miaka mitatu, kwa mujibu wa 42 CFR §98.33(4).

**3.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitawajibikia kuhakikisha watu wanatii sheria na kanuni zote za Jimbo na shirikisho na kanuni hii.

**a.** Wahudumu na wakufunzi wote wanaofanya kazi katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto wanawajibika kutii kanuni hii.

**4.** Leseni zinatumika tu katika eneo ambalo zimetolewa. Iwapo Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitahamia eneo lingine, ni lazima leseni mpya itolewe kabla kianze kufanya shughuli.

**a.** Leseni haiwezi kuhamishwa kutoka Kituo kimoja cha Utunzaji wa Watoto hadi kingine.

**b.** Ikiwa kuna tukio lisilotarajiwa, kama vile moto, linalofanya kituo kilichoidhinishwa kisiweze kuwa makazi ya watu, Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaweza kutoa huduma mahali pengine baada ya kuidhinishwa na Idara, kwa mujibu wa kanuni za Mpango wa Dharura wa Utunzaji wa Watoto wa Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu.

**c.** Eneo mbadala lazima pia liidhinishwe na Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto wa Jimbo au idara ya zimamoto ya eneo ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto kabla ya utoaji wa huduma za Utunzaji wa Watoto.

**5.** Majengo mawili (2) au zaidi yanapotumika au ikiwa yatatumika kuendesha Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinachoendeshwa na mtu mmoja, mtu huyo anapaswa kutuma maombi kwa Idara ili kupata leseni moja inayojumuisha majengo yote, mradi tu:

**a.** Majengo yapo kwenye ardhi moja au iliyojumuishwa, na Idara itabaini kwamba utoaji wa leseni moja ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto hautakuwa na madhara kwa afya, usalama, ustawi na maendeleo ya Watoto wanaohudumiwa;

**b.** Vituo hivi lazima viwe na Mkurugenzi mmoja.

**6.** Hakuna Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitakachowahudumia idadi ya Watoto inayozidi inayoruhusiwa katika leseni. Huduma za Utunzaji wa Watoto lazima ziwahudumie tu Watoto wa umri uliotajwa kwenye leseni iliyotolewa, na kwa uwiano sahihi wa wahudumu na Watoto kwa umri huo.

**a.** Huenda mabadiliko ya uwezo au umri yaruhusiwe kufanywa kwa hekima ya Idara, na inapobidi, kwa idhini ya watekelezaji wa kanuni wa eneo husika, na Ofisi ya Kikosi cha Zimamoto wa Jiji.

**b.** Leseni inaweza kurekebishwa au kutolewa upya ili kuongeza au kupunguza idadi ya Watoto wanaoruhusiwa au kubadilisha umri wa Watoto ambao wanaweza kuhudumiwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**B.** **Ustahiki wa Mwombaji na Mkurugenzi**. Mwombaji na Mkurugenzi anayependekezwa lazima aonyeshe nia na uwezo wake wa kuendesha na kusimamia Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa busara komavu, kuzingatia kwa ukarimu maslahi ya Watoto na kufuata kanuni hizi na sheria zote husika kila mara. Inapofanya uamuzi huu, Idara itazingatia kila mojawapo ya masuala yafuatayo kwa kadri yanavyohusiana na Mwombaji anayependekezwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto:

**1.** Rekodi na sifa za uaminifu na mwenendo halali katika biashara na mambo ya kibinafsi, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu:

**a.** Kukamatwa, kufunguliwa mashtaka au kupatikana na hatia;

**b.** Uchunguzi unaofanywa na Huduma za Ulinzi wa Watoto au Kitengo cha Upelelezi wa Nje ya Nyumbani cha Idara hii;

**c.** Kuondolewa kwa Watoto kwenye utunzaji au huduma ya Mwombaji au Mkurugenzi kwa amri ya mahakama;

**d.** Ulinzi wowote dhidi ya amri ya unyanyasaji au amri nyingine yoyote ambayo inatambua matokeo ya unyanyasaji wa nyumbani au vurugu za familia; na/au

**e.** Uchunguzi wowote wa awali wa leseni, leseni zinazotolewa kwa masharti, kusimamishwa kwa leseni, kukataliwa kwa maombi, faini na/au ubatilishaji kuhusu leseni ya Utunzaji wa Watoto au idhini iliyotolewa kwa Mwombaji au Mkurugenzi.

**2.** Maadili ambayo yanaonyesha uelewa wa, na kutii kanuni hii;

**3.** Taarifa ambayo inahusiana na uwezo au nia ya kutii sheria na kanuni zote zinazotumika;

**4.** Taarifa yoyote inayohusiana na uwezo wa kutoa huduma ya utunzaji wa Watoto ambayo ni salama na inayofaa ustawi wa Watoto;

**5.** Uzoefu husika, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kusimamia shughuli za kifedha na wahudumu wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinachotafutiwa leseni ; uzoefu katika nyanja ya utunzaji wa Watoto, maendeleo wa Watoto au maeneo yanayohusiana na utoaji wa huduma za utunzaji wa Watoto.

**6.** Mwombaji lazima aidhinishe Idara kukagua rekodi za tasisi zifuatazo ili kuamua utiifu wa sheria hii, kama sehemu ya mchakato wa kuomba na kupewa leseni mpya: historia ya uhalifu na rekodi ya udereva, inapohitajika; kumbukumbu za mahakama; sajili za wahalifu wa kingono wa Maine na kitaifa; Huduma za Ulinzi wa Watoto, na Uchunguzi wa Nje ya Nyumbani.

**C. Maombi**

**1.** Maombi ya leseni ya kwanza sharti yafanywe kwa Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu, kwenye fomu zilizotolewa na Idara, na ada inayofaa sharti ijumuishwe.

**a.** Hundi lazima itumwe kwa Mweka Hazina, Jimbo la Maine, na haiwezi kurejeshwa.

**b.** Maombi yasiyokamilika ambayo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na mwombaji yatakuwa batili baada ya siku sitini (60).

**c.** Leseni lazima itolewe kabla ya kuanza kwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto, la sivyo Mwombaji anaweza kuwekewa vikwazo.

**2.** Angalau siku sitini (60) kabla ya kuisha kwa muda wa leseni ya kuendesha Kituo cha Utunzaji wa Watoto, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwasilishe maombi na ada inayohitajika ya kusajiliwa upya kwenye Idara kwa kujaza fomu iliyotolewa na Idara, ikiambatana na maelezo yoyote nyongeza kama inavyoweza kuhitajika. Ni wajibu wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kutuma maombi ya kupewa leseni mpya bila kuchelewa.

**3.** Baada ya kupokea na kukagua maombi na uamuzi wa kutii Sheria ya Maine Iliyofanyiwa Marekebisho Ambayo Imefafanuliwa, pamoja na sheria zozote zilizopitishwa kufuatia sheria hii, Idara itatoa leseni mpya kwa muda wa miaka miwili (2), isipokuwa ikibaini kuwa kuna sababu mahususi na za kutosha ama za kukataa ombi la kutoa leseni upya au kusajili upya leseni kwa muda mfupi au kwa masharti fulani.

**4.** Ikiwa maombi ya kutoa leseni upya yatafanywa, leseni iliyopo itaendelea hadi uamuzi wa mwisho kuhusu utoaji leseni upya kufanywa, kwa mujibu wa 5 M.R.S §10002.

**5.** Mwombaji lazima amalize mafundisho yaliyoidhinishwa na Idara kwa mujibu wa Sehemu ya 8 ya sheria hii kabla ya leseni kutolewa.

**6.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitii Kanuni ya Usalama wa Maisha ya Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto wa Jimbo, Idara ya Usalama wa Umma.

**a.** Idara sharti ipokee taarifa iliyoandikwa, inayotolewa mara mbili kwa mwaka na Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto ya Serikali, inayoonyesha kuwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kimetii masharti ya *Kanuni ya Usalama wa Maisha ya Chama cha Kitaifa cha Ulinzi dhidi ya Moto.*

**b.** Hakuna leseni ya kuendesha Kituo cha Utunzaji wa Watoto katika eneo lolote itatolewa hadi Kituo hicho cha Utunzaji wa Watoto kifaulu katika ukaguzi wa kuridhisha kwa usalama na ulinzi dhidi ya moto, ikiwa ni pamoja na vifaa vinavyofanya kazi vya kutambua moto inavyohitajika.

**c.** Kama sharti linaloendelea la utoaji leseni, Idara ya Usalama wa Umma ya Maine, Ofisi ya Kikosi cha Zimamoto cha Jimbo, ni lazima ikague na kuidhinisha majengo ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto angalau kila baada ya miaka miwili (2).

**d.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto sharti kipate idhini kutoka kwa Idara ya Usalama wa Umma ya Maine, Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto ya Jimbo au mwakilishi wake, ambayo inabainisha hasa mahali ambapo utunzaji wa Watoto unaweza kutolewa (vyumba vya chini, vyumba mahususi ndani ya nyumba, na ghorofa ya pili au ya juu zaidi, ikiwa ni pamoja na vizuizi vyovyote vya umri wa watoto).

**e.** Ukaguzi wa ziada wa usalama dhidi ya moto lazima ufanywe wakati mfumo wa joto unabadilishwa, wakati mabadiliko makubwa ya kimuundo yanafanywa kwenye majengo, na kabla ya matumizi ya

vyumba vipya kwenye majengo. Kituo cha Utunzaji wa Watoto kina wajibu wa kuarifu Idara kuhusu mabadiliko yoyote yanayohitaji ukaguzi siku 10 kabla ya ujenzi kufanywa.

**f.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima vianzishe na kudumisha taratibu za kutii masahihisho, vikwazo au masharti yote yaliyobainishwa na Idara ya Usalama wa Umma ya Maine, Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto ya Jimbo au mwakilishi wake katika Mpango wa Marekebisho unaotokana na mapungufu yaliyotambuliwa wakati wa ukaguzi wa usalama dhidi ya moto, ndani ya muda uliowekwa.

**7.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kidumishe hati, na kuziwasilisha kwa Idara ikiomba hati hizi zinazoonyesha kuwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinatii kanuni na sheria za eneo husika, ikiwa ni pamoja na mipaka ya maeneo, au taarifa kutoka utawala wa eneo kwamba hakuna idhini inayohitajika.

**8.** Maombi ya kuongeza idadi ya Watoto ambao Kituo cha Utunzaji wa Watoto kimeidhinishwa kuhudumia, sharti yatumwe kwenda kwenye Idara, pamoja na ada inayotakiwa. Hakuna ongezeko la idadi ya Watoto ambao mpango umeidhinishwa kuhudumia litafanywa bila idhini ya awali iliyoandikwa kutoka kwa Idara, Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto ya Jimbo, na utawala wa utekelezaji wa kanuni za eneo, inapohitajika.

**9.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kipate idhini iliyoandikwa ya mmiliki wa mali au nyumba kwa nafasi yoyote iliyokodishwa au kupangishwa ili kutumika kama kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**D.** **Uchunguzi wa Kina.** Wahudumu wa Watoto walio na umri wa zaidi ya miaka 18 lazima watii masharti yote kwa mujibu wa Kanuni ya 10-148 C.M.R Ch. 34 ya Utoaji Leseni ya Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto.

**1.** Taarifa za kutostahiki zikipatikana katika sajili, hazina na hifadhidata zozote zinazohitajika kwa uchunguzi wa kina wa Mwombaji, au ikiwa Mwombaji haruhusiwi vinginevyo kwa sababu ya kukataa kuridhia kufanyiwa uchunguzi wa kina, au akitoa taarifa za uongo kwa maksudi kuhusiana na ukaguzi wa usuli, hakuna Leseni itakayotolewa kwa Mwombaji huyo.

**2.** Hakuna Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitakachoajiri Mhudumu wa Utunzaji wa Watoto, mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 ambaye hajatoa Barua ya Kustahiki kwa Mtoa Huduma inayoonyesha kuwa Mhudumu wa Utunzaji wa Watoto anastahiki, wala kumruhusu mtu yeyote anayejulikana na Kituo cha Utunzaji wa Watoto kuwa hastahiki chini ya Sheria hii kuweza kumfikia Mtoto yeyote katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**E.** **Aina na kipindi cha leseni**. Aina na kipindi cha leseni ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto iliyotolewa na Idara lazima izingatie masharti ya sheria hii.

**1.** Leseni ya muda itatolewa na Idara kwa mwombaji ambaye anakidhi vigezo vyote vinavyotumika, kwa mujibu wa 22 M.R.S. §7802(A):

**a.** Hajawahi kuendesha Kituo cha Utunzaji wa Watoto katika jimbo la Maine, au amehamia kwenye jengo jipya, au amefunga mpango na anaufungua upya;

**b.** Anatii sheria na kanuni zote zinazotumika za leseni ya muda; na

**c.** Anaonyesha uwezo wa kutii sheria na kanuni zote zinazotumika kwa leseni kamili.

**2.** Leseni ya muda iliyoandikwa inaweza kutolewa kwa muda usiopungua miezi mitatu (3) na usiozidi miezi 12.

**3.** Leseni kamili itatolewa na Idara kwa mwombaji ambaye anatii masharti yaliyowekwa katika sheria hii, kwa mujibu wa 22 M.R.S. §7802 (1) (B).

**4.** Leseni kamili itatolewa kwa kipindi cha miaka miwili (2), kwa mujibu wa 22 MRS §7802 (2)(B)(5).

**5.** Leseni iliyoandikwa yenye masharti inaweza kutolewa Idara ikibaini kuwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kimeshindwa kutii kanuni na sheria zinazotumika. Leseni yenye masharti lazima ibainishe masahihisho ambayo lazima yafanywe, na tarehe ya mwisho ya kufanya kila sahihisho, kwa mujibu wa 22 MRS §7802(1)(C).

**6.** Leseni yenye masharti itatolewa kwa muda maalum usiozidi miezi kumi na mbili (12), au sehemu iliyobaki ya muda wa leseni kamili ya awali, lolote ambalo Idara itaamua ni mwafaka kulingana na ukiukaji ulioainishwa katika Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa, kwa mujibu wa 22 MRS §7802(1)(C).

**7.** Kituo cha Utunzaji wa Waototo kilichoidhinishwa kinapopanga kuhamia eneo jipya, sharti kiwasilishe ombi la kupewa leseni ya eneo hilo jipya. Leseni ya muda inaweza kutolewa na Idara kwa ajili ya eneo hili jipya, kwa kuzingatia 22 MRS §8301-A(6), wakati:

**a.** Masharti yote yanayotumika yaliyowekwa katika sheria hii yametimizwa, isipokuwa ukaguzi au hatua nyingine ya taasisi ya serikali au mwanakandarasi wa taasisi hiyo ambayo inahitajika na sheria hii imecheleweshwa; na

**b.** Hakuna kitendo au ukosefu wa kitendo uliofanywa na mwombaji ulisababisha ucheleweshaji mkubwa na taasisi hiyo ya serikali au mwanakandarasi wa taasisi hiyo.

**8.** Leseni ya muda itatolewa kwa muda maalum, usiozidi miezi sita.

**F. Usimamizi.**

**1.** Shirika, ubia, chama au amana lazima itambue majina na anwani za maafisa wake, washirika, wadhamini au wakurugenzi, na lazima itoe, inapohitajika, hati, makubaliano ya ubia, katiba, vifungu vya ushirika, sheria, hati ya amana, au hati nyingine zinazosimamia wajibu wa kisheria na mamlaka ya huluki.

**2.** Bima.

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na bima ya dhima ya kima cha chini cha $100,000 kwa kila mtu, $300,000 kwa kila tukio; na ya uharibifu wa mali isiyopungua $5,000.

**b.** Leseni ya bima ya dhima sharti iwasilishwe kabla ya leseni kutolewa.

**3.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na nakala ya sheria hii inayoweza kufikiwa kwa urahisi kwenye majengo yake na lazima iweze kufikiwa na mtu yeyote baada ya kuwasilisha ombi.

**4.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto sharti kiwaruhusu wazazi/walezi wa Mtoto wawe na ufikiaji usio na kikomo wa kumtembelea Mtoto, kuangalia mpango wakati wowote ambapo Mtoto yuko kituoni na kutoa fursa za kushiriki katika shughuli.

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kibadilishane taarifa na wazazi/walezi wa Mtoto kuhusu Mtoto kwa marudio ya wakati yanayolingana na umri na ukuaji wa Mtoto husika.

**b.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwashauri wazazi/walezi wa Watoto kabla ya kuwaondoa Watoto kwenye kituo na lazima kipewe idhini iliyoandikwa ya wazazi/walezi wa kisheria.

**c.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiweze kufikiwa moja kwa moja na wazazi/walezi wa Watoto kwa njia ya simu wakati wote ambapo Watoto wapo kituoni.

**d.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwashauri wazazi/walezi wa Mtoto kabla ya kumruhusu Mtoto kushiriki katika shughuli yoyote hatari; kwa mfano, kuogelea, kupanda farasi au kurukia turubali.

**5.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwahimize wazazi/walezi wa kisheria kukitembelea kabla ya mtoto wao kupewa nafasi.

**6.** Nakala ya kitabu cha mwongozo wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto itatolewa kwa wazazi wote au walezi wa kisheria wakati wa kujisajili. Kitabu cha mwongozo lazima kiwe na, angalau:

**a.** Umri wa Watoto wanaohudumiwa;

**b.** Saa za kazi na ratiba ya kila siku;

**c.** Idadi ya Watoto wanaohudumiwa;

**d.** Uzingativu mahususi ikiwezekana, kama vile uzingativu wa elimu, uzingativu wa kidini, Montessori, shughuli za baada ya shule, burudani za msimu wa kiangazi, kituo cha mafundisho, n.k.;

**e.** Fursa za ushiriki wa Mzazi/Mlezi wa Kisheria;

**f.** Maelezo ya mbinu za kuwashauri Watoto zinazotumiwa na Wahudumu wa Watoto;

**g.** Huduma zinazotolewa, kama vile: utunzaji wa kimsingi wa Watoto, utunzaji kwa Watoto wenye mahitaji maalum, utunzaji wa mara kwa mara,
utunzaji kwa watoto wachanga/watoto wadogo, utunzaji kwa watoto wa shule ya chekechea, utunzaji kwa watoto wa umri wa kwenda shule, n.k.;

**h**. Ada (ikiwa ipo) ikijumuisha ada za kuchelewa kuwachukua watoto;

**i.** Sera ya likizo;

**j.** Masharti ya mkataba wowote au makubaliano ya usajili;

**k.** Haki za Watoto;

**l.** Taratibu za dharura na taarifa za kuhamishwa;

**m.** Kuripoti matukio na kuripoti kwa lazima visa vya Unyanyasaji au Kutelekezwa kwa Watoto;

**n.** Kanuni za kufukuzwa na kusimamishwa;

**o.** Udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza;

**p.** Kutoa dawa;

**q.** Kalenda ya kila mwaka ya tarehe za kufunga (ikiwa zipo);

**r.** Rasilimali zinazopatikana kwa uchunguzi wa kimaendeleo; na

s. Kuripoti kifo cha Mtoto na majeraha makubwa.

**7.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe kinatii masharti yanayotumika ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Marekani ya 1990, Pub. L. Nambari. 101-336, 104 Kanuni ya 328 (1990). Kutii viwango vya ufikivu vya ADA ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, yafuatayo:

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakiwezi kuagiza kwamba mzazi(wazazi)/mlezi/walezi wa kisheria wa Watoto walio na ulemavu wa kimwili, kihisia na/au kiakili wapatie Kituo cha Utunzaji wa Watoto taarifa zinazohusu ulemavu wa Mtoto, lakini wanahimizwa kuuliza maswali muhimu ya ukuaji kuhusu Watoto wote kabla ya kuingia, ili kuhakikisha mikakati inayofaa na yenye mafanikio imewekwa.

**b.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihakikishe kwamba wahudumu wote wamepewa mafundisho ya kutosha na/au wana uzoefu wa kutosha ili kukidhi mahitaji ya Watoto wote wanaowajibikia, kama itakavyohitajika.

**8.** Isipokuwa kama ilivyoelezwa kisheria, maelezo ya siri hayawezi kutolewa bila amri ya mahakama au kwa maandishi ya idhini ya mzazi au mlezi wa Mtoto ambaye taarifa zake za siri zimeombwa. Ukiukaji wa masharti haya utasababisha adhabu za kifedha kama ilivyobainishwa hapa na kwa mujibu wa 22 M.R.S. §7702-A. Taarifa za siri zinajumuisha:

**a.** Rekodi zote za Watoto.

**b.** Rekodi zote za wahudumu.

**c.** Maelezo ambayo yanabainisha, moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, mrejelewa, mlalamishi au mwasilishaji ripoti ya tuhuma za unyanyasaji na/au utelekezaji, na/au ukiukaji wa kanuni za leseni, kwa mujibu wa 22 M.R.S §7703(2)(G).

**d.** Taarifa kuhusu Watoto walio katika huduma ya utunzaji (au waliokuwa katika huduma ya utunzaji) lazima ifichuliwe tu baada ya kuidhinishwa kwa ripoti inayoandikwa na mlezi wa Mtoto kisheria, isipokuwa kama imebainishwa vinginevyo na sheria, na lazima ishirikiwe na Idara na wakala ulioidhinishwa wa kuwasajili watoto kwa mujibu wa 22 M.R.S Sura ya 1671, kwa ombi.

**e.** Rekodi za wahudumu lazima zitolewe kwa Idara baada ya ombi kutumwa, kwa mujibu wa 22 M.R.S Sura ya 1661.

**9.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na mwongozo wa Wahudumu wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto ambacho kinashughulikia yafuatayo:

**a.** Sera na utekelezaji wake. Hii lazima ijumuishe, angalau, sera za yafuatayo:

**i.** Kuripoti kama inavyohitajika kisheria,

**ii.** Kuwashauri watoto,

**iii.** Kuugua kwa watoto,

**iv.** Taratibu za kutoroka jengo lenye moto,

**v.** Taratibu za dharura na maafa,

**vi.** Sifa na mafundisho ya wahudumu,

**vii.** Usimamizi wa wahudumu/wakufunzi

**viii.** Kuripoti ukiukaji wa masharti ya leseni,

**ix.** Maadili ya kuwajumuisha Watoto wenye ulemavu,

**x.** Sera ya kulala salama,

**xi.** Kuwasilisha ripoti za majeraha makubwa na vifo vya Watoto,

**xii.** Kuzuia kufukuzwa na kusimamishwa,

**xiii.** Ukalimani kwa Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza,

**xiv.** Kuachiliwa kwa Watoto, na

**xv.** Usafirishaji wa Watoto (ikiwa upo).

**10.** Sharti kituo kipitishe sera iliyoandikwa ya kushughulikia matukio yote yanayoshukiwa ya unyanyasaji au utelekezaji wa Watoto kwa mujibu wa sheria za Maine. Sera iliyoandikwa lazima ijumuishe, lakini si tu, yafuatayo:

**a.** Utaratibu wa kutuma taarifa ya ndani ya tuhuma za unyanyasaji au utelekezaji;

**b.** Hali ambazo zinasababisha kutumwa kwa taarifa ya ndani ya mmiliki, mkurugenzi au mwakilishi;

**c.** Kanuni kwamba matukio yoyote yanayoshukiwa kuwa ya unyanyasaji na/au utelekezaji lazima yatumwe mara moja kwa mmiliki, mkurugenzi au mwakilishi;

**d.** Kanuni kwamba matukio yanayoshukiwa kuwa ya unyanyasaji na/au utelekezaji wa Watoto lazima yatumwe mara moja kwa huduma ya dharura ya Usajili wa Ulinzi wa Watoto;

**e.** Utambulisho wa wahudumu wanaohusika katika kuwasiliana na huduma ya dharura ya Usajili wa Ulinzi wa Watoto;

**f.** Itifaki ya kuwajulisha wahusika wote kwamba washukiwa wa unyanyasaji na utelekezaji wa Watoto umeripotiwa kwa idara ya Usajili wa Ulinzi wa Watoto;

**g.** Kukamilishwa kwa ripoti za matukio, ikijumuisha: maelezo ya madai au tuhuma, tarehe ambayo idara ya Usajili wa Ulinzi wa Watoto ilipokea mawasiliano, wahusika ambao waliarifiwa kuwa ripoti hiyo iliwasilishwa, na kama mzazi/mlezi aliarifiwa au la kuhusu madai hayo; na

**h.** Taarifa kwa mzazi, ikijumuisha uamuzi wa jinsi na maelezo gani yatashirikiwa na mzazi/mlezi wa kisheria wakati idara ya Usajili wa Ulinzi wa Watoto imepokea mawasiliano.

**11.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitengeneze sera iliyoandikwa ya kufuatwa ikiwa madai ya unyanyasaji au utelekezaji wa Watoto yamewasilishwa dhidi ya Mhudumu yeyote wa Huduma kwa Mtoto katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto. Sera hii iliyoandikwa lazima ijumuishe, lakini si tu, yafuatayo:

**a.** Hatua za kinga ili kuzuia tuhuma zinazoweza kutokea;

**b.** Masharti ya kuendelea kuajiriwa na kuwafikia watoto wakati wa uchunguzi unaofanywa na Idara;

**c.** Sababu za kusimamishwa kazi;

**d.** Kuhitajika kuripoti tuhuma za unyanyasaji na utelekezaji wa Mtoto unaotokea mahali popote kwa mujibu wa sheria; na

**e.** Arifa kwa wazazi.

**12.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kina jukumu la kuhakikisha kuwa sera zinafuatwa. Hii inajumuisha:

**a.** Wajibu wa kuanzisha na kudumisha muundo bora wa kifedha;

**b.** Kuhitimu kusimamia Kituo cha Utunzaji wa Watoto au kumwajiri mtu aliyehitimu kusimamia mradi huu; na

**c.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kizingatie kanuni na sheria zote za eneo, jimbo na shirikisho zinazohusiana na uendeshaji wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto katika jimbo la Maine.

**13.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwajibikie uendeshaji wa kila siku kwa kufuata sheria hii.

**a.** Ikiwa mkurugenzi hayupo kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto, Mhudumu wa Watoto aliyehitimu sharti ateuliwe kuwa msimamizi na apewe mamlaka ya kusimamia kituo hicho kwa kufuata sheria hii.

**b.** Kituo kilichoidhinishwa kwa Watoto 13-20 lazima kiajiri angalau mwalimu mmoja kiongozi mkuu ambaye anaweza kuwa mkurugenzi pia. Wasaidizi wanaweza kuajiriwa ili kufikia uwiano unaohitajika.

**c.** Kituo kilichoidhinishwa kuwahudumia zaidi ya Watoto 21 lazima kiajiri mwalimu mmoja mkuu kwa kila kundi la Watoto. Wasaidizi wanaweza kuajiriwa ili kufikia uwiano unaohitajika.

**d.** Ikiwa Mkurugenzi hayupo katika kituo kilichoidhinishwa kuwahudumia Watoto 50 au zaidi, Mhudumu wa Watoto ambaye anakidhi sifa za Mkurugenzi/Mwalimu mkuu lazima ateuliwe kuwa msimamizi na apewe mamlaka ya kusimamia kituo hicho kwa kufuata kanuni hii.

**14.** Ratiba ya sampuli ya shughuli za kila siku lazima ipachikwe katika kila darasa. Ratiba hii lazima ijumuishe yafuatayo, kulingana na saa za kazi:

**a.** Nyakati za milo/vitafunio;

**b.** Wakati wa kulala, kupumzika au kutafakari; na

**c.** Kipindi cha shughuli za ndani na nje zinazolingana na mahitaji ya maendeleo ya Watoto.

**d.** Inapohitajika, lazima ratiba irekebishwe ili kukidhi mahitaji ya kibinafsi ya Watoto.

**15.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kijiandikishe katika Mfumo wa Ukadiriaji na Uboreshaji wa Ubora wa Maine.

16. **Masharti ya Kuzuia Magonjwa ya Kuambukiza.** Kwa Shule za Chekechea pekee, baada ya kila miaka 2, kila mwenye leseni, msimamizi na wahudumu wengine wa Shule ya Chekechea wanaotoa huduma kwa Watoto sharti wathibitishwe kutokuwa na magonjwa ya kuambukiza na daktari aliyeidhinishwa, muuguzi au msaidizi wa daktari, kwa mujibu wa 22 M.R.S. §8402. Hili ni jambo la lazima ili kudumisha leseni kwa Shule za Chekechea, na Shule hizi za Chekechea lazima zidumishe rekodi zinazothibitisha utiifu wa kanuni hii.

**G. Mabadiliko ya leseni.** Ombi la kurekebisha leseni linahitajika wakati:

1. Kituo cha Utunzaji wa Watoto kingependa kuboresha uwezo, ndani ya masharti yaliyowekwa na Msimamizi wa Zimamoto wa Jimbo na sheria hii;

2. Kuna mabadiliko ya Mkurugenzi wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto; au

3. Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaomba idhini ya ujenzi, nafasi ya ziada ya kutumika, au mfumo wa joto unahitaji kubadilishwa.

**H. Ondoleo**

1. **Ombi la Ondoleo.** Idara inaweza, baada ya ombi lililoandikwa na mwombaji au Kituo chochote cha Utunzaji wa Watoto kuondoa au kurekebisha kifungu cha Sheria hizi ambacho hakijaamriwa na jimbo la Maine au sheria ya kitaifa. Kituo cha Utunzaji wa Watoto au mwombaji atatoa ushahidi wazi na wa kuridhisha, ikijumuisha kama inavyoombwa na Idara, maoni ya kitaalamu ambayo yanairidhisha Idara kwamba Kituo cha Utunzaji wa Watoto au njia mbadala ya mwombaji itatii dhamira ya kanuni ambayo inasababisha kuombwa kwa ondoleo au marekebisho. Maombi ya ondoleo au marekebisho lazima yajumuishe:

   a. Taarifa ya kanuni ambayo inasababisha kuombwa kwa ondoleo au marekebisho;

   b. Maelezo ya sababu kwa nini masharti hayawezi kutimizwa na kwa nini ondoleo au marekebisho yanaombwa; na

   c. Ufafanuzi wa mbinu mbadala iliyopendekezwa ili kutimiza dhamira ya kanuni ambayo mwombaji angependa iondolewe au kurekebishwa.

2. **Kukubaliwa au Kukataliwa kwa Ombi la Ondoleo.** Idara itakubali au kukataa ombi la ondoleo, kwa maandishi, ndani ya wiki nne baada ya kupokea ombi la ondoleo. Uamuzi ulioandikwa wa Idara utaeleza sababu za kukubaliwa au kukataliwa kwa Ombi la Ondoleo. Likikubaliwa, ondoleo hilo litawekewa kikomo cha muda wa Leseni; na nyongeza itatolewa ikiwa maslahi ya Mtoto/watoto yatazingatiwa.

## SEHEMU YA 3. ADA

**A. Ada.**

**1.** Ada ya leseni lazima iwasilishwe kwa kila ombi la leseni, kama itakavyoelekezwa na Idara.

**2.** Ada za utoaji leseni hazirejeshwi.

**3.** Ada za maombi ya leseni na usasishaji zitawekwa kulingana na uchambuzi wa gharama za Idara wa kutoa leseni. Ada hizi hazitazidi gharama ya kutoa leseni.

**4.** Kuchelewa kuwasilisha ombi la kusasisha leseni kutasababisha kuisha kwa muda wa leseni.

**B. Ada za taasisi zinazowahudumia Watoto 3 hadi 12.**

**1.** Ada ya maombi ya leseni ya muda mfupi ni $120.00.

**2.** Ada ya maombi ya leseni kamili au usasishaji wa miaka miwili ni $240.00.

**C. Ada za taasisi zinazowahudumia Watoto 13 au zaidi.**

**1.** Ada ya maombi ya leseni ya muda mfupi ni $120.00.

**2.** Ada ya maombi ya leseni kamili au usasishaji wa miaka miwili ni $240.00.

**D. Ada za Shule za Chekechea** Ada ya maombi ya leseni ya muda mfupi, ya kusasishwa au leseni kamili kwa Shule ya Chekechea ni $10.00.

## SEHEMU YA 4. UKAGUZI NA UCHUNGUZI

**A.** **Ukaguzi.** Idara kwa ujumla hufanya ukaguzi wa kituo bila kutangaza. Idara inaweza kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa hiari yake. Ukaguzi wa mara kwa mara hufanyika katika nyakati zifuatazo:

**1.** Baada ya kuwasilisha ombi;

**2.** Kila mwaka, baada ya tarehe ya kwanza ya leseni;

**3.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kikiomba kuboresha uwezo, mabadiliko ya majengo au huduma, mabadiliko au mapendekezo ya mabadiliko ya msimamizi, maelezo ya mpango, kituo halisi au huduma;

**4.** Kuchunguza madai ya ukiukaji wa kanuni, au madai ya unyanyasaji na/au utelekezaji unaoshukiwa;

**5.** Kwa ufuatiliaji wa kawaida wa utunzaji, ikijumuisha kubaini kufuata Mpango wa Utekelezaji au Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa ili kuhakikisha kuwa mapungufu yaliyotajwa yamerekebishwa.

**B.** **Haki ya kuingia**

**1.** Wahudumu wa Idara wana haki ya kuingia ndani ya majengo ya Kituo chochote cha Utunzaji wa Watoto kilichoidhinishwa, wakati wowote mwafaka, kwa mujibu wa 22 MRS §7804.

**2.** Wahudumu wa Idara wanaweza kuingia katika jengo la Kituo cha Utunzaji wa Watoto au la mtu binafsi aliyeripotiwa au kushukiwa kuhudumu bila leseni, kwa ruhusa tu ya mmiliki au msimamizi, kwa mujibu wa 22 M.R.S. §7702-B(7), au wakiwa na hati ya upekuzi kutoka kwa Mahakama ya Wilaya inayoidhinisha kuingia na kukagua, kama ilivyoonyeshwa hapa chini, kwenye 22 M.R.S. §7804.

**a.** Idara na afisa aliyeteuliwa ipasavyo au mhudumu wa Idara wana haki ya kuingia katika majengo ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto kisichoidhinishwa wakiwa na hati ya ukaguzi wa kiutawala iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni za Maine za Mwenendo wa Raia, Kanuni ya 80E, na Mahakama ya Wilaya, kwa wakati unaofaa na, wakiagiza, wana haki ya kukagua na kunakili vitabu vyovyote, uhasibu, karatasi, kumbukumbu na hati zingine ili kubaini hali ya kutii kifungu hiki. Kwa mujibu wa Kanuni za Maine za Utaratibu wa Kiraia, Kanuni ya 80E, haki ya Idara ya kuingia na kukagua inaweza kujumuisha majengo na hati zozote za mtu, kampuni, ubia, chama, shirika au taasisi nyingine ambayo Idara ina sababu ya kuamini kuwa inafanya kazi bila leseni.

**b.** Mmiliki au msimamizi wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kisicho na leseni hawezi kuingilia, au kukataza mahojiano ya watumiaji wa huduma za utunzaji wa Watoto na yanayofanywa na Idara.

**C.** **Vipengele vya ukaguzi.** Ili kubaini utiifu wa sheria hii, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiruhusu ufikiaji wa rekodi zote na sehemu yoyote ya majengo yanayowahudumia au kutumiwa na Watoto.

**1.** Wahudumu wa Idara wanaweza kuzungumza na Watoto, wazazi, na Wahudumu wa Watoto wakati wa ukaguzi.

**2.** Wahudumu wa Idara wanaweza kupiga picha sehemu yoyote ya majengo au kupiga picha hati. Idara itakipa Kituo cha Utunzaji wa Watoto nakala za picha zilizopigwa ikiwa kitaomba.

**D.** **Ripoti ya ukaguzi.** Idara itanukuu matukio yote ya ukiukaji wa sheria hii kwenye ripoti ya ukaguzi na itaeleza ukiukaji wowote uliogunduliwa wakati wa ukaguzi. Wahudumu wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto wanaweza kusahihisha ukiukaji wakati wa ukaguzi. Ukiukaji wote uliorekebishiwa kituoni utanukuliwa kwenye ripoti ya ukaguzi. Kituo cha Utunzaji wa Watoto na Idara zitaamua Mpango wa Utekelezaji, ili kujumuisha muda wa kurekebisha, kwa ukiukaji wowote ambao hauwezi kusahihishwa wakati wa ukaguzi.

1. Ikiwa Mpango wa Utekelezaji hauwezi kubainishwa wakati wa ukaguzi, Mpango wa Utekelezaji lazima uanzishwe na Kituo cha Utunzaji wa Watoto na Idara ndani ya siku tano za kazi baada ya ukaguzi.

2. Kufuatia ukaguzi huo, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kithibitishe kwamba kinatii kanuni za Mpango wa Utekelezaji ulioandikwa.

**E.** **Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa.** Kufuatia ukaguzi au uchunguzi, Idara inaweza kutoa Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa kwa sababu ya kutofuata sheria hii.

1. Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa utafafanua sheria ambazo Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakikufuata katika kanuni hii na kitaagiza hatua zinazopaswa kukamilishwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto ili kutii sheria hii, pamoja na muda wa marekebisho.

2. Kukosa kutii Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa kunaweza kusababisha kuchukuliwa hatua ya utekelezaji, hadi na kujumuisha kubatilishwa kwa leseni kwa mujibu wa Kifungu cha 21 cha sheria hii.

**F.** **Uchunguzi.** Idara itajibu ripoti ya mtu yeyote anayedai kuwa kumekuwa na ukiukaji wa kanuni za leseni au unyanyasaji na utelekezaji wa Mtoto.

1. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kishirikiane katika hatua zote za uchunguzi wa madai ya unyanyasaji na utelekezaji, kwa mujibu wa 22 MRS Sura ya 1674. Ushirikiano unajumuisha, lakini si tu, yafuatayo:

   a. Mmiliki au Mkurugenzi wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto hawezi kuzuia Idara kuwahoji kwa faragha Wahudumu wa Watoto;

   b. Kuruhusu mahojiano ya faragha yanayofanyiwa Watoto, kwa idhini au bila idhini ya mzazi, kwa mujibu wa 22 MRS Sura ya 1674;

   c. Kutoa taarifa za mawasiliano kwa familia za Watoto waliojisajili, kufuatia ombi la Idara;

   d. Kuwezesha ufikiaji wa rekodi zote za Watoto;

   e. Kuwezesha ufikiaji wa rekodi zote za Wahudumu wa Watoto wa sasa na wa zamani, ikijumuisha ufikiaji wa kadi za saa na nyenzo zingine za malipo kufuatia ombi;

   f. Kuwezesha ufikiaji wa rekodi zote za matukio na ripoti ya ajali; na

   g. Kuwezesha ufikiaji wa sehemu zote za Kituo cha Utunzaji wa Watoto kilichoidhinishwa, ikijumuisha maeneo ambayo hayatumiki kwa Utunzaji wa Watoto.

2. Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakipaswi kulipiza kisasi dhidi ya mwandishi yeyote au mwakilishi wake kwa kuwasilisha malalamiko. Ukiukaji wowote wa sheria uliotambuliwa kutokana na uchunguzi wa malalamiko utatolewa kwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa maandishi.

## SEHEMU YA 5. REKODI USIMAMIZI NA UHIFADHI

**A.** **Rekodi usimamizi.** Vituo sharti vitii yafuatayo:

**1.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihifadhi faili tofauti kwa kila Mhudumu wa Watoto, na Mtoto aliyehudumiwa. Rekodi hizi lazima zihifadhiwe na Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa muda usiopungua miaka mitatu baada ya Mtoto kuondoka kituoni au Mhudumu wa Watoto kuacha kazi. Rekodi za Mtoto na Mhudumu lazima ziwasilishwe ili zikaguliwe na Idara.

**2.** Rekodi zote za mahudhurio lazima zijumuishe tarehe, mwaka, saa za kuanza na za kukamilisha mahudhurio ya kila siku kwa kila kikundi cha Watoto. Orodha hii lazima iwasilishwe kwa ukaguzi na Idara na kuwekwa kituoni kwa miaka mitatu.

**3.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kirekodi saa halisi za kazi na muda wa mapumziko ambapo Wahudumu wa Watoto hawana uwezo wa kutoa huduma ya utunzaji na hawajahesabiwa kwenye uwiano wa wahudumu na Watoto. Rekodi hii lazima iwasilishwe kwa ukaguzi na Idara na kuwekwa kituoni kwa miaka mitatu.

**4.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihifadhi rekodi tofauti ya ripoti zote za madai ya unyanyasaji na/au utelekezaji wa watoto kwa mujibu wa 22 MRS §4011-A.

**5.** Rekodi ya mazoezi ya kutoroka moto kwa miaka mitatu iliyotangulia lazima iwasilishwe ili kukaguliwa na Idara; Idara ya Usalama wa Umma, Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto wa Jimbo, na wakaguzi wa ndani wa zimamoto.

**6.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitayarishe na kufuata sera ya usimamizi na hifadhi ya rekodi, ambayo lazima ijumuishe masharti ya ufikiaji wa rekodi za Watoto na walezi wa kisheria.

**7.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima vihifadhi rekodi wazi, zinazoweza kusomeka katika mpangilio bora na unaoweza kufikiwa.

**8.** Rekodi ya chanjo ya kichaa cha mbwa kwa wanyama wote vipenzi kwenye majengo.

**9.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinavyotoa shughuli za kuogelea na kutembea ndani ya maji lazima viweke rekodi iliyoandikwa ya aina, tarehe, saa na kipindi cha mafundisho ya taratibu za dharura za usalama wa maji na mazoezi yanayohitajika katika Sehemu ya 15 ya Kanuni hii.

**B.** **Kutunga rekodi ghushi.** Kutunga rekodi ghushi na hatia ya Daraja la D chini ya sheria ya 17-A MRS §453 na unaweza kusababisha Idara ichukuliwe hatua.

**C.** **Ukaguzi wa rekodi**. Rekodi lazima ziwasilishwe kwa ukaguzi baada ya ombi la Idara, bila idhini ya Mtoto au mlezi wake wa kisheria.

**1.** Wahudumu wa Watoto walioidhinishwa pekee ndio wanaoweza kufikia rekodi za shirika, kwa msingi wa haja ya kufahamu.

**2.** Katika saa za kazi, Wahudumu wa Watoto walioidhinishwa katika kila eneo la huduma lazima waweze kupata na kufikia rekodi zinazohifadhiwa nje ya kituo.

**D.** **Rekodi za Watoto.** Rekodi za watoto lazima zihifadhiwe katika sehemu moja kuu na zinaweza tu kufikiwa na Wahudumu wa Watoto walioidhinishwa. Rekodi za watoto lazima zisasishwe kila mwaka na kudumishwa kwa hali yenye mpangilio bora.

**1.** Rekodi lazima ijazwe wakati wa kusajiliwa na kudumishwa katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa kila Mtoto anayetunzwa (pamoja na jamaa) na lazima ijumuishe:

**a.** Jina, tarehe ya kuzaliwa, anwani ya mtaa na anwani ya barua ya posta ya Mtoto;

**b.** Jina, anwani ya mtaa, anwani ya barua ya posta na nambari ya simu ya mzazi (wazazi) au mlezi (walezi) wa kisheria;

**c.** Mahali pa ajira pa mzazi (wazazi) au mlezi (walezi) wa kisheria ikiwa wameajiriwa;

**d.** Nambari ya simu ya sasa ya mzazi (wazazi) au mlezi (walezi) wa kisheria;

**e.** Mbinu ya kuwasiliana na mzazi (wazazi) au (mlezi) walezi wa kisheria wakati Mtoto yupo kwenye utunzaji;

**f.** Jina na nambari ya simu ya mtu mwingine mbali na mzazi (wazazi) au (mlezi) walezi wa kisheria wa kuwasiliana naye iwapo mzazi (wazazi) hawezi kupatikana katika hali ya dharura;

**g.** Nakala ya makubaliano ya kifedha na mzazi (wazazi) au (mlezi) walezi wa kisheria;

**h.** Tarehe za usajili na kukomeshwa;

**i.** Rekodi za chanjo lazima zihifadhiwe kwa ajili ya kila Mtoto anayehudhuria mpango, ikiwa ni pamoja na jamaa na Watoto wa Wahudumu wa Watoto ambao wanahudhuria mpango zaidi ya siku moja kila mwezi;

**j.** Majina na nambari za simu za daktari wa Mtoto na daktari wa meno wa familia. Ikiwa hakuna daktari wa familia au daktari wa meno aliyetambuliwa, ni lazima ibainishwe kwenye fomu ya rekodi ya Mtoto;

**k.** Idhini iliyowekwa saini ya kupewa dawa, ikihitajika;

**l.** Idhini iliyowekwa saini ya kupewa huduma ya matibabu ya dharura;

**m.** Majina ya watu ambao wanaruhusiwa na mzazi (wazazi) au (mlezi) walezi wa kisheria kumwondoa Mtoto kwenye jengo la kituo;

**n.** Rekodi ya siku hiyo hiyo ya majeraha yote, ikijumuisha majeraha mabaya, Ajali na Matukio au mambo ya dharura, ambayo inaonyesha saa na tarehe ya arifa ya matamshi au maandishi ya Mzazi au Mlezi wa Kisheria. Sahihi ya Mzazi au Mlezi wa Kisheria lazima iwekwe kwenye ripoti ya Tukio ndani ya saa 48 baada ya tukio.

**o.** Rekodi iliyoandikwa ya mabadiliko makubwa ya mwonekano na/au usafi anapowasili, au mabadiliko makubwa ya tabia (kama vile: kuongezeka kwa vurugu, kutoshiriki shughuli, tabia ya kingono, na/au hasira za muda mrefu) na hali nyingine za afya, ikiwa zinajulikana;

**p.** Mizio inayojulikana, na hali zingine za kiafya, pamoja na mipango inayohusiana ya kiafya inapohitajika,

**q.** Hati zozote husika zinazohitajika kimatibabu (kwa mfano, kulala kwa mkao usio wa hali mlalo au kutotumia mafuta ya kujikinga na jua), ikihitajika;

**r.** Ithibati iliyowekwa saini na mzazi au mlezi wa kisheria kuthibitisha kwamba amepokea na kusoma kijitabu cha mwongozo wa mpango;

**s.** Ruhusa iliyowekwa saini ya matumizi au usambazaji wa picha au taarifa za kibinafsi za Mtoto kwenye machapisho yoyote, mitandao ya kijamii au nyenzo za matangazo;

**t.** Ruhusa iliyowekwa saini na wazazi wa Mtoto kabla ya kumruhusu Mtoto kushiriki katika shughuli yoyote hatari, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu kuogelea, kuendesha farasi na kutumia turubali. Ruhusa lazima itolewe upya angalau kila mwaka, na ionyeshe aina na eneo la shughuli:

**u.** Ruhusa iliyoandikwa na mzazi/mlezi ya kuruhusu matumizi ya mafuta ya kujikinga na jua;

**v.** Ruhusa iliyowekwa saini ya kumsafirisha Mtoto, ikihitajika; na

**w.** Ruhusa iliyowekwa saini ya kumruhusu Mtoto kuondoka kwenye jengo la kituo.

**2.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima viweke maelezo yaliyoandikwa kwenye rekodi ya Mtoto vikieleza kwa nini taarifa zozote zinazohitajika hazipo.

**E.** **Rekodi za wahudumu.** Rekodi ya wahudumu sharti iwekwe kwa ajili ya Wahudumu wote wa Utunzaji wa Watoto.

**1.** Rekodi za wahudumu lazima zihifadhiwe katika sehemu moja kuu na ya faragha kila wakati na zinaweza tu kufikiwa na Wahudumu wa Watoto walioidhinishwa.

**2.** Rekodi ya wahudumu lazima iwe na:

**a.** Jina, anwani ya sasa ya mtaa na ya barua ya posta, tarehe ya kuzaliwa na nambari ya simu ya sasa;

**b.** Hati za mafundisho yanayoendelea,

**c.** Tarehe za kuajiriwa na kusimamishwa kazi kwa Wahudumu wa Watoto. Sababu za kusimamishwa kazi lazima zihifadhiwe katika rekodi ya wahudumu kwa angalau mwaka mmoja;

**d.** Taarifa iliyowekwa saini, na tarehe na kila Mhudumu wa Watoto inayothibitisha kuwa amesoma na kuelewa kanuni ya sasa ya utoaji leseni;

**e.** Taarifa iliyowekwa saini na tarehe na kila Mhudumu wa Watoto inayothibitisha amesoma na kuelewa sera za wahudumu wa mpango, sera za usajili na kijitabu cha mwongozo kwa Wazazi;

**f.** Hati za hatua yoyote ya kinidhamu;

**g.** Hati za uchunguzi uliokamilishwa na ustahiki wa kuajiriwa zilizotolewa na Idara, kwa mujibu wa 45 CFR § 98.43; na

**h.** Hati za uchunguzi wa kimatibabu unaothibitisha kuwa wahudumu hawana magonjwa ya kuambukiza, kama inavyohitajika kwa Wahudumu wa Watoto wa Shule ya Chekechea kwa mujibu wa 22 MRS §8402 (3)(A).

**i.** Elimu, uzoefu na sifa nyinginezo;

**j.** Tathmini ya kila mwaka ya utendaji wa kila Mhudumu wa Watoto na Mkurugenzi au msimamizi wa karibu iliyowekwa saini na Mkurugenzi na mtathmini; na

**k.** Rekodi za chanjo.

**l.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kinukuu mipango yote ya utangulizi na mafundisho ya Wahudumu wote wa Huduma ya Watoto kwa uthibitisho wa kukamilishwa kwa mipango hii kutoka kwa mtu aliyehitimu, kupitia mbinu ya mtandaoni au ya mtu kibinafsi.

**3.** Wahudumu Wanaoshughulikia Huduma kwa Watoto wanaweza kukagua, kuongeza na kusahihisha taarifa zilizo katika rekodi zao. Ufikiaji wa rekodi za wahudumu waliopo na walioondoka unaweza tu kufanywa na Wahudumu wa Watoto walioidhinishwa kwa msingi wa haja ya kufahamu.

## SEHEMU YA 6. MASHARTI YA KURIPOTI

**A. Mabadiliko ya utunzaji wa watoto.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima vitume arifa iliyoandikwa kwa Idara kuhusu yafuatayo, ndani ya saa 24 baada ya kutokea:

**1.** Kufungwa kwa muda mrefu au kwa daima, na tarehe inayotarajiwa ya kufungwa;

**2.** Mabadiliko yoyote ya mfumo wa joto, mabadiliko yoyote ya kimuundo au mipango yoyote ya kutumia nafasi iliyopo kwenye kituo ambayo haijakaguliwa na kuidhinishwa. Hii inajumuisha mabadiliko yoyote ya kiasili au kimuundo katika jengo (majengo) au kwa misingi kama vile, lakini si tu, marekebisho, ukarabati, maboresho ya uwanja wa michezo au kujenga bwawa la kuogelea.

**3.** Mabadiliko yoyote ya nambari za simu au maelezo ya mawasiliano ya barua pepe.

**B. Ripoti ya lazima ya tuhuma za Kuwanyanyasa na/au kuwatelekeza watoto.** Mhudumu yeyote wa Watoto anayeshuku kuwa unyanyasaji na/au utelekezaji unafanyika lazima aripoti habari hii mara moja kwa idara ya Usajili na Ulinzi wa Watoto, kupita 1-800-452-1999, TTY 1-800-963-9490 ambayo ina wahudumu wa saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki.

**1.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihifadhi hati ambazo hazijahifadhiwa katika rekodi ya Watoto, ili kuhakikisha kwamba ripoti imefanywa.

**2.** Ripoti zote za tuhuma za unyanyasaji na/au utelekezaji wa Watoto, na majeraha mabaya ya Mtoto aliye na umri wa chini ya miezi sita au yasiyoathiri uwezo wa kutembea, sharti zifuate sheria ya 22 MRS §4011-A.

**C. Kuripoti kwa Idara matokeo mabaya ya maji ya kunywa.** Kwa Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinavyotakiwa kupima maji ya visima kwa mujibu wa Kifungu cha 13(A) hadi (C) cha sheria hii, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiripoti viwango vya ubora wa maji visivyoridhisha kwa Idara ndani ya saa 24 baada ya kupokea matokeo. Matokeo yasiyoridhisha ya ubora wa maji yanajumuisha viwango vyovyote vilivyoripotiwa na maabara vinavyozidi viwango ndani ya 10-144 CMR Sura ya 231, Kanuni Zinazohusiana na Maji ya Kunywa, Mpango wa A.

**D. Kuripoti kuharibika kwa mfumo wa maji machafu.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiarifu Idara na mkaguzi wa mabomba wa eneo ikiwa mfumo wa kutupa maji machafu utashindwa kufanya kazi ipasavyo.

**E. Kuripoti kuhusu hatua za kisheria.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiitumie kwa Idara ripoti iliyoandikwa ya mashtaka yoyote ya kisheria kati ya yafuatayo yaliyowasilisha dhidi ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto au Mhudumu yeyote wa Watoto aliyeajiriwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto ndani ya saa 24:

**1.** Mashtaka yoyote yanayotokana na hali zinazohusiana na utunzaji wa Watoto katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto; au

**2.** Mashtaka yoyote yanayoweza kuathiri utendakazi endelevu wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto; au

**3.** Kukamatwa, kushtakiwa au kuhukumiwa kwa sababu ya uhalifu wa kingono au ukatili unaowahusisha Watoto au watu wazima, au vitendo vyovyote haramu vinavyohusisha Watoto, iwe washukiwa wamefunguliwa mashtaka au la;

**4.** Kukamatwa, kushtakiwa au kuhukumiwa kwa kufanya kazi mtu akiwa amelewa au akiwa na kiwango cha juu cha kileo katika damu (OUI), au kwa sababu ya shughuli nyingine yoyote inayohusisha matumizi mabaya ya dawa za kulevya;

**5.** Uchunguzi wa Huduma za Kinga ya Mtoto;

**6.** Kuondolewa kwa Watoto kwenye utunzaji au huduma ya Mwenye Leseni wa Kituo cha Utunzaji kwa amri ya mahakama;

**7.** Ulinzi wowote dhidi ya amri ya unyanyasaji au amri nyingine yoyote ambayo inatambua Matokeo ya unyanyasaji wa nyumbani au vurugu za familia.

**8.** Pamoja na kuarifu Idara kwa maandishi kuhusu mashtaka yoyote ya kisheria kati ya yaliyo hapa juu, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiipe Idara idhini iliyoandikwa inayoiruhusu Idara kuchukua taarifa kuhusu mashtaka yaliyo hapa juu kutoka kwenye chanzo chochote.

**9.** Taarifa zinazotilia shaka ufaafu wa Mhudumu yeyote wa Watoto kuwatunza Watoto, ikijumuisha:

**i.** Hali yoyote inayohusiana na afya ya kimwili, afya ya akili au matumizi mabaya ya dawa za kulevya ambayo inaweza kutatiza uwezo wa mtu wa kutekeleza majukumu yake kwa usalama;

**ii.** Taarifa nyingine yoyote kuhusu hali ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto au matibabu ya Watoto, kama vile jeraha baya au kifo cha Mtoto katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto, ili kuwezesha Idara kubaini kama kuna tishio la afya, usalama na ustawi wa Watoto.

**10.** Iwapo taarifa kama ilivyoelezwa hapa juu ipo, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiitumie Idara idhini zilizoandikwa zinazoiruhusu Idara kuchukua taarifa kuhusu mojawapo ya masuala haya kutoka kwa maafisa au watu mwafaka ili kubaini kama kuna tishio la afya, usalama na ustawi ya Watoto.

**F.** **Taarifa Nyinginezo.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiiarifu Idara kuhusu mambo yafuatayo ndani ya saa 24 baada ya kutokea:

**1.** Vifo vyote na majeraha mabaya ya Watoto ambayo yanahitaji kushughulikiwa kimatibabu na mtoa huduma wa matibabu aliyeidhinishwa, baada ya kuwaarifu wahudumu wa matibabu ya dharura na wazazi/walezi wa Mtoto;

**2.** Madai yoyote ya unyanyasaji na utelekezaji wa Watoto yanayomtaja Mhudumu yeyote wa Watoto anayehusiana na Kituo cha Utunzaji wa Watoto, pamoja na ripoti ya papo hapo inayotumwa kwenye idara ya Usajili na Ulinzi wa Watoto inayohitajika katika Sehemu ya 6(B) hapa juu;

**3.** Tabia ya kingono ya Mtoto dhidi ya Mtoto mwingine, ufichuzi wa uchi wa makusudi au kugusana makusudi;

**4.** Ukiukaji wowote wa haki za Watoto ulioorodheshwa katika Sehemu ya 10 ya kanuni hii;

**5.** Mabadiliko yoyote ya umiliki;

**6.** Mabadiliko yoyote ya mtu aliyeteuliwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto au baraza tawala kuwa Mkurugenzi aliyehitimu.

**7.** Mabadiliko yoyote yanayotarajiwa ya mahali kilipo kituo:

**a.** Ikiwa kituo kitahamishwa kwa sababu ya hali ya dharura ambayo ilifanya eneo lililoidhinishwa kutotumika kwa muda; au

**b.** Iwapo kitahamishwa kabisa, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitume ombi la kupewa leseni ya eneo jipya. Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakiwezi kufanya kazi hadi Idara itoe leseni mpya ya eneo jipya.

**c.** Hatua za Idara kuhusu ripoti. Katika kuamua hatua ya kuchukuliwa kuhusu Leseni chini ya

hali zilizoorodheshwa hapa juu, Idara itaamua kama Kituo cha Utunzaji wa Watoto kimewasilisha ushahidi wa kutosha kuonyesha kwamba matatizo yaliyosababisha mojawapo ya hali zilizo hapa juu yametatuliwa vya kutosha hivi kwamba Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitaweza kutii Kanuni hizi.

## SEHEMU YA 7. UWIANO WA WAHUDUMU NA WATOTO, USIMAMIZI NA USTAHIKI

**A.** **Watoto wa umri wa chini ya wiki 6.** Hakuna Mtoto aliye na umri wa chini ya wiki sita, kama ilivyothibitishwa na cheti cha kuzaliwa au rekodi ya chanjo, anaweza kuwekwa katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**B.** **Vizuizi vya uwezo.**

**1.** Watoto wa Wahudumu lazima wahesabiwe katika vikundi vya umri vinavyofaa, na katika kubaini uwiano wa wahudumu kwa watoto, na uwezo wanapokuwa katika utunzaji kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**2.** Idadi ya Watoto wanaoruhusiwa inaweza kudhitiwa na Idara ikiwa mojawapo ya hali zifuatazo itatokea:

**a.** Nafasi ni chache au imepangwa kwa namna isiyo ya kawaida;

**b.** Mhudumu wa Watoto ana mapungufu ya kimwili ambayo yanaweza kuathiri uwezo wa Mhudumu wa Watoto wa kutunza, kusimamia au kushughulikia kwa njia salama mahitaji ya Watoto wanaotunzwa.

**C.** **Uwiano wa Wahudumu na Watoto.**

**1.** Idadi ya Watoto waliopo lazima isizidi uwezo ulioidhinishwa.

**2.** Idadi ya juu zaidi ya Watoto watakaokabidhiwa kila mtu mzima, bila kujumuisha Wahudumu walio na jukumu la kimsingi la ukarani, mapishi na matengenezo, lazima iwe kama ifuatavyo:

**a.** Masharti ya uwiano ya taasisi ndogo zinazowahudumia Watoto 3 hadi 12:

| UMRI WA WATOTO | UWIANO WA WAHUDUMU WA KITUO CHA UTUNZAJI NA WATOTO | | |
|---|---|---|---|
| Wiki 6 hadi miaka 2 | 1:4 | 2:8 | 3:12 |
| Miaka 2 hadi miaka 5 | 1:8 | 2:12 | Haitumiki |
| Zaidi ya miaka 5 | 1:12 | Haitumiki | Haitumiki |
| Umri mseto | Mhudumu 1:<br>Watoto 3 wa umri wa chini ya miaka 2 +<br>Watoto 3 wa umri wa 2 hadi 5 +<br>Watoto 2 wa umri wa zaidi ya miaka 5,<br>**au**<br>Watoto 8 wa umri wa 2 hadi 5 +<br>Watoto 2 wa umri wa zaidi ya miaka 5. | Wahudumu 2:<br>Watoto 6 wa umri wa chini ya miaka 2 + Watoto 6 wa umri wa zaidi ya miaka 2. | Wahudumu 3:<br>Watoto 12<br>(Watoto wasiozidi 9 wanaweza kuwa wa umri wa chini ya miaka 2). |

**b.** Masharti ya uwiano kwa vituo vinavyowahudumia Watoto 13 au zaidi:

| UMRI | UWIANO WA WAHUDUMU WA KITUO CHA UTUNZAJI NA WATOTO | UPEO WA UKUBWA WA KUNDI |
|---|---|---|
| Wiki 6 hadi mwaka 1 | 1:4 | 8 |
| Mwaka 1 hadi miaka 2 ½ | 1:4<br>1:5 | 12<br>10 |
| Miaka 2 ½ hadi 3 ½ | 1:7 | 21 |
| Miaka 3 hadi - Chini ya miaka 5 | 1:8<br>1:10 | 24<br>20 |
| Miaka 5 (Umri wa kwenda shule) hadi miaka 12 | 1:13 | Haitumiki |

**c.** Masharti ya uwiano kwa mipango ya Shule za Chekechea.

| UPEO WA UKUBWA WA KUNDI | UWIANO WA WAHUDUMU WA KITUO CHA UTUNZAJI NA WATOTO |
|---|---|
| 30 | 1:12 |

**3.** Mipango ya utunzaji wa watoto inayowahudumia Watoto 13 au zaidi:

**a.** Mhudumu mmoja wa Watoto anaweza kutoa huduma katika darasa moja ndani ya jengo kwa Watoto wasiozidi sita, licha ya umri wao, kwa muda usiozidi saa moja mwanzoni, na mwisho wa saa za kazi zilizoainishwa.

**b.** Angalau Wahudumu wawili wa Watoto lazima wawepo katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto ikiwa kuna Watoto saba au zaidi, licha ya umri wao.

**c.** Ukubwa wa kikundi na idadi ya Wahudumu wanaohitajika wa Kutunza Watoto lazima ibainishwe kulingana na umri wa Mtoto mchanga zaidi, wakati kuna watoto wa umri mbalimbali ndani ya kikundi.

**d.** Watoto Wakubwa zaidi wanaweza kujaza nafasi za Watoto wadogo, lakini Watoto wadogo hawawezi kujaza nafasi za Watoto wakubwa.

**e.** Hafla maalum zinazoandaliwa Kituoni lazima ziwezeshe usimamizi kwa mujibu wa sheria hii. Mtoto anayehudhuria hafla maalum chini ya uangalizi wa mzazi au mlezi wa kisheria hatajumuishwa katika uwiano wa wahudumu na Watoto. Hafla maalum zinazoandaliwa nje ya saa na siku za kawaida hazipaswi kujumuishwa chini ya sheria hii.

**D. Usimamizi.**

**1.** Watoto lazima wasimamiwe kila wakati.

**a.** Katika Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinavyowahudumia Watoto 3 hadi 12, Wahudumu wa Watoto lazima wafahamu shughuli na mahali alipo kila Mtoto aliye chini ya utunzaji wao.

**i.** Wahudumu wa Watoto lazima waweze kuwaona au kuwasikia Watoto wote wakati wote na waweze kuchukua hatua ya haraka inapohitajika.

**ii.** Wahudumu wa Watoto lazima wawepo nje wakati Watoto wa umri wa chini ya miaka minane wako nje.

**iii.** Iwapo Watoto wa umri wa zaidi ya miaka minane wako nje na Mhudumu wa Watoto hayupo binafsi, eneo la kuchezea lazima liwe limefungwa kwa ua na kituo lazima kiwe kinatii Kifungu cha 7(D)(1)(a)(i) cha kanuni hii.

**b.** Katika Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinavyowahudumia Watoto 13 au zaidi, Mhudumu wa Watoto lazima aweze kuwaona na kuwasikia Watoto wote, kuwajibikia shughuli inayoendelea ya Watoto, na kuwa na uwezo wa kuchukua hatua ya haraka inapohitajika.

**2.** Watoto wanapopangwa katika makundi kulingana na umri katika mipango inayowahudumia Watoto 13 au zaidi, vikundi vya Watoto lazima viwe ndani ya chumba binafsi, au eneo mahususi ndani ya chumba kikubwa, vikitenganishwa kwa kizigeu kinachotenganisha vikundi vya Watoto kimwonekano na kimwili. Eneo hili lazima libainishwe kwa kizuizi kinachoonekana, kizigeu au kigawanyaji kingine cha chumba chenye urefu juu ya upeo wa macho wa Watoto ambao watatumia eneo hilo.

**3.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwasimamize Watoto moja kwa moja, kupitia Wahudumu walio macho, huku pia kikikudumisha uwiano wa wahudumu na Watoto wakati wa mapumziko na/au kulala.

**a.** Mhudumu Mmoja wa Watoto anaweza kuondoka kwenye vikundi kwa muda usiozidi dakika tano ili kushughulikia mahitaji ya kibinafsi au ya mpango, ili mradi tu Mhudumu huyo anaendelea kupatikana wakati wa dharura.

**b.** Mwangaza uliofifishwa, lakini wa kutosha, ili kuwezesha usimamizi ambapo Watoto wote wanaonekana lazima udumishwe kila wakati.

**c.** Wafuatiliaji wanatumia video na sauti wanaweza kuchukuliwa kuwa njia inayokubalika ya usimamizi katika nafasi ya kulala iliyo karibu. Watoto Wanaolala lazima wakaguliwe kibinafsi angalau kila dakika 30.

**4.** Wahudumu wa Watoto lazima wamhudumie Mtoto anayelia au kuitana.

**E. Mpango wa kukabiliana na majanga.** Kituo lazima kiandae na kufuata mpango ulioandikwa wa kutafuta usaidizi wakati wa dharura ikiwa ni Mhudumu mmoja tu wa Watoto anayepatikana.

**F. Ustahiki wa Wahudumu.**

**1.** Wahudumu wote wa Watoto wanaofanya kazi bila usimamizi lazima wawe na umri wa angalau miaka 18. Wahudumu wa Watoto wa umri wa miaka 16 na 17 lazima wasimamiwe moja kwa moja na mhudumu mwingine aliye na umri wa zaidi ya miaka 18.

**a.** Wahudumu wote wa Watoto lazima wawe na cheti cha shule ya upili au cheti sawia, wawe wakihudhuria shule ya upili, au wawe wamejiandikisha katika mpango wa maandalizi ya Ukuzaji wa Elimu ya Jumla (GED) au mpango wa maandalizi ya Mtihani wa Usawa wa Shule ya Upili (HiSET).

**b.** Wahudumu wote wa Watoto lazima wathibitishe yafuatayo:

**i.** Uwezo na nia ya kutii sheria na kanuni zote zinazotumika;

**ii.** Uwezo wa kutoa huduma salama na za ukarimu;

**iii.** Historia ya uaminifu na tabia halali; na

**iv.** Wahudumu wa Watoto wanaofanya kazi peke yao hawafai kuwa na mapungufu ya kimwili ambayo yanaweza kuathiri uwezo wao wa kutunza, kusimamia au kushughulikia kwa njia salama mahitaji ya Watoto wanaotunzwa.

**c.** Wahudumu wote wa Watoto wanaowajibikia, au kusaidia katika utunzaji wa Watoto lazima wawe na uwezo wa kufanya maamuzi bora katika kuwahudumia Watoto, wathibitishe kuwa wanatii kila mara kanuni hii na sheria zote zinazohusika, na hawapaswi kujihusisha katika vitendo au tabia yoyote inayodhuru ustawi wa Watoto.

**2.** Wahudumu wote wa Watoto lazima waweze kutekeleza majukumu waliyopewa na kutimiza masharti yote yaliyo katika sheria hii. Wahudumu walio kazini hawaruhusiwi kutumia pombe, tumbaku, bangi ya burudani au dawa za kulevya. Dawa zilizoagizwa au Dawa zilizoidhinishwa ambazo haziathiri uwezo wa Mhudumu wa Watoto wa kutunza Watoto zinaruhusiwa.

**3.** Vituo vilivyoidhinishwa kwa watoto 3 - 12 lazima vimwajiri mtunzaji wa msingi, Mkurugenzi na/au mwalimu mkuu ambaye:

**a.** Ana angalau umri wa miaka 18, na ambaye ana cheti cha sasa cha huduma ya kwanza kwa watu wazima na watoto na ujuzi wa Ufufuzi wa Kumpulizia Mtu Mdomoni (CPR); na

**b.** Amekamilisha angalau saa 6 za mafundisho ya kwanza ya leseni katika mazingira salama na yenye; Ukuaji wa watoto; uchunguzi na tathmini; shughuli sahihi za ukuaji; ushauri; mahusiano ya kifamilia; utofauti wa watu binafsi na wa kitamaduni; Watoto wenye mahitaji maalum; maendeleo ya kibiashara na kitaaluma; na shughuli za utunzaji wa Watoto.

**4.** Vituo vilivyoidhinishwa kwa watoto 13 - 20 lazima vimwajiri angalau mkurugenzi au mwalimu mkuu mmoja. Mkurugenzi/Mwalimu mkuu anaweza kuwa mmiliki wa Kituo hiki cha Utunzaji wa Watoto. Mkurugenzi na/au mwalimu mkuu lazima awe na umri wa angalau miaka 21 na lazima atimize mojawapo ya masharti yafuatayo:

**a.** Kuhitimu kutoka shule ya upili iliyoidhinishwa au chuo kinacholingana nayo, na ajira ya miezi 12 katika Mpango wa Utunzaji wa Watoto ulioidhinishwa na saa 12 za mafundisho katika mazingira salama na yenye afya; Ukuaji wa watoto; uchunguzi na tathmini; shughuli sahihi za ukuaji; ushauri; mahusiano ya kifamilia; utofauti wa watu binafsi na wa kitamaduni; Watoto wenye mahitaji maalum; maendeleo ya kibiashara na kitaaluma, utunzaji wa Watoto, au Elimu ya Watoto; au

**b.** Saa 30 za muda vya kozi za chuo kikuu ikijumuisha saa sita za muda katika Elimu ya Watoto au masomo yanayohusiana kwa karibu, na uzoefu wa miezi sita (mazoezi ya kuajiriwa au ya chuo kikuu) katika Mpango wa Utunzaji wa Watoto ulioidhinishwa; au

**c.** Sifa za Mwanashahada wa Ukuaji wa Watoto (CDA) inayotolewa na Baraza la Tuzo za Kitaalamu, au sifa zilizoidhinishwa na Jimbo la Maine, na uzoefu wa moja kwa moja wa miezi sita wa utunzaji wa Watoto (ajira au mazoezi ya chuo kikuu).

**5.** Vituo vilivyoidhinishwa kwa ajili ya watoto 21 – 49 ni lazima viajiri Mkurugenzi na/au mwalimu mkuu ambaye ana umri wa angalau miaka 21, na anakidhi mojawapo ya masharti yafuatayo:

**a.** Shahada ya Kwanza ya Sanaa/Sayansi (AA/AS) katika Elimu ya Watoto; au

**b.** AA/AS ya vialamisho 12 katika Elimu ya Watoto au fani husika iliyoidhinishwa na Idara, na uzoefu wa moja kwa moja wa miaka miwili wa Utunzaji wa Watoto; au

**c.** Vialamisho 30 vya chuo kikuu katika Elimu ya Watoto, na mwaka mmoja wa uzoefu wa moja kwa moja wa utunzaji wa Watoto; au

**d.** Shahada ya Ukuaji wa Watoto (CDA) inayotolewa na Baraza la Tuzo za Kitaalamu, au sifa zilizoidhinishwa na Jimbo la Maine, na uzoefu wa moja kwa moja wa miaka mitatu wa utunzaji wa Watoto; au

**e.** Miaka mitano ya uzoefu wa moja kwa moja wa utunzaji wa Watoto, na saa 135 za mafundisho katika elimu ya watoto ikijumuisha mazingira yenye afya, salama na jumuishi; Ukuaji wa watoto; uchunguzi na tathmini; mazoezi sahihi ya maendeleo; mwongozo; mahusiano ya kifamilia; na utofauti wa kitamaduni.

**6.** Vituo vilivyoidhinishwa kwa ajili ya watoto 50 au zaidi ni lazima viajiri Mkurugenzi na/au mwalimu mkuu ambaye ana umri wa angalau miaka 21, na anakidhi mojawapo ya masharti yafuatayo:

**a.** Shahada ya Sayansi/Shahada ya Sanaa (BA/BS) katika Elimu ya Watoto; au

**b.** BA/BS katika fani husika na iliyoidhinishwa na Idara na saa 18 za muda vya Elimu ya Watoto na uzoefu wa moja kwa moja wa miaka mitatu wa utunzaji wa Watoto; au

**c.** Mwanashahada wa Sanaa/Sayansi (AA/AS) katika Elimu ya Watoto na miaka mitatu ya uzoefu wa moja kwa moja wa utunzaji wa Watoto; au

**d.** AA/AS katika fani husika na saa 18 za muda vya Elimu ya Watoto na uzoefu wa moja kwa moja wa miaka mitatu wa utunzaji wa Watoto; au

**e.** CDA ya sasa inayotolewa na Baraza la Tuzo za Kitaalamu, au sifa zilizoidhinishwa na Jimbo la Maine, na uzoefu wa moja kwa moja wa miaka mitano wa utunzaji wa Watoto;

**f.** Uzoefu wa miaka saba na saa 180 za mafundisho katika mada zilizoorodheshwa katika Sehemu ya 7(F)(4)(e) hapa juu; au

**g.** Kufikia Kiwango cha 5, 6, 7 au 8 cha mpango wa Maine Roads to Quality Career Lattice.

**7.** Mwalimu mkuu au mtu aliye na jukumu la msingi la kikundi cha Watoto katika mpango ulio na Watoto 13 au zaidi lazima awe na umri wa angalau miaka 18 na atimize mojawapo ya masharti yafuatayo:

**a.** CDA ya sasa inayotolewa na Baraza la Tuzo za Kitaalamu, au sifa zilizoidhinishwa na Jimbo la Maine; au

**b.** Miezi 12 ya uzoefu wa moja kwa moja wa utunzaji wa Watoto; au

**c.** Mwaka mmoja (saa 30 za muda) za elimu ya chuo ikijumuisha kozi moja ya somo linalohusiana na Watoto na uzoefu wa miezi sita.

**8.** Wakurugenzi na/au walimu wakuu wa Vituo vya Utunzaji wa Watoto wenye umri wa kwenda shule lazima wawe na AA/AS katika Elimu ya Watoto au vialamisho 30 vya chuo kikuu katika fani husika kama vile elimu ya msingi, Ukuaji wa watoto au usimamizi wa burudani.

## SEHEMU YA 8. MAFUNDISHO

**A.** **Wajibu wa Taasisi ya Utunzaji wa Watoto**. Kituo cha Utunzaji wa Watoto kina jukumu la kuhakikisha kwamba Wahudumu wote wa Watoto wanafahamu utendakazi wa kituo cha utunzaji wa Watoto na wanaelewa mahitaji muhimu ya kanuni hii.

**1.** Wahudumu wote wa Watoto lazima wapate mafundisho ya kutoroka moto na taratibu zingine za dharura na maafa ndani ya wiki ya kwanza ya huduma.

**B.** **Mafundisho ya utangulizi.** Wahudumu wote wa Watoto lazima wapate mafundisho katika fani zifuatazo ndani ya siku tisini za kwanza za huduma:

**1.** 10-148 CMR Ch. 32, Kanuni ya Kutoa Leseni kwa Taasisi za Utunzaji wa Watoto - Vituo vya Utunzaji wa Watoto, Shule za Chekechea, Taasisi Ndogo za Utunzaji wa Watoto

**2.** Sera na taratibu za mpango;

**3.** Kuzuia Ugonjwa wa Kifo cha Ghafla cha Watoto (SIDS) au Kifo cha Ghafla Kisichoeleweka (SUID), Ugonjwa wa Kumtikisa Mtoto, na maadili ya kulala salama;

**4.** Utoaji Dawa na idhini ya wazazi (Wahudumu wa Watoto hawawezi kusimamia utoaji wa Dawa hadi wapewe mafundisho);

**5.** Kuzuia na kukabiliana na hali za dharura za chakula na mzio;

**6.** Usalama wa majengo na nyumba;

**7.** Kuzuia na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya kusambaa; Tahadhari za Usalama wa Jumla na Viini vya Magonjwa Yanayoenezwa kwa Damu;

**8.** Utunzaji na uhifadhi wa nyenzo Hatari na taratibu za kutupa vichafuzi vya Kibayolojia;

**9.** Usafirishaji wa Watoto (ikiwa mtu husika atawajibikia usafirishaji wa Watoto; inahitajika mara mbili kila mwaka baada ya hapo);

**10.** Msaada wa kwanza kwa watu wazima na watoto pamoja na maonyesho ya ujuzi;

**11.** Ufufuzi wa Kumpulizia Mtu Mdomoni (CPR) kwa watu wazima na watoto kwa maonyesho ya ujuzi;

**12.** Mafundisho ya wawasilishaji ripoti walioidhinishwa na Idara;

**13.** Kwa mipango inayohudumia Watoto 13 au zaidi, mafundisho ya mpango wa huduma ya afya ya mpango uliotayarishwa na Mshauri wa Huduma ya Afya wa mpango huo.

**C.** **Mafundisho Yanayoendelea.** Vituo vyote vya Huduma ya Watoto lazima vihakikishe idadi inayofaa ya saa za mafundisho yanayoendelea kwa Wahudumu wa Watoto.

**1.** Wahudumu wote wa Watoto lazima wajisajili kwenye Mtandao wa Maendeleo ya Kitaalam wa Maine.

**a.** Mafundisho ya kila mwaka lazima yajumuishe ukaguzi wa mada za afya na usalama zinazotolewa na Mtandao wa Maendeleo ya Kitaalamu wa Maine ulioidhinishwa na jimbo.

**b.** Mafundisho yanayoendelea lazima yajumuishe mafundisho mapya ya wawasilishaji ripoti walioidhinishwa na Idara angalau mara moja kila baada ya miaka minne, kwa mujibu wa 22 MRS §4011-A(9).

**2.** Idadi ya kila mwaka ya saa za mafundisho zinazohitajika hutegemea ukubwa wa mradi na idadi ya saa ambazo Mhudumu wa Watoto hufanya kazi kwa wiki, kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

| Ukubwa wa Mpango | Zaidi ya Saa 20 | Chini ya Saa 20 |
|---|---|---|
| Chini ya Watoto 13 | 12 | |
| Zaidi ya Watoto 13 | 30 | 18 |

**a.** Mafundisho yote, ikijumuisha Msaada wa Kwanza kwa Watu Wazima na Watoto na saa za cheti cha CPR, yatahesabiwa kulingana na mahitaji ya mwaka ambao yalikamilishwa.

**b.** Hesabu ya saa za mafundisho kwa mwaka lazima ilingane na tarehe ya kutolewa kwa leseni ya Vituo vya Utunzaji wa Watoto.

**c.** Mafundisho yanayohitajika kwa Wahudumu wapya wa Watoto yatagawanywa kulingana na miezi ya ajira.

**d.** Ili kuhesabika katika idadi inayohitajika ya saa za mafundisho kwa kila mwaka, ni lazima mafundisho yalingane na utafiti wa sasa wa maadili bora yanayohusiana na ujuzi unaohitajika ili wahudumu wa Watoto waweze kutimiza masharti ya Watoto na yalingane na idadi ya Watoto wanaohudumiwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto. Mada za mafundisho zinajumuisha, lakini si tu, mazingira salama na yenye; Ukuaji wa watoto; uchunguzi na tathmini; shughuli sahihi za ukuaji; ushauri; mahusiano ya kifamilia; utofauti wa watu binafsi na wa kitamaduni; Watoto wenye mahitaji maalum; maendeleo ya kibiashara na kitaaluma; au shughuli za utunzaji wa Watoto.

**D.** **Kunukuu mafundisho**. Mpango huu lazima unukuu mafundisho yote ya utangulizi na yanayoendelea ya wahudumu wote kwa uthibitisho wa kukamilishwa kwa mipango hii kutoka kwa mtu aliyehitimu, kupitia mbinu ya mtandaoni au ya mtu kibinafsi.

## SEHEMU YA 9. KUWASHAURI WATOTO

**A.** **Mbinu chanya za kuwashauri Watoto.** Wahudumu wote wa Watoto lazima watumie mbinu chanya za kuwashauri Watoto zinazohimiza kujidhibiti, kujiongoza, kujistahi, kuwasiliana kuhusu mahitaji na matakwa na kushirikiana na wengine. Ushauri kwa mtoto unapaswa kukidhi mahitaji ya kibinafsi ya kila Mtoto.

**B.** **Utekelezaji thabiti na unaofaa wa kanuni za mpango.** Kanuni, matarajio na mipaka lazima itumike kwa uwazi na uthabiti na itekelezwe kwa njia inayoakisi uwezo wa ukuaji wa Mtoto.

**C.** **Mbinu bora za ushauri.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitumie mbinu bora za ushauri tu. Hii inaweza kujumuisha, lakini si tu, hatua kama vile:

**1.** Utatuzi wa migogoro,

**2.** Kuhimiza matumizi ya ujuzi wa lugha,

**3.** Kuelekeza kwingine,

**4.** Kutoa chaguo,

**5.** Kumsifu mtoto au kumhimiza,

**6.** Kutambua uwezo wa Mtoto,

**7.** Kuruhusu Watoto kwenda mapumziko yaliyosimamiwa na mtu mzima mbali na kikundi inapohitajika,

**8.** Kuwakumbusha Watoto matarajio kwa kutumia lugha chanya na wazi,

**9.** Kufundisha kujidhibiti,

**10.** Kuiga tabia njema, na

**11.** Kuruhusu tofauti za watu binafsi.

**D.** **Vitendo vibaya.** Vitendo ambavyo vinaweza kuwadhuru Watoto vimepigwa marufuku kabisa. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihakikishe kwamba hakuna Mtoto anayetendewa jambo linaloathiri ustawi wake, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu:

**1.** Adhabu ya kimwili. Adhabu ya kimwili ni vitendo vya kimwili vinavyoathiri mwili wa Mtoto, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, yafuatayo:

**a.** Kumpiga kofi, kumgonga, kumtikisika, kumsukuma na, kumchapa, kumchuna, kumsokota, kumpiga mateke, kumuuma, kumvuta sikio au kumchuna sikio;

**b.** Kumlazimisha Mtoto kuonja au kula vitu vikali, vichungu au vya kuchukiza kama njia ya Nidhamu;

**c.** Kunyunyizia maji kama njia ya kudhibiti tabia yake;

**d.** Kumfunga Mtoto kwa utepe mdomoni;

**e.** Vizuizi vya kimwili, kama vile kumfungia Mtoto kwenye kiti;

**f**. Kumwagiza au kumlazimisha Mtoto kufanya mkao mgumu kama vile: kuchuchumaa, kupiga magoti, kusimama na kushika mikono akiinyoosha kando au juu, kuinama, au kumwagiza au kumlazimisha Mtoto kurudia mwendo wa kimwili; au

**2.** Aina zingine za vitendo vya kikatili ambayo ni hatari kwa mwili wa Mtoto. Adhabu kali au ya kikatili, fedheha au matusi, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu:

**a.** Kumwaibisha na kumdhalilisha; au

**b.** Kumwadhibu kwa kujichafua, kujikojolea au kutotumia choo;

**c.** Kumdhalilisha au kumtusi Mtoto kwa njia nyingine yoyote.

**3.** Kumnyima chakula, vinywaji, mapumziko au muda wa kucheza nje kama adhabu au tishio la adhabu, au kumlazimisha kula au kunywa kinyume na mapenzi ya Mtoto;

**4.** Kumweka Mtoto kwenye mazingira ya lugha chafu, maonyesho ya vurugu, matumizi ya dawa za kulevya au maudhui ya ngono;

**5.** Kumwagiza Mtoto kunyamaza au kutofanya chochote kama hatua ya kinidhamu kwa muda unaozidi umri wa Mtoto huyo kwa kipimo cha dakika;

**6.** Kumfungia mtoto kwa njia isiyo ya kawaida, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, matumizi yasiyofaa ya viti virefu sana kwa umri wa mtoto, vitanda vya michezo au vya kulala visivyofaa, au kumwacha Mtoto bila utunzaji katika chumba chochote;

**7.** Kuondoa kifaa chochote saidizi ambacho kinaweza kumsababisha Mtoto kupoteza uhuru wake;

**8.** Kutumia vizuizi vya kimwili, isipokuwa kama mhudumu amefunzwa, na baada ya ukaguzi na idhini ya daktari aliyeidhinishwa kwa Leseni;

**9.** Ukosefu wa usimamizi;

**10.** Matamshi ya dharau kwa au kuwahusu Watoto au wazazi; au

**11.** Kumtendea ukatili.

## SEHEMU YA 10. HAKI ZA WATOTO NA WAZAZI

**A. Haki za Watoto.** Watoto wanaopokea utunzaji kutoka Vituo vya Utunzaji wa Watoto wana haki zifuatazo.

**1.** Watoto lazima wawe huru kutokana na unyanyasaji wa kihisia, kimwili na/au kingono, kutelekezwa na kutumiwa vibaya.

**2.** Kila Mtoto ana haki ya kuwa huru kutokana na vitendo au shughuli mbaya zinazoathiri ustawi wake, na matendo ambayo yanaweza kuwa hatari kwa Mtoto.

**3.** Kila Mtoto ana haki ya kuwa katika mazingira ambayo yanakidhi viwango vya afya na usalama katika kanuni hii.

**4.** Kila Mtoto lazima apewe huduma za utunzaji bila ubaguzi wa rangi, umri, asili ya kitaifa, dini, ulemavu, jinsia au muundo wa familia.

**5.** Watoto lazima wahudumiwe kwa utu, uzingativu na heshima huku ikitambuliwa kikamilifu kuwa wao ni watu binafsi na tofauti. Hii ni pamoja na Kituo cha Utunzaji wa Watoto kutumia mbinu mwafaka kiukuaji.

**6.** Kila Mtoto ana haki ya kutekelezewa mpango wowote wa huduma ambao umeandaliwa kwa ajili ya Mtoto huyo kwa kushirikiana na mashirika ya jamii au ya serikali na Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**7.** Kila Mtoto ana haki ya kupokea shughuli, nyenzo na vifaa vinavyomfaa Kiukuaji.

**8.** Watoto wenye ulemavu wana haki ya kufanyiwa marekebisho yanayofaa kwenye sera na desturi za Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**B. Haki za wazazi na walezi wa kisheria wa Watoto wanaopokea utunzaji kutoka kwa Taasisi za Utunzaji wa Watoto.**

**1.** Mzazi wa Mtoto au Mlezi wa Kisheria lazima apate taarifa kamili kuhusu bidhaa au huduma ambazo zimejumuishwa kwa kiwango wanacholipia huduma za utunzaji ya Mtoto.

**2.** Mzazi wa Mtoto au Mlezi wa Kisheria ana haki ya kufahamishwa kikamilifu kuhusu matokeo ya ukaguzi wa hivi majuzi uliofanywa na Idara. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwafahamishe Wazazi wa Watoto au Walezi wa Kisheria kwamba matokeo ya ukaguzi wa leseni ni taarifa za umma na matokeo ya ukaguzi lazima yabandikwe katika sehemu wazi kwenye Majengo.

**3.** Wazazi au Walezi wa Kisheria lazima wajulishwe na Kituo cha Utunzaji wa Watoto ndani ya siku mbili za kazi kuhusu hatua zozote zilizochukuliwa na Idara dhidi ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, maamuzi ya kupewa Leseni zenye masharti, kutopewa Leseni upya, au kutozwa faini au vikwazo vingine.

## SEHEMU YA 11. KURIPOTI KUHUSU KUNYANYASWA NA KUTELEKEZWA KWA WATOTO

**A.** **Masharti ya kuripoti kuhusu Kunyanyaswa na kutelekezwa kwa Watoto.** Wahudumu wote wa Watoto lazima wawasiliane papo hapo na kitengo cha Usajili wa Kinga za Watoto cha Idara ya Afya na Huduma ya Kibinadamu kupitia simu ya dharura (800-452-1999) wanaposhuku kuwa Mtoto ananyanyaswa au kutelekezwa.

**B.** **Masharti ya Taasisi ya Utunzaji wa Watoto ya kutoa taarifa.** Mkurugenzi lazima awajulishe Wahudumu wote wa Watoto wakati wa mafundisho ya utangulizi kuhusu hali yao kama Wawasilishaji Ripoti Wanaowajibika, na wajibu wao wa kutuma ripoti kwa Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu wakati wowote ambapo kuna sababu za msingi za kushuku kuwa Mtoto ananyanyaswa au kutelekezwa, na kutii mafundisho yanayoendelea ya Mwasilishaji Ripoti Aliyeidhinishwa, kwa Wahudumu wote wa Watoto kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya 8 ya Kanuni hii.

**C.** **Maagizo yaliyoandikwa ambayo yamewasilishwa.** Wahudumu wa Watoto lazima wapokee maagizo yaliyoandikwa kuhusu ripoti ya Kunyanyaswa au Kutelekezwa kwa Mtoto ambayo ina muhtasari wa sheria ya Jimbo la Maine ya kuripoti unyanyasaji wa Mtoto na taarifa inayothibitisha kuwa hawatafutwa kazi au kuadhibiwa kwa sababu tu wametoa ripoti ya Kunyanyaswa au Kutelekezwa kwa Mtoto.

**D.** **Nambari ya dharura iliyochapishwa.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihakikishe kwamba nambari ya simu ya Idara ya Usajili wa Ulinzi wa Watoto imebandikwa katika eneo kuu linaloweza kufikiwa kwa urahisi kwenye Majengo.

## SEHEMU YA 12. AFYA NA MATIBABU

**A.** **Chanjo.** Rekodi za chanjo lazima zihifadhiwe ili kuhakikisha kuwa matibabu sahihi yanabainishwa na kutolewa iwapo kuna mzuko wa ugonjwa au jambo la dharura la afya ya umma.

**1.** Watoto wote wanaotunzwa sharti wakidhi mahitaji yafuatayo:

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na rekodi ya sasa ya chanjo iliyohifadhiwa kwa kila Mtoto, ambayo inanukuu kwa uwazi hali ya sasa ya chanjo ya kila Mtoto kulingana na Viwango vya Vituo vya Utunzaji wa Mchana vya Idara (inayopatikana katika https://www.maine.gov/dhhs/mecdc/infectious disease/immunization/documents/Childcare%20Immunization%20Standards.pdf na iliyochapishwa tarehe 8 Agosti, 2021), ndani ya siku 30 baada ya Mtoto kusajiliwa kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa mara ya kwanza, na kusasishwa kama itakavyohitajika baadaye, au

**b.** Kipimo cha damu kinachothibitisha kingamwili dhidi ya surua, matumbwitumbwi, rubela na varisela (tetekuwanga), kilichowekwa kwenye rekodi ya Mtoto na kusasishwa kwa wakati ufaao.

**c.** Kwa mujibu wa P.L. 2019, Ch. 154, § 11, kuanzia tarehe 1 Septemba, 2021, ni lazima Watoto wapewe chanjo kama ilivyobainishwa hapa na mtoto anapaswa tu kutopokea chanjo ikiwa kuna sababu za kimatibabu pekee. Daktari wa Mtoto, muuguzi au msaidizi wa daktari lazima atoe hati inayothibitisha kwamba inashauriwa chanjo isitolewe kwa sababu za kiafya.

**2.** Wahudumu wa Watoto na Watoto Wasiochanjwa. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihifadhi orodha ya watu wote ambao hawajachanjwa, licha ya umri wao. Ikiwa ugonjwa utazuka kama inavyofafanuliwa na viwango vya kuripoti vya CDC, Mtoto ambaye hajachanjwa lazima asijumuishwe kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa mujibu wa mwongozo wa CDC au hadi Mtoto apate chanjo inayohitajika au uthibitisho wa kinga uwe kwenye rekodi.

**3.** Rekodi za chanjo. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwasilishe rekodi za chanjo kwa Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu, Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa cha Maine, baada ya kuombwa kufanya hivyo.

**4**. Rekodi za chanjo dhidi ya pepopunda, kifaduro na dondakoo zinahitajika kwa Wahudumu wote wa Watoto.

**a.** Kwa Wahudumu wa Watoto waliozaliwa baada ya 1956, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kichukue na kuhifadhi Cheti cha Chanjo dhidi ya surua, matumbwitumbwi, rubela, pepopunda na dondakoo.

**b.** Rekodi za chanjo dhidi ya surua, matumbwitumbwi na rubela hazihitajiki kwa Wahudumu wa Watoto waliozaliwa kabla ya 1957. Vipimo vya damu vya maabarani vinavyothibitisha chanjo pia vinaweza kukubaliwa.

**c.** Hati zilizoandikwa na daktari pekee zikisema kwamba chanjo hiyo haifai kiafya zinampa Mhudumu wa Watoto ondoleo la kutii Kifungu cha 12(A)(4)(a) na (b).

**B.** **Masharti ya tathmini.** Idara ikiwa na sababu za kuridhisha za kuamini kwamba Mwombaji au Mhudumu wa Watoto hawezi kutoa huduma salama ya utunzaji wa Watoto, Idara inaweza kuomba ripoti kutoka kwa mtaalamu aliyehitimu au afisa anayefaa, ambayo inajumuisha uamuzi wa mtathmini wa uwezo wa mtu huyo kutunza Watoto kwa usalama.

**1.** Uchunguzi wa kimwili au tathmini nyingine haihitajiki ikiwa Mwombaji au Mhudumu wa Watoto atakiri kwa maandishi kwamba ni kinyume na mafundisho na maadili yake ya kidini.

**2.** Ikiwa Mwombaji au Mhudumu wa Watoto anakataa kutathminiwa, Idara itaamua kama kuna ushahidi wa kutosha kubaini kama mtu huyo anaweza kutunza Watoto kwa usalama.

**C. Ushauri wa huduma za afya.**

**1.** Kwa Vituo vya Utunzaji wa Watoto vilivyoidhinishwa kwa Watoto 3 hadi 12:

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na miongozo iliyoandikwa ya kuzuia na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na mbinu zingine za afya zinazofaa kwa Vituo vya Utunzaji wa Watoto vya ukubwa huu.

**b.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihakikishe kuwa mwongozo huo unapatikana na kusomwa na Wahudumu wote wa Watoto

**2.** Kwa Vituo vya Utunzaji wa Watoto vilivyoidhinishwa kwa Watoto 13 au zaidi:

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na mkataba ulioandikwa baina yake na daktari, msaidizi wa daktari, muuguzi anayehudumu au muuguzi aliyesajiliwa mwenye uzoefu wa kutibu au kuwahudumia Watoto ili kutumika kama mshauri wa afya. Mkataba huu lazima usasishwe wakati wa kutoa upya leseni.

**b.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na mpango ulioidhinishwa na mshauri wa afya ambao lazima ujumuishe:

**i.** Mpango wa kufikia huduma za matibabu ya dharura;

**ii.** Kuzuia na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza;

**iii.** Sera ya utoaji dawa inayojumuisha utambulisho wa Wahudumu wa Watoto wanaoruhusiwa kutoa dawa na taratibu za kurekodi za utoaji au usambazaji wa dawa; na

**iv.** Utoaji mafundisho kwa Wahudumu wote wa Watoto walio katika mpango wa huduma ya afya wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**D. Ufuatiliaji wa afya.** Wahudumu wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima wamfuatilie Mtoto kila siku anapowasili na wakati wote wa kukaa kwa Mtoto ili kubaini dalili bayana za ugonjwa kama vile homa, kuendesha, kutapika au vipele vya ngozi.

**1.** Mtoto akiwa na ugonjwa unaobainika dhahiri, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kifuate taratibu za kiafya zinazofaa.

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kilichoidhinishwa kuwahudumia Watoto 3 hadi 12 lazima kifuate mwongozo ulio katika kijitabu kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya 12(C)(1)(a) hapa juu.

**b.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kilichoidhinishwa kuwahudumia Watoto 13 au zaidi lazima kifuate kauli yake ya sera ya afya iliyoandikwa.

**2.** Wahudumu wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto wanapotambua au kushuku kuwa Mtoto ameambukizwa ugonjwa au hali inayopaswa kuripotiwa, wahudumu wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiarifu Kituo cha Maine cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (MECDC).

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiarifu MECDC papo hapo kwa njia ya simu kwa hali za Aina ya 1, na ndani ya saa 48 hali za Aina ya 2. Mbinu za Mawasiliano za MECDC: Simu: 1-800-821-5821 (saa 24 kwa siku); FAKSI: 1-800-293-7534 (saa 24 kwa siku); au TTY: Huduma ya simu ya Maine kwa watu wenye matatizo ya kusikia ya 711 (saa 24 kwa siku).

**b.** Ili upate orodha ya hali zinazopaswa kuripotiwa za Aina ya 1 na 2, rejelea 10-144 CMR Sura ya 258, Kanuni za Udhibiti wa Hali Zinazopaswa Kuripotiwa, Sura ya 2(I). http://www.maine.gov/sos/cec/rules/10/144/144c258.doc

**E.** **Kuwatuma Watoto Nyumbani wanapougua.** Mtoto anapougua, lakini hahitaji usaidizi wa dharura wa kimatibabu, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kibaini kama Mtoto huyu anapaswa kurudishwa nyumbani. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiarifu mzazi/mlezi wa Mtoto ambaye ana dalili zinazomhitaji kutengwa.

**F.** **Ugonjwa, majeraha makubwa, matukio na ajali.**

**1.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiarifu mzazi au mlezi wa kisheria wa Mtoto papo hapo kuhusu ugonjwa wowote, jeraha baya au tukio lolote linalomhusisha Mtoto wao. Mtu mzima aliyeteuliwa na mzazi au mlezi wa kisheria lazima aarifiwe papo hapo iwapo mzazi au mlezi wa kisheria hapatikani.

**2.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kirekodi ajali, majeraha, matukio au hali zote za dharura katika rekodi ya Mtoto siku ya tukio, na mzazi au mlezi wa kisheria lazima akague na kuweka sahihi hati ndani ya siku mbili za kazi.

**G.** **Huduma ya kwanza**. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na kifaa cha huduma ya kwanza na mwongozo wa sasa wa huduma ya kwanza.

**1.** Kisanduku kamili cha huduma ya kwanza lazima kipatikane kwa urahisi katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinawachohudumia Watoto 3 hadi 12, katika ziara zote za nyanjani, na wakati wa kuwasafirisha Watoto.

**2.** Miradi inayowahudumia Watoto 13 au zaidi lazima iwe na mwongozo na vifaa tofauti vya huduma ya kwanza katika kila darasa.

**3.** Kisanduku cha huduma ya kwanza lazima kiwe safi kila wakati, kihifadhiwe katika sehemu maalum inayofikika kwa urahisi, inayojulikana na Wahudumu wa Watoto na kiwekwe mbali na Watoto.

**4.** Kisanduku kamili cha huduma ya kwanza kinajumuisha, lakini si tu, mkanda wa kunata, bendeji ya kunata, pedi za shashi, bendeji ya shashi, glavu zinazoweza kutupwa, pakiti ya nyenzo ya kugandisha ya papo hapo, makasi, vibano, kipimajoto na vipangusio vyenye dawa ya kuua viini.

**5.** Kisanduku cha huduma ya kwanza lazima kisiwe na vifaa vilivyokwisha matumizi.

**H.** **Kutoa dawa.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaweza kumpa Mtoto dawa iliyoagizwa na daktari tu ikiwa kimepokea idhini ambayo Mzazi ameandika, kuweka saini na tarehe.

**1.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kipeane tu dawa iliyoagiziwa Mtoto mahsusi, kulingana na maagizo ya lebo yaliyo kwenye chombo asili.

**2.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakipaswi kumpa Mtoto dawa zozote zisizoagizwa na daktari bila ruhusa iliyoandikwa na mzazi. Ruhusa kupitia simu, ujumbe wa SMS au barua pepe inaruhusiwa katika

hali za dharura, ikiwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitanukuu hati inayothibitisha kutoa dawa na kupata ruhusa iliyoandikwa na mzazi haraka iwezekanavyo.

**3.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiweke rekodi iliyoandikwa, kikibainisha kila wakati Mtoto alipewa dawa ambayo haijaagizwa na daktari.

**4.** Dawa zote, zilizowekwa kwenye jokofu au la, lazima:

**a.** Zisiweze kufikiwa na Watoto hata kidogo,

**b.** Zihifadhiwe katika halijoto inayofaa, na

**c.** Zitupwe baada ya muda wake kuisha.

**5.** Matumizi ya bangi ya kimatibabu katika Vituo vya Utunzaji Watoto yanadhibitiwa na sheria ya 18-691 CMR Sura ya 2, Kanuni ya Maine ya Mpango wa Matumizi ya Bangi ya Kimatibabu.

**I.** **Kunawa Mikono.** Watu lazima wanawe mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihakikishe kwamba watu wazima na Watoto wote wananawa mikono angalau katika hali zifuatazo:

**1.** Mara moja kabla na baada ya kula vitafunio na milo, ikiwa ni pamoja na kuwanawisha mikono watoto wote wachanga na wakubwa kabla ya milo yote;

**2.** Kila baada ya kubadilisha nepi au kwenda haja;

**3.** Kabla na baada ya kuandaa chakula; na

**4.** Kabla na baada ya kupewadawa.

**J.** **Kuzuia kuhatarishwa na damu na viowevu vya mwili**. Wahudumu wa Watoto lazima wachukue hatua ili kuzuia uhatarisho unaoweza kusababishwa na damu na viowevu vingine vinavyoweza kuambukiza, hatua ambazo zinaweza kujumuisha matumizi ya glavu zinazoweza kutupwa. Wanapohitajika kugusa damu, viowevu vya mwili, ute, uchafu wa mwili, utando au ngozi iliyochibuka, Wahudumu lazima:

**1.** Wanawe mikono yao baada ya kugusa vitu hivi, hata ikiwa wamevaa glavu;

**2.** Wahakikishe wanadhibiti taka kwa njia salama kwa kutupa mara moja vitu vinavyopaswa kutumiwa mara moja ambavyo vimechafuka; na

**3.** Kusafisha na kupaka viua viiini kwenye sehemu na vifaa vinavyotumika tena.

**K.** **Taratibu za hali ya dharura.** Vituo lazima viwe na utaratibu wa kukabiliana na hali za dharura ya kimatibabu. Uwiano wa Wahudumu na Watoto lazima udumishwe, na Wahudumu wa Watoto wataitwa ili kudumisha uwiano unaohitajika. Wahudumu wote wa Watoto wanapaswa kupewa mafundisho ya kudhibiti hali ya dharura hadi madaktari wa dharura wafike.

## SEHEMU YA 13. MAJI SAFI NA MAJI TAKA

**A.** **Maji safi.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitoe hati za usalama wa maji safi yanayotumiwa na Watoto na Wahudumu wa Watoto walio kituoni. Ikiwa hakuna maji ya kutosha, huenda kituo kisiweze kupewa leseni ya kwanza au inayotolewa upya.

**1.** Vituo vinavyotoa maji ya kunywa kutoka kisima chao lazima vithibitishe vina maji ya ubora wa kuridhisha kwa kupima vichafuzi vifuatavyo kwenye maabara iliyoidhinishwa na jimbo la Maine:

**a.** Floridi,

**b.** Urani,

**c.** Arseniki,

**d.** Sampuli ya kwanza ya madini ya risasi,

**e.** Naitreti, na

**f.** Jumla ya bakteria ya kolifomu.

**2.** Vituo vinavyotoa maji kwenye kisima cha maji ya manispaa lazima vithibitishe vina maji ya ubora wa kuridhisha kwa kuchukua na kupima sampuli moja ya mkusanyiko wa kwanza kabla ya kupokea leseni. Chombo cha sampuli lazima kiwe kimetolewa na maabara iliyoidhinishwa na jimbo la Maine na kiwe na uwezo wa lita moja.

**B.** **Vipimo vya maji vinavyoendelea vya kila mwaka kwa Taasisi za Utunzaji wa Watoto zenye visima.** Vituo vinavyotoa maji kwenye kisima chao lazima viyapime maji yao kila mwaka kubaini kama kuna bakteria ya kolifomu na naitreti. Sampuli lazima zichambuliwe na matokeo yaliripotiwe na maabara iliyoidhinishwa na jimbo la Maine. Vituo lazima vihifadhi ripoti za ubora wa maji kwa ukaguzi wa Idara.

**C.** **Vipimo vya maji vya miaka mitano kwa taasisi zenye visima.** Pamoja na vipimo vya kila mwaka vinavyohitajika kwa mujibu wa Kifungu cha 13(B) hapa juu, vituo vinavyotoa maji kwenye visima vyake lazima vipime maji yake kila baada ya miaka mitano kubaini angalau vichafuzi vifuatavyo: floridi, urani, sampuli ya madini ya risasi ya mkusanyiko wa kwanza na arseniki.

**D.** **Mikataba ya maji ya chupa.** Iwapo kituo kitachagua kutumia na kutoa maji ya chupa kwa sababu ya kuwepo kwa kichafuzi kimoja au vingi vilivyoorodheshwa katika Sehemu ya 13(A)(1)(a-e) hapa juu, basi Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaweza kuendeshwa chini ya mkataba wa maji ya chupa baina yake na Idara. Chini ya mkataba huu, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima:

**1.** Kitumie maji ya chupa kwa matumizi yote na maandalizi ya chakula;

**2.** Kuwatumia taarifa iliyoandikwa wazazi wa Watoto walioandikishwa na wanaotarajiwa kusajiliwa kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto ambapo mtoto anatarajiwa kutumia maji ya chupa kwa matumizi yote na maandalizi ya chakula;

**3.** Kubandika mkataba mahali ambapo unaweza kuonekana kwa urahisi na wazazi; na

**4.** Kuendelea kupima maji kila mwaka kwa mujibu wa Kifungu cha 13(B) cha kanuni hii.

**E.** **Mifumo ya maji isiyo ya muda mfupi, isiyo ya jamii.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinachotoa maji ya kunywa kwenye kisima na kuwapa Wahudumu na Watoto 25 au zaidi ni lazima kitii sheria ya 10-144 CMR Sura ya 231, Kanuni Zinazohusiana na Maji ya Kunywa, zilizorekebishwa mara ya mwisho tarehe 9 Mei 2016.

**F.** **Maji safi na maji taka.** Katika saa zote za kazi, usambazaji wa maji na utupaji wa maji taka lazima ufikie viwango vya Idara ya Afya na Huduma za Binadamu, Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa cha Maine, Kitengo cha Afya ya Mazingira na Jamii ili kukidhi uwezo ulioidhinishwa wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**1.** Ikiwa mfumo wa utupaji maji taka haufanyi kazi ipasavyo, Kituo cha Huduma ya Mtoto lazima kifungwe.

**2.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaweza kuanza tena kufanya kazi wakati mfumo wa utupaji maji taka utaanza kufanya kazi ipasavyo.

## SEHEMU YA 14. MAZINGIRA NA USALAMA

**A. Hali ya jumla ya jengo na majengo yaliyo karibu**. Kituo lazima kichukue hatua za haraka kurekebisha hali yoyote katika jengo halisi au kwenye kituo, ambayo inahatarisha maisha, afya au usalama wa Watoto.

**1.** Ngazi zinazotumiwa na Watoto lazima ziwe na vizuizi imara vya kushika.

**2.** Ngazi lazima ziwe zimezungukwa na kuta au vizuizi. Ngazi zilizo katika maeneo zinazotumiwa na watoto wachanga, watoto wadogo na watoto wa umri wa shule ya chekechea lazima zikingwe kwa lango au mlango.

**3.** Vifaa vya umeme katika maeneo yanayotumiwa na watoto wachanga, watoto wadogo na Watoto wa shule ya chekechea lazima vikingwe kwa vifuniko vya usalama, plagi, vifaa vinavyostahimili uharibifu au njia nyinginezo.

**4.** Dawa Zozote, Nyenzo Zenye Sumu, Nyenzo Hatari na vitu vingine hatari kwa Watoto kama vile viberiti, tishari, fataki na vifaa vya umeme lazima viwekwe mahali ambapo Watoto hawawezi kuvifikia.

**5.** Uvutaji sigara ni marufuku kwenye majengo wakati Watoto wapo kituoni.

**6.** Kamba na nyuzi zenye urefu wa kutosha kuzunguka shingo ya Mtoto (inchi sita au zaidi) hazipaswi kuwekwa mahali zinapoweza kufikiwa na Watoto isipokuwa kama Mtoto anashiriki katika shughuli ya burudani au elimu akisimamiwa na mtu mzima.

**7.** Vifaa vilivyo na kamba ya umeme lazima vipachikwe ukutani ili kuzuia kuanguka, au kamba lazima isiweze kufikiwa na Watoto wa umri wa chini ya miaka mitano.

**8.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na simu inayofanya.

**9.** Kituo kinaweza kufunga lango kuu ili kuzuia watu kuingia kutoka nje, mradi tu mlango unaweza kufunguliwa kwa njia huru kutoka ndani, na kuna mbinu ya kuwajulisha Wahudumu wa Watoto kuhusu wazazi/walezi au wageni wengine wanaowasili.

**10.** Vitu na vifaa vya kuchezea lazima daima viwe safi na katika hali salama na viwe vinafanya kazi.

**11.** Eneo la kuangukia na linalovizunguka vifaa vyote vya kuchezea ndani ya majengo ambalo linaweza kudhibiti kuanguka kutoka urefu wa zaidi ya inchi 29 lazima lifunikwe kwa mikeka au nyenzo za kupunguza mwanguko ambazo zinaenea angalau inchi 39 zaidi ya ukingo wa nje wa kifaa kwenda pande zote. Ikiwa muundo wa kuchezea unazidi inchi 48 kwa urefu, mkeka wa kupunguza mwanguko lazima uwe na unene wa angalau inchi mbili.

**12.** Samani, vitu vingine vizito, na/au vitu ambavyo vinaweza kuanguka kwa urahisi au visivyo thabiti lazima vihifadhiwe ukutani au sakafuni.

**13.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima Kisafishe sehemu za juu kila siku katika maeneo yote walipo Watoto. Bidhaa za kusafisha hazipaswi kutumiwa karibu na Watoto na mzunguko wa hewa wa kutosha lazima udumishwe wakati zinatumiwa.

**14.** Watoto hawaruhusiwi kuwa karibu na vifaa vya umeme vinapoendeshwa, na ni lazima vifaa vya umeme vihifadhiwe mahali wasipoweza kufikia au viwe na ulinzi ili kuzuia Mtoto yeyote asijeruhiwe wakati havitumiwi.

**15.** Mikoba ya Wahudumu, mifuko, Dawa na vitu vingine lazima viwekwe mbali na Watoto.

**16.** Njia zote za kuingia na kutoka lazima ziwe wazi ili kuwezesha uokoaji wakati wote.

**17.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima vimwage takataka kwenye mapipa, vifaa vya kuchakata upya na vyombo vya mbolea na viondoe vitu kwenye nafasi ya utunzaji wa Watoto wakati vifaa hivi vinajazwa, au mapema zaidi ikiwa uchafu uliomo unasababisha harufu mbaya au ni hatari ya kiafya.

**B.** **Wakati wa kucheza nje na kupumzika unahitajika.** Watoto lazima wawe na fursa za kufanya shughuli za ndani na nje.

**1.** Watoto wanaohudhuria shughuli kwa saa zisizozidi nne lazima wapate fursa ya kupumzika au kutulia kwa angalau dakika 10 kulingana na mahitaji ya Mtoto.

**2.** Watoto wanaohudhuria shughuli kwa zaidi ya saa nne lazima wapate fursa ya kupumzika au kutulia kwa saa moja au zaidi kulingana na umri na mahitaji ya Mtoto.

**3.** Watoto wanaohudhuria shughuli kwa zaidi ya saa nne, na wenye umri wa zaidi ya miezi 12 wanapaswa kuwa na kipindi cha angalau dakika 60 za kucheza nje kila siku. Watoto wachanga lazima watoke nje angalau mara moja kwa siku.

**4.** Hali ya hewa ikiwa hatari kwa Watoto kwa mujibu wa shirika la Child Care Weather Watch na Kielezo cha Ubora wa Hewa, shughuli za jumla za mwendo zitabadilishwa na kuwa za nje.

**5.** Televisheni, kutazama video, na/au matumizi ya kompyuta au vifaa vya kielektroniki vya mkononi yatakuwa ya kielimu, mwafaka kwa umri na yasizidi saa moja kila siku. Wakati shule zimefungwa kwa dharura, watoto wa umri wa kwenda shule wanaweza kutumia vifaa vya kielektroniki kwa elimu ya mbali kwa muda unaohitajika ili kukidhi matarajio ya kielimu yanayohitajika.

**6.** Shughuli lazima zifae kiukuaji.

**C.** **Viwango vya kuridhisha vya madini ya risasi**. Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima vitii sheria ya 22 MRS Ch. 252 ya Udhibiti wa Sumu ya Madini ya Risasi, kuhusu matumizi ya rangi yenye madini ya risasi kwenye vifaa vya kuchezea, samani au sehemu zozote za ndani au za nje.

**1.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto vitafanya uchunguzi kila mwaka kubaini hatari zinazoweza kutokea kutokana na rangi iliyobambuliwa na/au kuchibuka.

**2.** Kituo hakitajumuishwa kwenye uchunguzi huu ikiwa:

**a.** Jengo lake lilijengwa mwaka 1978 au baadaye;

**b.** Jengo lake limeidhinishwa kuwa halina hatari za madini ya risasi na halina rangi iliyotengenezwa kwa madini ya risasi ndani ya miezi 12 iliyopita;

**c.** Hali ya usalama dhidi ya madini ya risasi imedumishwa kupitia tathmini mpya iliyofanywa miezi 6 baada ya uidhinishaji wa awali wa usalama dhidi ya madini ya risasi na kila mwaka baadaye kupitia kwa mkaguzi wa madini ya risasi au mtathmini wa hatari; au

**d.** Kituo hakiwahudumii Watoto walio na umri wa chini ya miaka sita.

**3.** Ukaguzi wa madini ya risasi unaofanywa na mkaguzi aliyeidhinishwa wa jimbo la Maine au mtathmini wa hatari lazima ukamilishwe ikiwa uchunguzi unaonyesha uwezekano wa uchafuzi wa rangi yenye madini ya risasi.

**4.** Iwapo ushahidi wa rangi yenye madini ya risasi utapatikana katika jengo lililojengwa kabla ya 1978, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwaarifu kwa kuwaandikia wazazi wa Watoto wote walio katika kituo, pamoja na familia zinazotarajiwa kujiunga kuhusu uwezekano wa uchafuzi wa rangi yenye

madini ya risasi. Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihifadhi katika rekodi ya kila Mtoto hati iliyoandikwa ya kukiri kupokea arifa inayohitajika hapa juu.

**5.** Urekebishaji wote wa rangi na vumbi yenye madini ya risasi lazima ufanywe kwa kufuata maadili ya kufanya kazi kwa usalama dhidi ya madini ya risasi kwa mujibu wa sheria ya 10-144 CMR Sura ya 292, Kanuni Zinazohusiana na Sheria ya Udhibiti wa Sumu ya Madini ya Risasi.

**D.** **Monoksidi ya kaboni.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima viwe na mfumo unaofanya kazi wa kugundua monoksidi ya kaboni.

**1.** Vifaa vinaweza kuwa vya kielektroniki (vya kuingiza au vya kuunganisha kwa waya) au vitambuzi vya monoksidi ya kaboni vinavyoendeshwa kwa betri ambavyo vinakidhi masharti ya Underwriters Laboratories Inc. (Ulioidhinishwa na UL); au mfumo wa kielektroniki wa kugundua monoksidi ya kaboni uliounganishwa kwenye mfumo wa kielektroniki wa kengele/kugundua moshi ambao umeidhinishwa na UL.

**2.** Angalau kigunduzi kimoja cha monoksidi ya kaboni lazima kisakinishwe kwenye kila ngazi ya kila jengo la Kituo cha Utunzaji wa Watoto na kitambuzi lazima kisakinishwe kwa mujibu wa Idara ya Usalama wa Umma ya Maine, Ofisi ya Kikosi cha Zimamoto cha Serikali au maagizo ya mwakilishi.

**E.** **Kiwangojoto cha jengo.**

**1.** Kiwango cha joto cha chini zaidi cha angalau 65º Farenhaiti kinachopimwa katika urefu usiozidi futi mbili kutoka sakafuni lazima kidumishwe katika nafasi ambapo Watoto wanaishi.

**2.** Ikiwa halijoto ya ndani ya nyumba inazidi 82º Farenhaiti, basi Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitumie mbinu za kupoza nafasi walipo Watoto.

**3.** Viyoyozi, vipepeo vya umeme na vipasha joto lazima vifungwe mbali na Watoto wote au viwe na ulinzi unaomzuia Mtoto yeyote kujeruhiwa.

**4.** Vipasha joto vinavyobebeka vinavyotumia umeme lazima viidhinishwe na Idara ya Usalama wa Umma ya Maine, Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto ya Jimbo au mwakilishi wake. Vipasha joto lazima vihifadhiwe kwa namna ya kuzuia majeraha na kuchomeka, na vipachikwe na kuendeshwa kwa mujibu wa mwongozo wa mtengenezaji.

**F.** **Mwangaza na Upenyezaji Hewa.**

**1.** Kila chumba kinachotumiwa na Watoto lazima kiwe na mwanga wa kutosha ili kuwezesha kutembea salama kupitia nafasi zake. Mwanga asili unahitajika katika chumba chochote kinachotumiwa na Watoto kwa zaidi ya saa nne kwa siku.

**2.** Nafasi zote za ndani zinazotumiwa na Watoto lazima ziwe na hewa ya kutosha.

**a.** Madirisha yanapaswa kufunguliwa wakati halijoto ya nje na ubora wa hewa ni mwafaka.

**b.** Milango na madirisha yanayotumiwa kuingiza hewa lazima yawe na vizibaji vilivyofungwa kwa njia salama.

**c.** Ni lazima kituo kirekebishe hali yoyote ya unyevunyevu inayosababisha ukungu, kuvu au harufu mbaya kabla ya Watoto kuishi katika nafasi hiyo.

**G.** **Nafasi ya Chini Zaidi Inayoweza Kutumika.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitenge nafasi isiyopungua futi mraba thelathini na tano (35) za inayoweza kutumika kwa kila Mtoto.

**1.** Maeneo ambayo hayapaswi kuhesabiwa kuwa mahali panapoweza kutumika ikiwa ni pamoja na, lakini si tu vifaa, shoroba za ukumbi, makabati, sehemu za kufungulia milango, hifadhi za bidhaa, veranda, bafu, nafasi za walimu, sehemu za kutayarishia chakula na ofisi.

**2.** Idadi ya juu zaidi ya Watoto wanaokaa katika chumba chochote haipaswi kuzidi masharti ya nafasi inayoweza kutumika kwa kila Mtoto wakati wowote, isipokuwa kwa shughuli za mara kwa mara za kikundi kikubwa kama inavyoonyeshwa katika ratiba iliyoandikwa.

**H.** **Sehemu za nje za kuchezea.** Kituo lazima kiwe na ufikiaji wa eneo la nje la kuchezea, lenye nafasi ya kutosha kuchezea Watoto wote kwa usalama, na mitaro ya maji inayozuia maji kusongamana.

**1.** Katika viwanja vya michezo vinavyonuiwa kuhudumia Watoto wa umri wote, mpangilio wa njia, uzio na mandhari ya uwanja wa michezo lazima uonyeshe maeneo tofauti ya makundi ya umri tofauti. Maeneo yanapaswa kutengwa kwa eneo la vizuizi, ikiwa ni pamoja na , lakini si tu, miti au madawati.

**2.** Ikiwa kuna hali za hatari katika eneo la michezo ya nje, Watoto lazima walindwe dhidi ya hali hizo kwa uzio au vizuizi vingine vinavyofaa.

**a.** Hali hatari ikiwa in pamoja na, lakini si tu, barabara, sehemu yoyote yenye maji, njia za reli zinazotumika, miinuko au matuta, au eneo lingine lolote hatari.

**b.** Uzio unapaswa kuwa na urefu wa angalau inchi 48. Eneo lolote lililofungwa lazima liwe na angalau lango moja, ambalo linafungwa kwa komeo ambao haiwezi kufunguliwa na watoto.

**c.** Lazima kuwe na njia ya kutoka uwanjani isipokuwa kupitia jengo.

**3.** Vifaa vya kuchezea vya ndani na nje lazima vipangwe ili kuwawezesha Wahudumu wa Watoto kuwaona Watoto wote wakati wote ili waweze kuwasimamia.

**4.** Kofia za usalama lazima zivaliwe ipasavyo kwa shughuli zote zenye hatari za kujeruhiwa kichwa (k.m. kuendesha baiskeli, skuta, viatu vyenye magurudumu, bao zenye magurudumu, bao za kuteleza kwenye theluji na/au magurudumu yanayotumia).

**5.** Kifaa chenye urefu unaozidi inchi 36 kwenye sehemu ya kupanda au kusimama kitakuwa na nyenzo za kufyonza nishati chini yake.

**a.** Nyenzo za kufyonza nishati zinajumuisha nyenzo za legevu za kujaza kama vile vibanzi vya mbao za uwanja wa michezo, kokoto njegere, vigae vya mpira au mikeka, au mchanga.

**b.** Nyenzo ya kufyonza nishati lazima ienee kando ya kifaa pande zote ili kuzuia majeraha mtoto anapoanguka.

**c.** Iwapo unatumia nyenzo za kufyonza nishati zisizo za kujaza, vifaa vyote vya kubembea, kukwea na kutelezea lazima viwe na kiasi cha kutosha cha nyenzo za kufyonza nishati ili kuzuia majeraha, kulingana na urefu wa kifaa.

**d.** Zege au lami haipaswi kutumiwa.

**6.** Vifaa mbalimbali vinavyofaa kwa umri na mahitaji ya Watoto wote wanaotunzwa lazima viwepo. Vifaa vya kubembea, kukwea na kutelezea lazima viwe:

**a.** Vimeegemezwa salama, vimesafishwa na kukarabatiwa ipasavyo na kujengwa kwa njia salama; na

**b.** Vimewekwa umbali wa kutosha ili kuzuia majeraha yanayotokana na sehemu zozote ngumu, ikiwa ni pamoja na nguzo, ua, vibanda na vifaa vingine vya kuchezea.

**7.** Eneo la kuchezea lazima lisiwe na vitu hatari na likaguliwe kwa macho kila siku, kabla ya Watoto kufika kwenye eneo hilo.

**8.** Masanduku ya mchanga au rundo la mchanga lazima lidumishwe katika hali salama na safi.

**9.** Maeneo ya michezo ya nje lazima yawe na kivuli.

**a.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitahakikisha kuwalinda Watoto dhidi ya miale mikali ya jua kwa kuwavalisha kofia au kuwapaka mafuta ya kujikinga dhidi ya jua (isipokuwa kama mzazi wa Mtoto ametoa maelekezo mengine).

**b.** Watoto wa umri wa chini ya miezi sita lazima walindwe dhidi ya miale ya jua ya moja kwa moja, na Wahudumu wa Watoto hawawezi kumpaka mafuta ya kumkinga dhidi ya miale ya jua isipokuwa mzazi wa Mtoto awasilishe pendekezo la daktari. Hati zilizoandikwa na daktari lazima zihifadhiwe kwenye faili ya Mtoto.

**10.** Idara haitaagiza kutengwa kwa nafasi ya kucheza nje katika mipango ya Shule za Chekechea, ikiwa mtaala unajumuisha angalau dakika 20 za shughuli za jumla za mwendo.

**11.** Katika Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinavyowahudumia Watoto 13 au zaidi, vikundi vya Watoto vinaweza kuwepo kwenye maeneo ya kuchezea kwa wakati mmoja ikiwa:

**a.** Uwiano wa Wahudumu na Watoto kwa kila kikundi unadumishwa kila wakati;

**b.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kina sera iliyoandikwa kuhusu michezo ya nje, ikiwa ni pamoja na:

**i.** Idadi ya juu ya Watoto ambao wanaweza kuwepo kwa wakati mmoja;

**ii.** Masharti mahususi ya usimamizi, kama vile kugawanya sehemu za kuchezea kwa Watoto wa umri tofauti; na

**iii.** Nafasi na shughuli za Wahudumu wa Utunzaji wa Watoto.

**c.** Wahudumu wote wa Watoto wamepewa mafundisho na wanatii sera za michezo ya nje.

**d.** Wazazi/walezi wote lazima wapokee nakala ya sera iliyoandikwa ya michezo ya nje.

**I.** **Silaha.** Bunduki, visu vya kuwinda, pinde na mishale, na silaha zingine haziruhusiwi kwenye majengo ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

**J.** **Nyenzo, Vinyago, Vifaa na shughuli.** Nyenzo, vinyago, vifaa na shughuli lazima ziwe zinafaa Kiukuaji na kitamaduni kwa Watoto waliosajiliwa.

**1.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kitoe vifaa vya kuchezea na kuhimiza kuandaliwa kwa shughuli za ndani na nje zinazolingana na vikundi mbalimbali vya umri na idadi ya Watoto.

**a.** Watoto wachanga: Aina za kutosha za vifaa vya kuchezea, muziki na vitabu vilivyoundwa ili kuchochea uvumbuzi, ukuaji wa misuli midogo na mikubwa, uratibu wa macho na mikono, na hisia za kuona, kusikia na kuhisi.

**b.** Watoto wachanga na Watoto wa umri wa kwenda shule ya chekechea: Aina mbalimbali za shughuli katika kila mojawapo ya maeneo yafuatayo: vitalu, mchezo wa kuigiza, lugha na kusoma, sanaa na ufundi, michezo na mazoezi ya kudhibiti (kama vile michezo ya bodi na mafumbo), shughuli za hisia (kama vile mchanga na maji), sayansi na maumbile, na muziki.

**c.** Watoto wa umri wa kwenda shule: Aina mbalimbali za shughuli katika kila mojawapo ya maeneo yafuatayo: vitabu na lugha, sanaa na ufundi, michezo, sayansi na maumbile, na muziki.

**2.** Vitu na vifaa vya kuchezea ambavyo vimerejeshwa na watengenezaji au Tume ya Marekani ya Usalama wa Bidhaa (CPSC) lazima viondolewe kwenye Majengo, virekebishwe, au vibadilishwe kulingana na maelezo yanayopatikana.

**3.** Kituo lazima kiwe na mavazi ya ziada ya Watoto, ikiwa mavazi yamechafuka, kuharibika au hayakutolewa kwa shughuli za siku hiyo.

**K.** **Vifaa.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na vifaa vinavyokidhi mahitaji ya Watoto wanaohudumiwa.

**1.** Nafasi ya binafsi na inayofikiwa kwa urahisi lazima itengewe kwa ajili ya mavazi ya Watoto ya kuchezea na vitu vyao vya binafsi.

**2.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kimpe kila Mtoto vifaa vyake vya usafi (mswaki wa meno, brashi ya nywele, kichana, n.k.) na vitu vya binafsi (taulo, glasi ya kunywea) ikiwa anahitaji kuvitumia.

**3.** Ikiwa kuna vifaa vya kuoga:

**a.** Watoto hawapaswi kuoga pamoja au kushiriki maji ya kuoga;

**b.** Hodhi au mifereji ya bafu inapaswa kusafishwa kabla ya kutumiwa na Mtoto mwingine;

**c.** Watoto lazima wapewe vitambaa na taulo safi; na

**d.** Hakuna Mtoto aliye chini ya umri wa miaka mitano atakayeachwa bila kusimamiwa akiwa ndani ya beseni au bafu.

**L.** **Vitanda vya watoto na matandiko.**

**1.** Kitanda cha kulala au cha kuchezea kinachokidhi viwango vya usalama vya Tume ya Usalama wa Bidhaa(CPSC), vinavyopatikana kwenye https://www.cpsc.gov/s3fs-public/5023.pdf, lazima itolewe kwa kila Mtoto wa umri wa hadi miezi 18.

**a.** Hakuna kitanda cha kulala au cha kuchezea kinachoweza kutumiwa kulala zaidi ya Mtoto mmoja kwa wakati mmoja.

**b.** Vitanda vya ghorofa mbili au nyingi haviruhusiwi.

**c.** Mikeka lazima iwe isiyopenyeza maji au inayoweza kuoshwa.

**d.** Kila kitanda lazima kiwe na godoro lisiloweza kupenyeza maji, thabiti na linalotoshea ambalo liko upana wa vidole viwili pande zote za fremu ya kitanda.

**e.** Vifaa vya aina yoyote vinavyozuia Watoto kutembea havipaswi kutumiwa kwenye vitanda.

**f.** Vitu vya kuchezea vikiwemo simu za mikononi na vifaa vya aina nyingine vya kuchezea ambavyo vimeundwa kuunganishwa kwenye sehemu yoyote ya kitanda havipaswi kutumiwa. Vitanda vyote vya kuchezea lazima vitumike pamoja na godoro asili au lingine lililopendekezwa na mtengenezaji.

**g.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinavyoweza kufikiwa lazima viwe na angalau kitanda kimoja cha magurudumu cha kuwaokoa watoto wachanga wasioweza kutembea. Vitanda vya kuchezea vyenye magurudumu havijaidhinishwa kutumika kama vitanda vya uokoaji.

**2.** Vitanda vya watoto wachanga vinavyokidhi viwango vya usalama vya CPSC vinaweza kutumika kwa watoto wachanga walio na umri wa hadi miezi mitano, wa uzito unaofaa. Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakiwezi kutumia vitanda vya watoto wachanga kwa mtoto ambaye anaweza kuinua kifua chake kutoka sehemu ya kulala bila kusaidiwa.

**3.** Vitanda vya kulala, vitanda vya watoto wachanga na vitanda vya kuchezea vya watoto wachanga walio na umri wa chini ya miezi 12 lazima viwe na matandiko laini au yaliyolegea ikiwa ni pamoja na, lakini si tu: pedi za kupunguza sauti, mito, pamba, vifariji, blanketi, vifaa vya kubadilisha mkao wa kulala, bibu au vitu vya kuchezea vilivyojazwa. Blanketi inayoweza kuvaliwa isiyozuia mikono na yiliyovaliwa ipasavyo inaruhusiwa.

**a.** Vitanda, mikeka, vitanda vya kuchezea na vitanda vya watoto wachanga lazima visafishwe na kunyunyizwa dawa ya kuua viini baada ya kutumiwa na Watoto tofauti, vinapochafuka, au angalau mara moja kwa wiki.

**b.** Magodoro yote ya vitanda vya kulala, vitanda vya watoto wachanga na vitanda vya kuchezea vitafunikwa kwa karatasi iliyotoshea vizuri.

**c.** Vitanda vya kulala, vitanda vidogo, vitanda vya kawaida, mikeka au vitanda vya kuchezea vinavyotumiwa kulala lazima vipangwe kwa njia ambayo itahakikisha kwamba vimetenganishwa kwa angalau futi 2 ili kuwawezesha watu kutembea kati yake vinapotumika, au vitenganishwe kwa kigawanyaji kigumu upande mmoja.

**4.** Kila Mtoto wa umri wa chini ya miaka mitano anayetunzwa kwa muda wa zaidi ya saa nne shari apewe mkeka, kitanda au kitanda kidogo tofauti chenye blanketi au mfuko wa kulalia. Matandiko yote yanapaswa kusafishwa kabla ya kutumiwa na Mtoto mwingine. Matandiko yote lazima yasafishwe kama inavyohitajika, au angalau kila wiki.

**a.** Blanketi, mifuko ya kulalia, matandiko, vitanda na mikeka lazima vihifadhiwe kwa njia ambayo inahakikisha kwamba sehemu za kulala hazigusani au lazima zioshwe na kutiwa dawa kabla ya kutumiwa tena ikiwa zimehifadhiwa kwa njia inayowezesha sehemu za kulala kugusana wakati wa kuhifadhiwa.

**b.** Shuka za kulala lazima zioshwe au kubadilishwa kabla ya kutumiwa na Mtoto mwingine. Shuka za kulala na blanketi zote zinazoweza kuvaliwa lazima zisafishwe inavyohitajika, lakini zisizidi zaidi ya wiki moja.

**5.** Watoto hawapaswi kufungwa kwa nguvu katika blanketi na vichwa vyao visifunikwe wakati wa kulala au kupumzika.

**M.** **Vyoo.** Vifaa vya kuosha na vyoo vyenye maji moto na baridi ya mfereji pamoja na sabuni lazima viwepo kituoni.

**1.** Choo na beseni moja ya kuogea vinahitajika kwa kila Watoto ishirini (20), lazima viweze kufikiwa kwa urahisi na Watoto hawa, na kuwezesha usimamizi unaoendelea wa Watoto.

**2.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima viwe na sinki moja ya kunawia mikono katika kila eneo la kubadilishia nepi, iliyo sehemu ambapo usimamizi wa Watoto wote katika kikundi unaweza kuendelea.

**3.** Ngazi, jukwaa fupi au mbinu nyingine lazima iwekwe karibu na vyoo na beseni za kuogea, kwa ajili ya Watoto wanaohitaji usaidizi kuzifikia na kuzitumia.

**4.** Halijoto ya maji haipaswi kuzidi 120° Farenhaiti katika mifereji ya matumizi ya Watoto.

**5.** Bidhaa za karatasi zinazoweza kutupwa baada ya kutumiwa, au vitambaa na taulo safi zilizochaguliwa kibinafsi zinaweza kutumika. Vitambaa na taulo safi zilizochaguliwa kibinafsi lazima zifuliwe kila siku.

**N. Kutumia nepi/Kwenda choo**

**1.** Watoto lazima waangaliwe angalau kila baada ya saa mbili (2) kuhakikisha hawana nepi au nguo zilizo na unyevu au choo, na lazima zibadilishwe haraka iwezekanavyo.

**2.** Nepi zenye unyevu au choo zinazoweza kutupwa lazima ziwekwe kwenye pipa lenye karatasi ya plastiki na lenye kifuniko, na kutenganishwa na takataka au uchafu mwingine, na ziwe mbali na sehemu za kuchezea au za kutayarishia chakula, au kuwekwa kwenye mfuko binafsi na kufungiwa ndani ya pipa la takataka lenye mifuko kadhaa.

**3.** Shughuli ya kufunga nepi lazima ifanyiwe kwenye meza ya kubadilishia au mkeka wa plastiki unaoweza kuoshwa ambao husafishwa baada ya kutumika kila mara, au ambao una kifuniko cha kutumika mara moja.

**4.** Meza au mkeka wa kubadilishia nepi hauwezi kuwekwa jikoni au katika eneo la kuandalia chakula.

**5.** Wahudumu wa Watoto lazima wanawe mikono na kunawisha mikono ya Watoto kwa sabuni na maji yanayotiririka kila baada ya kubadilisha nepi.

**6.** Kwa Watoto wanaotumia nepi za vitambaa, nepi hii lazima iwe na kitambaa safi cha ndani, na kinachofyonza unyevu kilicho ndani ya nyenzo ya nje isiyopenyeza maji ambayo huzuia kinyesi na mkojo kutoka.

**a.** Nepi na nyenzo hii ya nje lazima zibadilishwe kwa pamoja.

**b.** Nguo na nepi za nguo ambazo zimechafuliwa na mkojo au kinyesi lazima ziwekwe mara moja kwenye mfuko au chombo safi kinachoweza kufunikwa (bila kuoshwa, kutikiswa au kumwagwa) na zipelekwe nyumbani siku hiyo ili kusafishwa.

**c.** Mfuko au chombo hiki kinachoweza kufunikwa lazima kihifadhiwe mbali na Watoto.

**7.** Ni lazima kituo kishirikiane na familia ili kubaini kauni bora kuhusu choo kulingana na mahitaji ya kila Mtoto.

**8.** Vipokezi vya viti vya choo lazima vimwagwe uchafu wake mara tu baada ya kutumiwa, vioshwe na kusafishwa kwenye sinki isiyotumika kutayarishia chakula.

**9.** Vipokezi vya viti vya choo haviwezi kutumika katika eneo la kuandalia chakula.

**O. Wanyama vipenzi**

**1.** Wanyama vipenzi hawapaswi kuwa hatari kwa Watoto.

**2.** Jengo lazima lisiwe na taka ya wanyama vipenzi au wanyama wengine, na sehemu ya ndani ya kituo lazima isiwe na harufu ya taka ya wanyama.

**3.** Masanduku ya taka ya wanyama vipenzi hayapaswi kuhifadhiwa katika sehemu za kutayarishia au kupakulia chakula, na lazima yafunikwe ili Watoto wasiguse taka hii.

**4.** Wanyama vipenzi wote lazima wachanjwe dhidi ya kichaa cha mbwa na rekodi ya chanjo ya kila mnyama kipenzi lazima ihifadhiwe kama ilivyobainishwa katika Sehemu ya 5 ya sheria hii.

**P. Mazoezi ya kutoroka moto**

**1.** Mazoezi ya kutoroka moto lazima yafanywe angalau mara moja kwa mwezi kwa Watoto na watu wazima wote walio kituoni kwa kutumia angalau njia mbili (2) za kutoka. Rekodi ya mazoezi yote ya kutoroka moto lazima iwekwe kama ilivyoainishwa katika sehemu ya 5 ya Sheria hii.

**2.** Mazoezi ya kutoroka moto lazima yafanywe kulingana na sera na taratibu ambazo zimewekwa katika kila chumba kinachotumiwa na Watoto.

**3.** Kengele za kuvuta au vigunduzi vya moshi lazima vitumike, inapowezekana, kufanya mazoezi ya kutoroka moto.

**Q. Mpango wa kujiandalia jambo la dharura.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima viwe na mpango ulioandikwa wa kujiandalia jambo la dharura iwapo utatokea moto, maafa ya asili, au hali nyingine ya kutisha ambayo inaweza kusababisha hatari ya kiafya au kiusalama kwa Watoto katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto. Wahudumu wa Watoto lazima wakague mpango wa kujiandalia jambo la dharura kila mwaka na kusasisha mafundisho inapohitajika. Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima vihifadhi nakala iliyosasishwa ya mpango wa kuhamishwa na kumpa maelezo ya taratibu za dharura za kuhamishwa kila Mzazi au Mlezi wa Kisheria wa Mtoto wakati wa kumsajili Mtoto kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto na wakati wowote mpango unasasishwa.

**1.** Mpango lazima utoe mipango ifuatayo:

- **a.** Uhamishaji, ikiwa ni pamoja na kituo maalum ya kuhamishiwa, na njia ya uokoaji;
- **b.** Uwezo wa kufungwa kwa kituo au makazi kwa dharura;
- **c.** Taratibu za kuwafahamisha Wazazi/walezi wa Kisheria;
- **d.** Taratibu za kushughulikia mahitaji ya Watoto binafsi wakiwemo Watoto wenye mahitaji maalum;
- **e.** Kushirikiana na maafisa wa usimamizi wa dharura wa ndani; na
- **f.** Mwongozo wa kuendelea na huduma za utunzaji wa Watoto katika kipindi cha baada ya jambo la dharura au maafa.

**2.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kifanye zoezi la uokoaji angalau mara mbili kwa mwaka na tarehe hizi lazima zirekodiwe na ziweze kupatikana ili kukaguliwa. Mazoezi ya kuiga unakubalika.

**3**. Wahudumu wote wa Watoto lazima wafunzwe na kufahamu mpango wa maandalizi ya dharura.

## SEHEMU YA 15. KUOGELEA NA KUETEMBEA MAJINI

**A.** **Sera kuhusu shughuli za ndani ya maji na taratibu za usalama**. Usimamizi wa moja kwa moja na wa karibu wa Watoto unahitajika wakati wote, unaofanywa na Wahudumu wa Watoto walio karibu ili kuwezesha kutoa usaidizi na kuweza kuwaona na kuwasikia Watoto wote walio katika eneo la kuogelea au kutembea ndani ya maji.

**1.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinachotoa shughuli za kuogelea au kutembea majini lazima kiandae sera na taratibu kuhusu shughuli za kuogelea na kutembea majini, na taratibu za usalama.

**2.** Sera na taratibu lazima zijumuishe shughuli zote za kuogelea au kutembea majini zinazofanyika katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto na pia nje ya kituo, kwa mfano, kwenye Bwawa la kuogelea la umma au ufuoni.

**3.** Sera na taratibu lazima zijumuishe mpango wa dharura ulioandikwa unaohusiana na shughuli zozote za kuogelea au kutembea majini, licha ya mahali zinafanyika. Mpango huu lazima upatikane kwa Wahudumu wote. Mpango huu lazima ujumuishe taratibu za dharura za matibabu, dharura zinazosababishwa na kemikali, kuzama majini, hali mbaya ya hewa na kuthibitisha mara kwa mara kwamba Watoto wote wako salama.

**B.** **Ruhusa ya mzazi**. Kabla ya kuruhusu Mtoto kushiriki shughuli za maji, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na ruhusa iliyoandikwa na Mzazi au mlezi wa Kisheria. Angalau kila mwaka, ni lazima fomu iliyoandikwa ya ruhusa ya Mzazi isasishwe, iwekwe saini na kuandikwa tarehe na Mzazi au mlezi wa Kisheria. Fomu ya ruhusa ya Wazazi iliyotiwa saini na tarehe lazima iwekwe katika faili inayotunzwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa rekodi za kila Mtoto. Fomu ya ruhusa ya Mzazi lazima ijumuishe:

**1.** Jina la Mtoto na tarehe ya kuzaliwa;

**2.** Shughuli za maji zinazotolewa;

**3.** Uwezo wa kuogelea wa Mtoto;

**4.** Mahali ambapo shughuli za maji zinafanyika;

**5.** Kuwepo au kutokuwepo kwa mlinzi; na

**6.** Sahihi na tarehe ya Mzazi.

**C.** **Sehemu.** Vifaa vyote vya kuchezea ndani ya maji lazima viwekwe kwenye nyasi au nyenzo inayofyonza nishati vinapotumika.

**D.** **Kiwango cha chini cha mafundisho na leseni inayohitajika kwa shughuli za maji.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na wahudumu wa maji waliopewa mafundisho sahihi, kama inavyofafanuliwa na sheria hii, wawepo kila wakati katika mafundisho ya kuogelea au shughuli zingine za kuogelea au kutembea ndani ya maji.

**1.** Mabwawa ya kutembea ndani. Watoto lazima wakatazwe kuingia kwenye Bwawa la Kutembea Ndani ya Maji ikiwa hakuna uangalizi wa Mhudumu wa Kutembea Ndani ya Maji.

**2.** Mabwawa ya Kuogelea. Watoto lazima wakatazwe kuingia kwenye Bwawa la Kuogelea lolote au lenye upana zaidi ya Bwawa la Kutembea Ndani ya Maji ikiwa hakuna uangalizi wa Mhudumu wa Usalama wa Maji.

**3.** Mlinzi Aliyethibitishwa. Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinavyotoa shughuli za kuogelea kwenye maeneo yenye maji ya kina cha zaidi ya inchi 48 wakati wowote lazima vihakikishe kuwa Mlinzi Aliyeidhinishwa anahudumu wakati wa shughuli ya kuogelea. Nakala ya Cheti cha sasa cha Mafundisho ya Mlinzi lazima iwe imehifadhiwa kwenye mpango huu.

**E.** **Usafi**. Mabwawa ya Kuogelea lazima yawe na uwazi wa kutosha. Sehemu ya chini ya Bwawa lazima iweze kuonekana wazi katika sehemu yenye kina kikuu zaidi. Mabwawa ya kuogelea lazima yawe na mfumo wa kuchuja na/au kusafisha maji kwa dawa. Mabwawa ya kutembea ndani ya maji lazima yasafishwe na kuondolewa maji kila siku, na inavyohitajika ili kuondoa uchafu unaoonekana.

**F.** **Ufikiaji wa Bwawa**.

**1.** Mabwawa yote ya kutembea ndani ya maji lazima yaondolewe maji wakati hayatumiki.

**2.** Hodhi za maji moto lazima zilindwe kwa uzio au vizuizi vilivyofungwa ili kuzuia Watoto kuzifikia.

**3.** Mabwawa yote ya kuogelea ya ardhini yaliyo katika maeneo yanayofikiwa na Watoto lazima yawe na uzio. Uzio lazima uwe na urefu wa futi nne na Lango linalofungwa.

**4.** Mabwawa ya Kuogelea yaliyo juu ya ardhi lazima yawe na kuta zenye urefu wa angalau futi nne ambazo watoto hawawezi kupanda, au lazima zizungukwe kwa uzio wa angalau futi nne kwa urefu na kulindwa kwa Lango linalofungwa. Wakati Bwawa halitumiki, lazima ngazi ziondolewe kwenye Bwawa au kulindwa vinginevyo ili kuzuia watoto kulifikia bila usimamizi.

**G.** **Mazoezi na taratibu za kujiandalia hali za dharura**.

**1.** Mabwawa yote lazima yawe na simu ya dharura katika eneo la Bwawa. Simu hizi lazima ziweze kupiga moja kwa moja kwenda kwa usaidizi wa dharura.

**2.** Mazoezi ya uokoaji wa dharura wa maji lazima ufanywe angalau mara moja kwa mwezi katika mwezi wowote ambao shughuli za maji hufanyika. Mazoezi haya lazima yafanywe kulingana na sera na taratibu, ambazo zinajumuisha matumizi ya vifaa vya usalama, uokoaji wa Watoto, mbinu za kidesturi za kuhakikisha Watoto wote wapo, na pia mawasiliano ya dharura.

**3.** Kituo lazima kiweke rekodi iliyoandikwa ya aina, tarehe, wakati na muda wa mafundisho na mazoezi.

**H.** **Uwiano wa Wahudumu na Watoto wakati wa shughuli za maji.** Uwiano wa Wahudumu na Watoto lazima udumishwe wakati wote katika shughuli za kuogelea na kutembea ndani ya maji.

**1.** Wahudumu wa Bwawa la Kutembea Ndani wanaweza kujumuishwa katika uwiano wa Wahudumu na Watoto. Wahudumu wa usalama wa maji, waokoaji na wakufunzi wa kuogelea hawawezi kujumuishwa katika uwiano wa Wahudumu na Watoto. Wahudumu wa usalama wa maji na Walinzi wa Maji Waliothibitishwa lazima wawe nje na karibu na Bwawa la Kuogelea.

**2.** Wakati Watoto wasiozidi watatu wako kwenye Bwawa la Kuogelea, mhudumu wa usalama wa maji anaweza kujumuishwa katika uwiano wa Wahudumu na Watoto. Mhudumu wa usalama wa maji lazima awajibikie kipekee wa usimamizi wa Watoto katika Bwawa la Kuogelea.

**3.** Ikiwa bwawa lina kina cha zaidi ya futi nne wakati wowote, ni Wahudumu wa Watoto wanaoweza kuogelea pekee ambao wanaweza kujumuishwa katika uwiano wa Wahudumu na Watoto.

**I.** **Mabwawa ya Kuogelea.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto vilivyo na Mabwawa ya Kuogelea kwenye majengo lazima vifahamu taratibu za dharura, matumizi ya vifaa vya usalama na mawasiliano ya dharura.

**1.** Wahudumu wa vituo lazima wakamilishe orodha ya ukaguzi wa usalama siku yoyote ambayo shughuli ya kuogelea imefanywa. Orodha ya ukaguzi itatolewa na Idara na lazima iwekwe saini na mtu anayewajibikia shughuli za kuogelea siku hiyo.

**2.** Kanuni za usalama zinazosomeka ambazo zinahusu matumizi ya Mabwawa ya Kuogelea ni lazima ziwekwe mahali panapoonekana wazi na lazima zisomwe na kukaguliwa kila wiki na kila Mhudumu wa Watoto anayehusika na usimamizi wa Watoto.

**J. Mabwawa ya nje ya kituo au hifadhi asili za maji**

**1.** Kwa shughuli za maji za nje ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto, Mlinzi Aliyeidhinishwa aliye kwenye zamu, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwasilishe mhudumu mmoja wa usalama wa maji kwa kila Watoto 20 waliopo.

**a.** Walinzi wa Maji walioidhinishwa hawapaswi kuhesabiwa kama wahudumu wa usalama wa maji. Wahudumu wa usalama wa maji hawapaswi kujumuishwa katika uwiano wa Wahudumu na Watoto. Wahudumu wa ziada wa Watoto lazima wawepo ili kutimiza masharti ya uwiano wa Wahudumu na Watoto.

**b.** Shughuli za maji katika maeneo asilia ya maji lazima ziandaliwe tu kwenye eneo mahususi lililoandaliwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa kutumia vizuizi vya ardhini na majini vinavyoonekana.

**2.** Kwa shughuli za maji za nje ya kituo au maeneo asili ya maji, Mlinzi Aliyeidhinishwa akiwa hayupo kwenye zamu, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwasilishe mhudumu mmoja wa usalama wa maji kwa kila Watoto 13 waliopo.

**a.** Wahudumu wa usalama wa maji na Walinzi wa Maji Walioidhinishwa hawapaswi kujumuishwa katika uwiano wa Wahudumu na Watoto. Wahudumu wa ziada wa Watoto lazima wawepo ili kutimiza masharti ya uwiano wa Wahudumu na Watoto.

**b.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinachotoa shughuli za maji kwenye maeneo asili ya maji au kwenye madimbwi yenye kina cha zaidi ya inchi 24 lazima kitume ilani iliyoandikwa kwa kila Mzazi wa Mtoto au Mlezi wa Kisheria kwamba hakutakuwa na mlinzi aliye kwenye zamu.

**c.** Wahudumu wasiopungua wawili ambao wana umri wa angalau miaka 18 lazima wawepo kila wakati katika shughuli za maji kwenye vyanzo asili vya maji.

**d.** Shughuli za maji katika maeneo asili ya maji lazima ziandaliwe tu kwenye eneo mahususi lililoandaliwa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto. Kabla Mtoto yeyote kuingia majini, Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihakikishe kuwa kizuizi, kama vile eneo lililofungiwa kamba na maboya kipo, ambacho kinaweka mipaka ya eneo la kuogelea kwenye ziwa au bwawa katika eneo lisilozidi futi 16 kwa upana katika mahali popote, na vitenganisho katika sehemu ya maji ambayo haina kina kinachozidi futi nne katika sehemu yoyote.

**K. Watoto Wasiojua Kuogelea**. Ni lazima watoto wote Wasiojua kuogelea watambuliwe wazi kwa njia inayoonekana na kutambuliwa kwa urahisi na Wahudumu wa Watoto, wahudumu wa usalama wa maji na Walinzi wa Maji Walioidhinishwa kama inavyotumika.

## SEHEMU YA 16. VIFAA VYA VYAKULA NA VYA JIKONI

**A.** **Vyakula na vitafunio vyenye virutubisho vyote.** Milo na vitafunwa vinavyotolewa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima viwe na lishe na usawa bora wa virutubisho. Kila mlo (kifungua kinywa, chakula cha mchana na cha jioni) na vitafunio vinavyotolewa na Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima vijumuishe virutubisho kama vile protini, bidhaa za maziwa, matunda na mboga, maji na nafaka**.**

**1.** Watoto lazima wapewe ufikiaji wa maji ya kunywa wakati wote.

**2.** Vitafunio mbalimbali vyenye lishe na vinavyojumuisha bidhaa za maziwa, matunda, maji, mboga na nafaka vitatolewa.

**3.** Lazima Watoto wapewe maziwa, maji au kibadala cha maziwa katika milo na vitafunio vyote.

**4.** Vipimo vya chakula vinavyotolewa lazima viendane na umri na hamu ya chakula ya Mtoto.

**5.** Wahudumu wanaweza kuwahimiza Watoto kujaribu vyakula vipya, lakini hakuna Mtoto atakayelazimishwa kula chochote asichotaka.

**6.** Vyakula visivyo na afya kama vile vyakula vyepesi, vyakula vya haraka na vyakula vilivyochakatwa sana vyenye chumvi au sukari nyingi ni vinaweza kutumiwa tu kwenye matukio maalum kama vile sherehe za likizo na sherehe za siku ya kuzaliwa. Soda haipaswi kutumiwa wakati wowote.

**7.** Wakia 4 hadi 6 pekee za juisi asili 100 isiyo na sukari nyongeza zinaweza kupewa Watoto wa umri wa zaidi ya miezi 12, mara isiyozidi moja kila siku.

**8.** Watoto lazima wapewe muda wa kula chakula chao, wasiharakishwe wakati wa mlo au vitafunio, na lazima wawe wameketi. Watoto lazima wasiruhusiwe kucheza, kutazama televisheni au kutumia vifaa vya kielektroniki wakati wa chakula au vitafunio.

**B.** **Kunawa mikono.** Watu wote wazima na Watoto wote lazima wanawe mikono punde kabla ya kuandaa au kulavitafunio na milo.

**C.** **Mizio.** Hati kuhusu mizio ya chakula waliyo nayo Watoto/madhara ya chakula kama ilivyothibitishwa na daktari lazima iweze kupatikana kwa urahisi na kukaguliwa na Wahudumu wote wanaohusika na utayarishaji na upakuaji chakula. Chakula lazima kitayarishwe kulingana na mpango ulioandikwa kwa kila Mtoto mwenye mzio wa chakula au anayeathiriwa na chakula. Mpango lazima ukaguliwe na kusasishwa jinsi mahitaji ya Watoto yanapobadilika au angalau mara moja kwa mwaka.

**D.** **Majukumu ya Wahudumu wa Utunzaji wa Watoto**

**1.** Wahudumu wa Watoto ambao wanaugua hawaruhusiwi kufanyia kazi katika eneo la kuandalia chakula. Wahudumu wa Watoto walio na vidonda wazi ambavyo haviwezi kufunikwa hawapaswi kushughulikia au kuandaa chakula.

**2.** Watoto wanaweza kuruhusiwa katika maeneo ya kutayarisha chakula tu wakati wanasimamiwa moja kwa moja na Mhudumu wa Watoto na hakuna hatari ya kujeruhiwa na vifaa vya jikoni.

**3.** Wahudumu na Watoto lazima waweze kuwaona na kuwasikia Watoto wote wakati wa kula chakula na vitafunio.

**4.** Mtoto hawezi kupewa chakula chochote kilichobakishwa na Mtoto mwingine.

**E. Hifadhi ya Chakula**

1. Vyakula vyote vilivyochafuliwa, vilivyoharibika na vilivyoisha muda lazima vitupwe mara moja. Chakula au kinywaji cha mikebe iliyovimba, yenye kutu, iliyobondeka au inayovuja hakipaswi kuliwa na lazima kitupwe mara moja.

2. Vyakula vyote vinavyoharibika lazima vihifadhiwe katika halijoto inayolofaa

3. Jokofu lazima zidumishwe kwa halijoto isiyozidi 40° Farenhaiti. Kipimajoto kinapaswa kuwekwa kwenye jokofu kila wakati.

4. Friza lazima zidumishwe kwa halijoto isiyozidi 0° Farenhaiti. Kipimajoto kinapaswa kuwekwa kwenye friza kila wakati.

5. Chakula kilichohifadhiwa kwenye jokofu lazima kihifadhiwe kwa njia ambayo inawezesha mzunguko bora wa hewa baridi. Vyakula vyote lazima vifunikwe. Vyombo vya chakula vilivyo kwenye jokofu katika Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima viwe na lebo na tarehe. Vyombo vya masalio ya vyakula vinapaswa kutolewa ndani ya siku tatu baada ya kutayarishwa.

6. Chakula cha mchana kilicho kwenye visanduku/mikoba au chakula kingine kinachotoka kutoka nje ya mpango lazima kiwekwe kwenye jokofu ikihitajika.

**F. Maandalizi ya Chakula**

1. Vyakula vilivyogandishwa lazima vinganduliwe kwenye jokofu au kwa maji baridi ya mfereji. Vyakula vilivyogandishwa ambavyo vimeganduliwa kwenye maikrowevu lazima vipakuliwe papo hapo au kutayarishwa ili kupakuliwa.

2. Matunda na mboga mbichi lazima yaoshwe vizuri kabla ya kutumiwa.

3. Chakula, ikiwa kimepashwa joto, lazima kitolewe kwa Watoto baada tu ya halijoto yake chakula hiki kuchanganywa, kukorogwa na kukaguliwa ili kuzuia kuwachoma watu.

**G. Vifaa na Vyombo**

1. Sehemu zote za kuandalia na kulia chakula lazima zisafishwe kabla na baada ya matumizi.

2. Sahani na vyombo lazima vioshwe kwenye mashine ya kiotomatiki au vioshwe kabisa kwa maji moto ya sabuni na kusuzwa kwa maji moto.

3. Bidhaa za karatasi lazima zitumiwe mara moja na lazima zitupwe baada ya kutumiwa.

4. Vyombo vya kutumiwa mara moja lazima vitumike mara moja tu.

**H. Vifaa vya jikoni**

1. Maeneo ya jikoni lazima yawe na mwanga wa kutosha, yadumishwe yakiwa safi na kupandwa taratibu.

2. Sehemu ya kutayarishia chakula halipaswi kutumika kwa shughuli nyingine wakati chakula au kinywaji kinatayarishwa au kupakuliwa.

3. Vyakula na vinywaji vyote moto lazima viwekwe mbali na Watoto. Mhudumu ambaye anapika au kunywa kinywaji moto hapaswi kuwapakata Watoto.

**4.** Katika Vituo vya Utunzaji wa Watoto, wanyama vipenzi hawapaswi kuwekwa au kuruhusiwa katika maeneo ambapo vyakula au vinywaji vinatayarishwa.

**5.** Sinki sahihi zenye mifereji iliyoidhinishwa, pamoja na maji moto na baridi yenye ya shinikizo lazima yatolewe katika vyumba vyote ambapo vyakula au kinywaji hutayarishiwa, au vyombo kuoshewa. Bafu hazipaswi kutumiwa kuandalia vyakula, kusafisha chupa za watoto wachanga, au kuosha vyombo.

**6.** Sehemu zinazoguswa na vyakula au vinywaji lazima ziwe zinaweza kusafishwa kwa urahisi, zisiwe na vitu vingi, na zitengenezwe inavyofaa.

**7.** Vifaa vya jikoni lazima vidumishwe katika hali safi bila wadudu, panya na uchafu mwingine. Vyombo, vifaa na vyakula vyote lazima vihifadhiwe mahali safi, pakavu pasipo na wadudu, panya, na uchafuzi mwingine wowote, na lazima viandaliwe kwa namna ya kuzuia uchafuzi.

**8.** Mifereji ya maji chafu katika Mipango ya Utunzaji wa Watoto inayohudumia Watoto 13 au zaidi haifai kuwekwa juu ya sehemu za kuandaa chakula, kuhifadhi au kupakulia.

**9.** Jokofu lazima lidumishwe katika hali safi, bila kuvu na vitu vinavyomwagika.

## SEHEMU YA 17. USAFIRISHAJI

**A.** **Masharti ya madereva.** Mtu yeyote anayewabeba kwa gari Watoto wanaopokea utunzaji kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima awe na leseni ifaayo ya kuendesha daraja la gari husika, kila mwaka awasilishe hati iliyosainiwa inayoidhinisha Idara kukagua rekodi za Ofisi ya Magari, apokee matokeo yanayostahiki kwa mujibu wa Ofisi ya Ukaguzi wa Magari, na kukamilisha mafundisho yaliyoidhinishwa na Idara ya usafiri wa Watoto kabla ya kuwabeba Watoto kwa gari na angalau kila baada ya miaka miwili.

**1.** Makosa yafuatayo yanamsababisha dereva kupigwa marufuku kuwabeba kwa gari Watoto wanaopokea utunzaji kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto wakati wowote yanapofanywa:

a. Hatia ya gari inayosababisha kifo,

b. Ukaidi wa kukataa kutii amri ya kusimama ya afisa sheria,

c. Mauaji ya jinai yanayotokana na kuendesha gari.

**2.** Makosa yafuatayo yanamsababisha dereva kupigwa marufuku kuwabeba kwa gari Watoto wanaopokea utunzaji kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto yanapofanywa ndani ya miaka mitano iliyopita:

a. OUI ya Jinai,

b. Kuendesha gari wakati leseni imesimamishwa au kughairiwa,

c. Kuendesha gari kwa namna inayohatarisha maisha,

d. Kukataa kutii amri ya kusimama ya afisa sheria,

e. Kuendesha kwa kasi ya jinai

**B.** **Uwezo wa gari usiopaswa kukiukwa.** Idadi ya watu wanaosafirishwa kwenye gari lolote haipaswi kuzidi uwezo wa kuketi kwenye gari, isipokuwa katika tukio la uokoaji na kuhamishwa kwa dharura kwenda kwenye kituo cha kuhamishiwa kilicho wazi.

**C.** **Usalama katika magari.**

**1.** Hakuna Mtoto atakayeruhusiwa kwenye gari lolote bila uangalizi wa Watu wazima.

**2.** Ni lazima Watoto wakae wakiwa wamefunga mikanda ya usalama au viti vya usalama vya Watoto kwa mujibu wa 29-A M.R.S. § 2081.

**3.** Masharti ya magari yaliyo hapa juu hayatatumika kwa magari ambayo hayaendeshwi na madereva wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto, kama vile mabasi ya shule, teksi na/au mashirika ya usafiri wa umma.

**4.** Watoto wanaosafirishwa kwa basi la shule ambao wana umri wa chini ya miaka 4 lazima waketi kwenye viti vya usalama vya Watoto kwa mujibu wa 29-A M.R.S. § 2081.

**5.** Silaha hazipaswi kusafirishwa kwa gari lolote ambalo linawasafirisha Watoto.

**D.** **Safari za Nyanjani**

**1.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima viwe na taratibu za kuwahesabu Watoto wote kila wakati.

**2.** Ni lazima Watoto wahesabiwe wakati wa kuondoka na kuingia Kituoni, na pia mara kwa mara wakati wa Safari ya Nyanjani.

## SEHEMU YA 18. UTUNZAJI WA WATOTO WACHANGA NA WAKUBWA

**A.** **Sheria za ziada za mpango zinazowahudumia watoto.** Kando na sheria zilizotangulia, Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinachowahudumia Watoto wa umri wa wiki sita hadi miezi 36 lazima kitii sheria za sehemu hii.

**B.** **Vizuizi vya ghorofa ya kwanza**. Watoto wa umri wa chini ya miaka miwili hawaruhusiwi kupita ghorofa za kwanza au ghorofa zenye mlango wa kutokea kwenye kiwango cha daraja.

**C.** **Kukuza mahitaji ya kimaendeleo.** Mahitaji ya kimaendeleo ya Watoto Wachanga na Watoto Wadogo lazima yakuzwe kwa njia zifuatazo:

**1.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kihakikishe kwamba Watoto Wachanga na Watoto Wadogo wanapewa shughuli mbalimbali ili kukuza maendeleo sahihi katika nyanja zote za kujifunza, kulingana na mahitaji ya kimaendeleo ya kila Mtoto.

**2.** Kila Mtoto lazima aruhusiwe kuanzisha na kufuata ratiba yake mwenyewe ya kulala, kupumzika, na kuamka;

**3.** Watoto Wachanga na Watoto Wadogo hawapaswi kuruhusiwa kutumia vifaa vya kucheza au vitu wanavyoweza kumeza au kuwakaba koo. Watoto hawapaswi kupewa vyakula ambavyo vina hatari ya kuwakaba kwa sababu ya ukubwa, umbo au ugumu;

**4.** Mkao wa kila Mtoto Mchanga lazima ubadilishwe kila dakika 30, wakati Mtoto ameamka;

**5.** Watoto Wachanga lazima wapewe vipindi vya mazoezi ya tumbo kila siku wakisimamiwa;

**6.** Matumizi ya vifaa vya Watoto Wachanga ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, vifaa vya kurukia na kubembea, ambavyo watoto hawaruhusiwi kutumia kwa zaidi ya dakika 30 mfululizo; na

**7.** Watoto wachanga na watoto wadogo wanaweza kupangwa katika kikundi tu ikiwa jumla ya idadi haizidi Watoto 8.

**D.** **Kula**

**1.** Vyombo vya maziwa ya mama lazima viandikwe jina la Mtoto, yawekwe tarehe na kuhifadhiwa au kutupwa kwa mujibu wa maelezo yaliyo kwenye jedwali lililo hapa chini.

| Mahali pa Kuhifadhi na Halijoto | | | |
|---|---|---|---|
| Aina ya Maziwa ya Mama: | Rafu<br>77°F (25°C) au baridi zaidi (halijoto ya kawaida) | Jokofu<br>40°F (4°C) | Friza<br>0°F (-18°C) au baridi zaidi |
| Yaliyotolewa kwenye titi hivi punde | Hadi saa 4 | Hadi siku 4 | Ndani ya miezi 6 ni bora zaidi<br>Hadi miezi 12 inakubalika |
| Yaliyogandu liwa, Yaliyokuwa Yamegandishwa Awali | Saa 1–2 | Hadi Siku 1 (Saa 24) | USIWAHI kugandisha tena maziwa ya binadamu baada ya kuyeyushwa |
| Mabaki ya Chakula | Ikiwa mtoto hakumaliza chakula cha chupa, tumia ndani ya saa 2 baada ya mtoto kumaliza kula. | | |

**2.** Poda ya maziwa lazima itengenezwe kutokana na bidhaa zilizotayarishiwa viwandani. Michanganyiko ya poda ya maziwa iliyotengenezewa nyumbani imepigwa marufuku.

**3.** Maziwa poda na maziwa ya mama lazima viwe na tarehe na jina la Mtoto.

**4.** Tumia poda ya maziwa ndani ya saa 2 baada ya kutayarisha na ndani ya saa 1 kutoka wakati ulianza kumlisha. Ikiwa poda ya maziwa ya Watoto Wachanga iliyoandaliwa haitatumika ndani ya saa 2, hifadhi chupa mara moja kwenye jokofu na uitumie ndani ya saa 24.

**5.** Kiasi na ratiba ya lishe lazima ikidhi mahitaji ya Mtoto.

**6.** Wahudumu wa Watoto lazima wawapakate Watoto Wachanga ambao hawawezi kujinyonyesha chupa ili wawalishe.

**7.** Watoto wanaojinyonyesha chupa lazima wawe wameketi na wanaoweza kufikiwa na Wahudumu wa Watoto.

**8.** Ikiwa maziwa ya mama au ya poda yanapashwa moto, chupa lazima ziwekwe kwenye maji ya moto (sio ya kuchemsha) kwa muda usiodizi dakika tano, baada ya hapo chupa lazima itikiswe vizuri, na kiwangojoto kupimwa kabla ya kumlisha. Chupa za posa au maziwa ya mama hazipaswi kupashwa joto kwenye maikrowevu.

**9.** Kiti au meza inayotumika kulisha Watoto Wachanga na watoto wadogo lazima iwe imetengenezwa kwa muundo hivi kwamba Mtoto hawezi kuteleza au kuanguka.

**10.** Sahani na chupa zinazotumiwa kulisha watoto lazima ziwe zimetengenezwa kwa nyenzo zisizoweza kuvunjika, au zifunikwe kwa nyenzo ambayo huzuia kuvunjika na isiwe na kemikali ya bisfenoli A (BPA).

**11.** Wazazi lazima wajulishwe mara moja ikiwa Mtoto amenyweshwa maziwa ya mama ya Mtoto mwingine kwa bahati mbaya. Vituo vya Utunzaji wa Watoto lazima viwe na taarifa kuhusu vipimo vya ufuatiliaji na kushiriki matokeo.

**12.** Mikebe ya chakula iliyofunguliwa awali haitakubaliwa katika Kituo cha Utunzaji wa Watoto. Mikebe yote ya chakula cha watoto kilichoandaliwa viwandani itakuwa na lebo ya tarehe iliyofunguliwa na wahudumu wa kituo. Vyombo vyote vya vyakula vya watoto vilivyotengenezwa nyumbani vina lebo ya tarehe iliyopokelewa na kituo. Chakula chochote ambacho hakijatumika kitatupwa baada ya muda usiozidi siku mbili (2) kufuatia tarehe ya kufunguliwa au tarehe ya kupokea chakula cha watoto kilichotengenezwa nyumbani. Chakula cha watoto cha kutengenezwa nyumbani ambacho kimegandishwa lazima kitupwe baada ya mwezi mmoja ikiwa hakitatumiwa.

**E.** **Kulala/Kupumzika.** Kituo lazima kitii masharti ya Kifungu cha 14(L) cha sheria hii, na:

**1.** Ni lazima Watoto Wachanga walazwe kwa migongo yao katika kitanda kidogo kilichoidhinishwa, kitanda cha kulala, au kitanda cha michezo wanapolala, isipokuwa mzazi wa Mtoto akitoa mapendekezo tofauti ya daktari. Hati zilizoandikwa na daktari lazima ziwekwe kwenye faili ya Mtoto.

**2.** Kila Mtoto/Mtoto Mchanga lazima aruhusiwe kufuata ratiba yake ya kulala/kupumzika, isipokuwa kama hati mahususi iliyoandikwa na daktari iko kwenye faili ya Mtoto.

**3.** Kinga ya kifuani na nguo zilizo na kamba au kofia lazima ziondolewe kabla ya kumweka mtoto kitandani ili kulala.

**4.** Hairuhusiwi kuwafunga Watoto kwa vitambaa vilivyokazwa

**5.** Vitanda vya kulala na vya kuchezea vinaweza tu kutumiwa na Mtoto mmoja kwa wakati mmoja.

## SEHEMU YA 19. UTUNZAJI WA WATOTO WA USIKU

**A.** **Sheria za ziada za utunzaji wa usiku.** Kituo kinachopokea Watoto kwa ajili ya utunzaji wa Usiku lazima kitii masharti ya sehemu hii, pamoja na sehemu nyingine za kanuni hii.

**B.** **Utunzaji wa watoto binafsi.** Juhudi maalum lazima zifanywe na Kituo cha Utunzaji wa Watoto ili kuhakikisha utunzaji wa wakati wa kulala na kuamka umemfaa kila Mtoto binafsi.

**1.** Wahudumu wa Watoto lazima wawe macho, watoe usimamizi ufaao, na wamakinikie mahitaji ya Watoto.

**2.** Katika Vituo vya Utunzaji wa Watoto, angalau wafanyakazi wawili lazima wawe katika mpango wakati wote katika saa ambazo utunzaji wa usiku unafanywa.

**C.** **Vyumba vinavyotumika kulala au kupumzika**. Vyumba vyote vinavyotumiwa kulala au kupumzika lazima viidhinishwe na Ofisi ya Msimamizi wa Zimamoto wa Jimbo.

**1.** Chumba kilicho juu ya ghorofa ya kwanza kinaweza kutumika kulala au kupumzika ikiwa chumba hicho kina njia mbili za kutokea, huku njia moja ikiwa ya kutoka ikielekea nje moja kwa moja, na njia ya kufikia ghorofa ya chini kwa usalama.

**2.** Kituo cha Utunzaji wa Watoto lazima kiwe na kibali kilichoandikwa kutoka kwa Mzazi wa kila Mtoto anayetunzwa, licha ya umri wake, akiruhusu mtoto wake ashiriki chumba cha kulala na Mtoto mwingine. Watoto wa umri wa kwenda shule lazima watengewe maeneo ya kulala ya jinsia maalum na maeneo ya kibinafsi ya kuvalia. Ndugu na dada wa jinsia tofauti wanaweza kulala sehemu moja kwa idhini iliyoandikwa ya mzazi.

**D.** **Vitanda na matandiko.** Kituo kinachotoa huduma ya usiku lazima kiwe na kitanda cha kulala ambacho ni salama na imara kwa kila mtoto mchanga, na kitanda salama na imara chenye godoro na mto kwa kila Mtoto mkubwa.

**1.** Vitanda vya ghorofa ya juu lazima viwe na reli ya usalama.

**2.** Vitanda vya maji havipaswi kutumiwa kwa Watoto wa umri wa chini ya miezi 36.

**3.** Shuka lazima zibadilishwe kila wiki baada ya kutumiwa na Watoto tofauti, au mara nyingi zaidi ikihitajika. Hakuna Mtoto anayeruhusiwa kulala kwenye kitanda chenye unyevu.

**4.** Vitanda vilivyopangwa sambamba lazima viachane kwa angalau mita mbili.

**5.** Vitanda vya watoto wachanga lazima viwe vinazingatia Kifungu cha 14(L) cha sheria hii.

**6.** Mikeka haiwezi kutumika kulala usiku kucha.

## SEHEMU YA 20. MIPANGO YA UTUNZAJI YA WATOTO WA UMRI WA KWENDA SHULE NA HUDUMA ZA MARA KWA MARA

A. **Sheria za ziada za Vituo vya Utunzaji wa Watoto wa umri wa kwenda shule.** Kando na sheria zilizotangulia, Vituo vya Utunzaji wa Watoto wa Umri wa Shule lazima vitii sehemu hii. Vituo vya Utunzaji wa Watoto wa Umri wa Kwenda Shule zinajumuisha (A) vifaa vilivyoidhinishwa kwa watoto kumi na watatu (13) au zaidi ambavyo vinajumuisha Mpango wa Utunzaji wa Watoto wa Umri wa Kwenda Shule, na (B) vifaa vilivyoidhinishwa kwa watoto wasiozidi kumi na wawili (12) ambavyo vinawahudumia Watoto walio na umri wa kwenda shule pekee.

1. Lazima kuwe na nafasi, shughuli na vifaa vya shughuli za kikundi na watoto binafsi;

2. Shughuli zilizopangwa lazima ziakisi ufahamu wa mahitaji ya kijamii, kihisia, kimwili na kiakili ya Watoto wakubwa zaidi; na

3. Kituo lazima kiruhusu muda wa shughuli ya mtoto binafsi ambapo wanajielekeza.

4. Vituo vya Utunzaji wa Watoto wa umri wa kwenda shule vilivyo katika majengo ya shule za umma, kama inavyofafanuliwa na kuidhinishwa na Idara ya Elimu, havitahitajika kutii sheria zifuatazo.

   **a.** Sehemu za 2(A)(6)(a), 2(C)(7), na 2(C)(8) kuhusu kutii sheria;

   **b.** Sehemu ya 7(C)(3)(b) kuhusu haja ya kuwepo kwa wahudumu wawili;

   **c.** Sehemu ya 14(A)(1-2) kuhusu ngazi;

   **d.** Sehemu ya 14(D) kuhusu vitambuzi vya monoksidi ya kaboni; na

   **e.** Sehemu ya 14(F)(2)(b) kuhusu skrini.

B. **Mipango ya Utunzaji wa Mara kwa Mara.** Sheria za Ziada za Mipango ya Utunzaji wa Mara kwa Mara: Kando na sheria zilizotangulia, Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinavyotoa Huduma ya Mara kwa Mara lazima vitii sehemu hii.

1. Kituo lazima kiwe na utaratibu ulioandikwa ili kuhakikisha kwamba Mtoto amepokezwa kwa mtu anayemsajili Mtoto pekee au mtu mwingine aliyeidhinishwa na mzazi au mlezi aliyemsajili Mtoto huyo.

2. Mpango huu lazima uwe na njia ya kutambua kila Mtoto akiwa kituoni, kwa lebo ya jina au mbinu nyingine.

3. Mpango huu unaweza tu kutoa dawa za uokoaji kwa Watoto walio kituoni, na wakati tu vigezo vilivyo katika Sehemu ya 12(H)(1) vimetimizwa.

4. Mipango ya Utunzaji wa Mara kwa Mara haijumuishwi katika sehemu zifuatazo:

   **a.** Sehemu ya 5(D)(1)(c) na (d) kuhusu jina, na nambari ya simu ya mahali pa kazi pa wazazi); na

   **b.** Sehemu ya 5(D)(1)(j) kuhusu jina na nambari ya simu ya daktari wa Mtoto na daktari wa meno.

   **c.** Nakala ya makubaliano ya kifedha na Mzazi (wazazi) au Mlezi (Walezi) wa Kisheria.

   **d.** Sehemu ya 5(D)(1)(i) inayohitaji rekodi za chanjo

   **e.** Sehemu ya 5(D)(1)(h) Tarehe za kujisajili na kukomesha.

## SEHEMU YA 21. HAKI ZA UTEKELEZAJI, UTUMAJI MAOMBI TENA BAADAYE NA RUFAA

**A.** **Utekelezaji.** Idara inaweza kukiagiza Kituo chochote cha Utunzaji wa Watoto kutatua ukiukaji wowote kwa njia, na ndani ya muda uliowekwa, ambao Idara itaamua kuwa inafaa ili kuhakikisha kwamba sheria hii inafuatwa au kulinda afya na usalama wa Watoto. Idara inaweza kuchukua hatua moja au nyingi zilizobainishwa humu, katika kiwango chochote kinachofaa, ili kushughulikia ukiukaji wa sheria hii au sheria zinazotumika.

**B.** **Adhabu za Kiraia.** Idara inaweza kutathmini adhabu za kiraia kwa mujibu wa ratiba ya adhabu iliyoainishwa katika sheria hii, ikiwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitashindwa kutii sheria zinazotumika na/au kanuni hii.

**1.** Adhabu inaweza kukaguliwa kubaini kama kuna ukiukaji kama ilivyowekwa kwenye sheria hii.

**2.** Adhabu ya kiraia inatolewa kupitia Notisi ya Adhabu za Kiraia. Notisi itaeleza kila aina ya ukiukaji, kanuni au sheria ambayo imekiukwa na kiasi chochote kilichopangwa cha adhabu ya kiraia inayolingana na ukiukaji huo.

**3.** Idara imeweka ratiba ifuatayo ya adhabu za kiraia kwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa kushindwa kutatua ukiukaji kwa kufuata ratiba ya matukio ya Idara kwa mujibu wa 22 MRS §7702-A:

**a.** **Ukiukaji unaohusiana na rekodi/ufumbuzi**: $500.00 kwa kila ukiukaji.

**b.** **Ukiukaji unaohusiana na uwiano wa Watoto na wahudumu** – kiasi kischozidi $500/kwa kila tukio au $500/idadi ya Watoto iliyozidi kiwango kilichowekwa na sheria hii, au zote mbili.

**5.** Vituo vya Utunzaji wa Watoto vinatakiwa kulipa Idara kiasi cha adhabu ya kiraia ndani ya siku 30 baada ya kupokea Notisi ya Adhabu ya Kiraia. Ikiwa Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakijalipa jumla ya faini zinazodaiwa kabla ya kuchukua upya leseni, basi ombi la kuchukua upya leseni litakataliwa.

**6.** Kuweka adhabu ya raia hakuchukuliwi, kwa njia yoyote ile, kuwa sababu ya kuongeza makataa ya kutii sheria.

**C.** **Leseni yenye masharti.** Idara inaweza kutoa Leseni yenye masharti, Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaposhindwa kutii sheria na kanuni zinazotumika na, kwa uamuzi wa Idara, maslahi muhimu zaidi ya umma yatazingatiwa kwa kutoa leseni au kibali chenye masharti, kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazotumika na 22 MRS §7802(1)(C).

**1.** Notisi ya Leseni ya masharti itajumuisha Mpango wa Utendaji Ulioelekezwa, ambao lazima ubainishe ni lini na ni masahihisho gani yanapaswa kufanywa katika kipindi cha uidhinishaji au leseni yenye masharti.

**2.** Kukosa kukamilisha au kutii Mpango wa Utekelezaji Ulioelekezwa kunaweza kusababisha hatua zaidi kuchukuliwa, hadi, na kujumuisha kughairiwa kwa leseni.

**D.** **Kusitishwa kwa leseni.** Idara inaweza kusimamisha au kutafuta kusimamisha Leseni kama ifuatavyo:

**1.** **Kusimamishwa kwa Kiutawala/Agizo la Kufunga:** Kwa mujibu wa sheria ya 22 M.R.S. § 8301-A(5), wakati wowote ambapo kuna hali zinazohatarisha afya na usalama wa Watoto papo hapo, Kamishna anaweza kutoa amri ya kufungwa kwa kituo, ambayo itasimamisha leseni ya Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa hadi siku 10, ikisubiri uchunguzi zaidi au kabla ya kupokea amri ya kusimamishwa kwa dharura kutoka kwa mahakama. Idara itaagiza kwamba agizo la kufungwa liandikwe kwenye Kituo cha Utunzaji wa Watoto na kuwekwa hadharani kadri itakavyoamua kuwa itawafaa zaidi wazazi na wateja wengine watarajiwa.

2. **Kusimamishwa kwa Dharura:** Kwa mujibu wa sheria ya 22 M.R.S. § 7802(3)(C), wakati wowote, baada ya uchunguzi, masharti yanapatikana ambayo, kwa maoni ya Idara, yanahatarisha papo hapo afya na usalama wa watu wanaohudhuria Kituo cha Utunzaji wa Watoto, Idara inaweza kuiomba Mahakama ya Wilaya kutoa uamuzi wa dharura wa kusimamishwa kwa kituo kwa mujibu wa sheria ya 4 MRS §184 (6).

E. **Rufaa na Mamlaka ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.** Kwa mujibu wa sheria ya 22 M.R.S. § 7702-B(4), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina mamlaka ya kuwasilisha malalamiko katika Mahakama ya Wilaya kuomba adhabu ya kiraia au maagizo ya vizuizi, au yote mawili, wakati Idara inadai kuwa mtu, kampuni, ubia, chama, shirika au taasisi nyingine, kama inavyofaa hapa, inaendesha Kituo cha Utunzaji wa Watoto kama ilivyofafanuliwa katika sheria ya 22 M.R.S. § 8301-A(B) bila kupewa leseni kwanza.

1. Adhabu za kiraia: Kwa mujibu wa sheria ya 22 M.R.S. § 7702-B(3), adhabu ya kiraia haipungui $500 wala haizidi $10,000 kwa siku. Kila siku ya ukiukaji inachukuliwa kuwa kosa tofauti.

2. Maagizo ya vizuizi: Kwa mujibu wa sheria ya 22 M.R.S. § 7702-B(3), bila kuzingatia masuluhisho mengine yoyote yanayotolewa na sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaweza kuomba amri ya kuagiza kufuata sheria ya 22 M.R.S. § 7702-B(1).

F. **Kukataa kutoa au kusasisha leseni.** Idara inaweza kukataa kutoa au kusasisha leseni wakati Kituo cha Utunzaji wa Watoto kitashindwa kutii sheria na kanuni zinazotumika. Notisi ya Kukataa kutoa au kusasisha leseni itakuwa iliyoandikwa, itaonyesha sababu za kukataa, na itatumwa kwa njia ya posta au kuwasilishwa kwa Mwombaji au Kituo cha Utunzaji wa Watoto.

G. **Kubatilishwa kwa Leseni.** Idara inaweza kubatilisha leseni kamili au ya muda kwa kukiuka sheria na kanuni zinazotumika za kufanya, kuruhusu, kusaidia au kuunga mkono vitendo vyovyote haramu katika uendeshaji wa Kituo cha Utunzaji wa Watoto au kwa kufanya vitendo au mwenendo unaoathiri ustawi wa Watoto wanaohudhuria Kituo cha Utunzaji wa Watoto kwa mujibu wa sheria ya 22 MRS §7802(3)(D).

H. **Kughairiwa kwa Leseni Yenye Masharti.** Idara inaweza kughairi Leseni yenye masharti Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaposhindwa kutii masharti ya Leseni.

I. **Makubaliano ya Idhini.** Idara inaweza kutoa Makubaliano ya Idhini badala ya vikwazo vingine rasmi. Ikiwa Makubaliano ya Idhini hayatafuatwa, Idara inaweza kuchukua hatua zaidi ya leseni.

J. **Kizuizi cha utumaji maombi tena baada ya kunyimwa au kughairiwa kwa leseni.** Kikomo cha muda kifuatacho kinatumika kwa ombi jipya baada ya kunyimwa au kughairiwa kwa leseni.

1. Wakati kituo kimenyimwa leseni au imeghairiwa wakati mmoja, Mwombaji au Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakiwezi kutuma tena ombi la Leseni kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kutekelezwa kwa uamuzi wa kunyimwa au kughairiwa kwa leseni ikiwa rufaa haijakatwa; au ikiwa rufaa imekatwa, kutoka tarehe ya kutekelezwa kwa uamuzi wa mwisho wa kamishna au amri ya mahakama ya ukaguzi, lolote litakalotokea baadaye.

2. Ikiwa kituo kimenyimwa Leseni au imeghairiwa mara mbili, mwombaji au Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakiwezi kutuma tena ombi la Leseni kwa muda wa miaka miwili kuanzia tarehe ya kutekelezwa kwa uamuzi wa pili wa kunyimwa au kughairiwa kwa leseni ikiwa rufaa haijakatwa kuhusiana na uamuzi huu; au ikiwa rufaa imekatwa, kutoka tarehe ya kutekelezwa kwa uamuzi wa mwisho wa kamishna au amri ya mahakama ya ukaguzi, lolote litakalotokea baadaye.

3. Ikiwa kituo kimenyimwa Leseni au imeghairiwa mara tatu, Mwombaji au Kituo cha Utunzaji wa Watoto hakiwezi kupokea Leseni nyingine ya utunzaji wa Watoto.

**K.** **Ombi la baadaye la Leseni kamili.** Ombi la baadaye la Leseni kamili linaweza kuzingatiwa na Idara baada ya mojawapo ya hatua zifuatazo, baada ya mapungufu yaliyoainishwa na Idara wakati hatua hiyo ilichukuliwa yatatuliwa:

1. Utoaji au ubatilishaji wa Leseni yenye masharti;
2. Marekebisho au maboresho ya Leseni;
3. Kukataa kutoa au kusasisha Leseni kamili.
4. Kughairiwa au kusimamishwa kwa Leseni kamili; au
5. Kukataa kutoa Leseni ya muda.

**L.** **Kutolewa kwa leseni kamili baada ya mapungufu kusahihishwa.** Ombi la Leseni kamili linaweza kuzingatiwa na Idara tu wakati mapungufu yaliyotambuliwa na Idara yametatuliwa.

**M.** **Haki ya kukata rufaa.**

1. Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaweza kukata rufaa ya hatua ya Idara na kuomba kikao cha kusikilizwa kiusimamizi kama ifuatavyo:
   - **a.** Rufaa lazima iwe imeandikwa na lazima ieleze suala/maswala mahususi yanayokatiwa rufaa.
   - **b.** Rufaa lazima ifanywe ndani ya siku 30 baada ya kupokea notisi ya hatua kulingana na haki ya kukata rufaa na lazima itumwe au ipelekwe kwa Mkaguzi wa Usikilizaji wa Idara.
   - **c.** Hatua zifuatazo ziko chini ya haki ya kukata rufaa:
     - **i.** Kunyimwa Ondoleo lililoombwa;
     - **ii.** Utoaji wa Leseni yenye masharti, ikiwa ni pamoja na marekebisho au maboresho ya Leseni, kupunguzwa kwa uwezo wa Leseni au kusitishwa kwa usajili mpya, kunapohitajika na Idara kwa kushirikiana na leseni yenye masharti;
     - **iii.** Kusitishwa kwa Leseni kwa Dharura;
     - **iv.** Kubatilishwa kwa Leseni yenye masharti;
     - **v.** Kukataa kutoa au kusasisha Leseni kamili.
     - **vi.** Adhabu za kiraia; au
   - **d.** Vitendo vilivyo chini ya haki ya kukata rufaa vitasimamishwa hadi Idara ifanye uamuzi wa mwisho wa wakala, isipokuwa ikiwa Leseni imesimamishwa chini ya Kifungu cha 21 (D)(1-2).
2. Kesi hiyo itaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Usikilizaji wa Utawala wa Idara katika 10-144 CMR Sura ya 1.
3. Kituo cha Utunzaji wa Watoto kinaweza kukata rufaa dhidi ya hatua ya mwisho ya wakala kwa Mahakama ya Juu.

## MAMLAKA YA KISHERIA NA HISTORIA YA UDHIBITI

**Kutokana na 10-148 CMR Sura ya 32 ya Sasa, Kanuni za Kuidhinishwa kwa Vituo vya Utunzaji wa Watoto:**

MAMLAKA YA KISHERIA
22 M.R.S.A. Sura ya 1673; 5 M.R.S.A. §8054; Uamuzi wa 2007 Sura ya 199

TAREHE YA KUTUMIKA:
Tarehe 20 Januari, 1980

ILIREKEBISHWA:
Tarehe 11 Machi, 1980 - Sehemu ya 4 (B)
Tarehe 16 Februari, 1982 - Sehemu ya 7 (iliongezwa)
Tarehe 04 Machi, 1986
Tarehe 11 Februari, 1987

GHAIRI NA UBADILISHE:
Tarehe 01 Desemba, 1991

ILIREKEBISHWA:
Tarehe 14 Mei, 1995 - Sehemu ya 2B

MAREKEBISHO YASIYO MAKUU:
Tarehe 11 Februari, 1998 - kuondolewa kwa §III rudufu

ILIREKEBISHWA:
Tarehe 01 Julai, 1998

MAREKEBISHO YASIYO MAKUU:
Tarehe 15 Machi, 2000 - halijoto iliyorekebishwa katika XVII(C)(6)(f), kubadilisha fonti, umbizo

ILIGHAIRIWA NA KUBADILISHWA:
Tarehe 12 Novemba, 2002 - kuwasilisha kipengee cha 2002-336

MAREKEBISHO YASIYO MAKUU:
Tarehe 03 Machi, 2003

ILIREKEBISHWA:
Tarehe 17 Agosti, 2004 - kuwasilisha kipengee cha 2004-318

ILIREKEBISHWA:
Tarehe 31 Januari, 2008 - kuwasilisha kipengee cha 2008-8
Tarehe 1 Juni, 2008 - kuwasilisha kipengee cha 2008-234 (DHARURA)
Tarehe 27 Agosti, 2008 - kuwasilisha kipengee cha 2008-382

**Kutokana na 10-148 CMR Sura ya 36 ya Sasa, Kanuni za Kuidhinishwa kwa Shule za Chekechea:**

TAREHE YA KUTUMIKA:
Tarehe 30 Julai, 1976 (Iliwasilishwa tarehe 15-1-80)

ILIGHAIRIWA NA KUBADILISHWA:

Tarehe 14 Mei, 1995

Tarehe 27 Septemba, 2004 – kuwasilisha kipengee cha 2004-271. Pia ilibadilisha jina la sura kutoka "Kanuni za Idhini ya Kuendesha Shule ya Chekechea au Huduma ya utunzaji ya Watoto Iliyosajiliwa" hadi "Kanuni za Utoaji wa Leseni kwa Shule za Chekechea"

MAREKEBISHO YASIYO MAKUU:

Tarehe 2 Machi, 2005 - tahajia, nafasi na herufi kubwa pekee